

““Tegemea mambo makuu kutoka kwa Mungu.
Thubutu mambo makuu kwa ajili ya Mungu” William Carey



Hatua
ZA
UAMSHO
BINAFSI

Kujazwa Roho Mtakatifu

HELMUT HAUßEIL

Mchapishaji:

Asilia: "Schritte zur persönlichen Erweckung"

TOP Life Wegweiser-Verlag GmbH, Wien

Austrian Publishing House

Verlagsarchivnummer: 040 415

(asilia) ISBN: 978-3-903002-14-2

Matoleo ya Kiswahili - Yamechapishwa:

Mchapishaji: Kibidula (Family Development International)

SLP 17, Mafinga, Tanzania

ISBN: 978-9987-726-17-2

Usanifu: Simon Eitzenberger, www.desim.de

Msanidi: Konrad Print & Medien, www.konrad-medien.de

Usimamizi wa mradii: Christian Stroeck

Upigaji picha: Henry Stober

Ufasiri kutoka from the English edition: Kibidula Publishing Department

Mawasiliano na oda katika lugha za kigeni:

© Helmut Haubeil, Rosenheimer Str. 49

D-83043 Bad Aibling / Oberbayern – Ujerumani

Barua-pepe: helmut@haubeil.net au kikirejeshwa.helmut@haubeil.com

Simu: +49 (0)8061 4900 712

Fasiri:

Toleo la asili ni kwa Kijerumani

Lugha za Ulaya

Kibulgaria, Kikorasia, Kicheki, Kidenmaki,

Kiingereza, Kifaransa, Kihungaria, Kiitaliano,

Kilativia, Kinorwe, Kipolandii, Kireno, Kiromania,

Kirusi, Kiserbia, Kislovenia, Kihispania, Kiswideni.

Katika Maandalizi: Kialbania, Kifaransa-Kanada,

Kiduchi.

Lugha za Asia

Bahasa-Indonesia, Kichina (China, Singapo),

Kifilipino - Ufilipino, India: Kihindi, Kitelugu, Kiodia,

Kimizo, Kitai: Tailandi, Kiurdu-Pakistani,

Kivietnamu – Katika Maandalizi: Bahasa-Malesia,

Farsi (Irani), Kimongolia, Kitonga – Visiwa nya Tonga

Tovuti:

www.steps-to-personal-revival.info na www.schritte-zur-persönlichen-erweckung.info

hana kutakuwa na lugha zote zilizofasiriwa kwa ajili ya kusoma, kuprinti, kutuma kwa rafiki.

Dondoo muhimu: Shuhuda (zaidi ya 100), Maendeleo (Ambapo Bwana aliandaa kitabu), Jinsi gani

ya kuamsha shauku? Nukuu za Roho Mtakatifu (zimechaguliwa), Kiongozi (Dondoo kwa ajili ya

Kiongozi na uzoefu mahususi), Waeleze Watu (tuna uwezekano gani?), Mawasiliano. Pia kuna kitabu

kwa ajili ya ufuatiliaji: 'Abide in Jesus'.

Taarifa za Oda:

Kwa ajili ya vipengele nya kina, angalia ukurasa wa 2

Isipokuwa kama imedokezwa vinginevyo, nukuu zote za Maandiko zimechukuliwa kutoka katika Biblia ya Swahili Union Version. Hakimiliki 1952, 1997 Chama cha Biblia cha Kimataifa. Haki zote zimehifadhiwa ulimwenguni kote. Imetumika kwa ruhusa ya Chama cha Biblia cha Kimataifa.

HATUA
ZA
UAMSHO BINAFSI

K U A G I Z A

TANZANIA

Kibidula
SLP 17
Mafinga
Tanzania

USA

Remnant Publications
649 E. Chicago Rd
Coldwater MI, 49036
Phone 800-423-1319
or 517-279-13043
Web address for orders:
www.remnantpublications.com
Available at your Adventist Book Centers

Canada

Lucas Jurek
118 G First Avenue North
Williams Lake, BC
V2G 1Y8
Email: lucasjurek@gmail.com
Mobile number: 250 983 - 2650

Australien

Colin Hone
Booklets in English
colin.hone@murrayhone.com.au

Philippines

Allan D. Faina
Email: berevived714@gmail.com
SDA church
Fidela Herrera Subd
Bgy. Santol, Tanza, Cavite-4108
Phones: (63) 926 054 1175

Russia

Source of Life Publishing House
Vostochnaya St. 9, Zaoksky 301000
Tula Region, Russia
Tel. +78 73 42 01 01
www.lifesource.ru

Europe - Russian - language literature

Christa Medien GmbH
Pulverweg 6
D-21337 Lüneburg (Germany)
Tel. +49 (0)4131 9835-580
www.christa-medien.eu
und www.christa-shop.eu
E-Mail: info@christa-medien.eu

Germany and abroad

Wertvoll leben
Im Kiesel 3, D-73635 Rudersberg
www.wertvollleben.com
Email: info@wertvollleben.com
Phone: +49 (0)7183 - 3071332
Phone: +49 (0)7183 - 3099847

Austria

TOP Life Wegweiser-Verlag
Prager Str.287, A-1210 Wien/Vienna
www.toplife-center.com
Email: info@wegweiser-verlag.at
Phone +43 (0)13199301-0

Austria and Germany

Adventist Book Center
Bogenhofen, A-4963 St.Peter/Hart
www.adventistbookcenter.at
Email: info@adventistbookcenter.at
Phone +43 (0)2294000

Switzerland

Advent-Verlag
Leissigenstr. 17, CH-3704 Krattigen
www.av-buchshop.ch
Email: info@adventverlag.ch
Phone +41 33 654 1065

S P E A K E R F O R S E M I N A R S

USA and many countries: www.spiritbaptism.org – start page scroll down

Germany, Austria, Switzerland, European countries:

www.steps-to-personal-revival.info - click German version – Kontakt page – scroll down

Phillipines: Allan D. Faina, Email: allan@lightingtheworld.org, SDA church:

Fidela Herrera Subd, Bgy. Santol, Tanza, Cavite-4108, Phones: (63) 926 054 1175

Hatua
ZA
Uamsho Binafsi

*Kujazwa
Roho Mtakatifu*

HELMUT HAUBEIL

7

UTANGULIZI
HATUA ZA UAMSHO BINAFSI

Kujazwa Roho Mtakatifu

9

UTANGULIZI KWA VIONGOZI WA
SASA NA WA SIKU ZIJAZO
KUZIDISHA MAVUNO

15

SURA YA 1

ZAWADI YA THAMANI ZAIDI YA YESU
Yesu alifundisha nini kuhusu Roho Mtakatifu?

Je unaufahamu ujumbe mkuu zaidi wa Yesu?

24

SURA YA 2

NI NINI KIINI CHA MATATIZO YETU?

Je kuna chanzo chochote cha kiroho kwa matatizo yetu? Je chanzo ni ukosefu wa Roho Mtakatifu?

47

SURA YA 3

JE MATATIZO YETU YANATATULIKA-JINSI GANI?

*Tunavezaje kukua na kuwa Wakristo wenyewe furaha na imara?
Je Roho Mtakatifu anawezaje kuyajaza maisha yetu?*

62

SURA YA 4

TOFAUTI GANI TUNAYOWEZA KUTARAJIA?

*Tuna faida gani tukiwa na maisha yaliyojazwa na Roho Mtakatifu?
Tunakosa kitu gani tusipoomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu?*

82

SURA YA 5

UFUNGUO KWA UZOEFU WA UTENDAJI

*Ninawezaje kutekeleza na kupata uzoefu wa jibu la Mungu kwangu?
Ninapaswa kuomba kwa namna gani ili niwe na uhakika wa kujazwa na Roho
Mtakatifu?*

96

SURA YA 6

KUNA UZOEFU GANI ULIO MBELE YETU?

Uzoefu binafsi, na vile vile uzoefu kutoka makanisani, Konferensi na Unioni

106

SURA YA 7

SHAUKU NA KUSHIRIKISHA WENGINE

*Furaha tuitoayo hurudi miyoni mwetu wenyewe. (Mithali ya Kijerumani)
Ninawezaje kuwasaidia watu wengine kupata "Uzima Tele". (Yohana 10, 10)*

116

HITIMISHO

117

KIAMBATISHO

Inapendekezwa usome zaidi

MWONGOZO WA SIKU 40

Uzoefu Mpya wa Kuishi na Roho Mtakatifu

BWANA WETU MWENYEWE AMETOA
AMRI¹

MJAZWE UPYA ROHO
MTAKATIFU KILA WAKATI
NA MARA KWA MARA!²

¹ E. G. White, Mount of Blessing, MB 20.3 (egwwritings.org)

² Johannes Mager, Auf den Spuren des Heiligen Geistes (Lüneburg, 1999), Seite 101

HATUA ZA UAMSHO BINAFSI

Kujazwa Roho Mtakatifu

*Kwa nini nilijkunta għafla tu
najishughulisha sana na suala la
“Maisha katrika Roho Mtakatifu”?*

Agosti 14, 2011, nilipokuwa Kandergrund katika Nyanda za Juu za Bernese huko Uswisi uhusiano muhimu ulidhihirika kwangu. Nilitambua sababu ya kiroho kwa nini tunapoteza baadhi ya vijana wetu. Nilishituka sana. Niliwfikiria watoto wangu na wajukuu zangu. Tangu hapo nimekuwa nikilifikiria sana jambo hili.

Sasa ninaamini kwamba sababu hiyo ya kiroho ndiyo inayohusika katika idadi kubwa ya matatizo yetu; hasa matatizo binafsi, kwenye makanisa mahalia na katika kanisa zima la kiulimwengu. Ni ukosefu wa Roho Mtakatifu.

Ikiwa hii ndiyo sababu, basi tunapaswa kulishughulikia jambo hili haraka. Kama chanzo cha tatizo kinawenza kuondolewa au kupunguzwa kwa kiasi fulani, basi matatizo mengi yatakuwa ya juu juu au yatatatuliwa.

Wengine wanasemaje kuhusu upungufu huu:

- ▶ **EMIL BRUNNER**, *Mwanatheoloja wa Kikristo aliyefanya matengenezo, aliandika kwamba Roho Mtakatifu “daima amekuwa zaidi au pungufu ya mtoto wa kambo wa theologia.”¹*
- ▶ **D. MARTIN LLOYD-JONES**: “Kamaninaweza kusema ule ukweli, basi hakuna mada juu ya imani ya kibiblia ambayo imepuuzwa sana huko nyuma au wakati huu kama mada ya Roho Mtakatifu.... Nina uhakika kwamba hii ndiyo sababu ya kudhoofika kwa imani ya kikristo.”²
- ▶ **LEROY E. FROOM**: “Nina uhakika kwamba ukosefu wa Roho Mtakatifu ndiyo tatizo letu bayu zaidi.”³
- ▶ **DWIGHT NELSON**: “Kanisa letu limetumia kila kitu kuandaa taratibu, mipango na programu za kuvutia, lakini kama hatimaye hatutakiri kafilisika kwetu kiroho [ukosefu wa Roho Mtakatifu], ambako kumetukumba sisi wachungaji na viongozi, basi hatutawenza kamwe kutoka ndani ya Ukristo wetu uliozoleka wa kawaida.”⁴

Kwanza tunataka kuvuviwa na Neno la Mungu jinsi ambavyo mavuno mengi yanawezekana kwetu.

Baada ya hapo, tuangalie ombi la Bwana Yesu Kristo juu ya Roho Mtakatifu.

1 Johannes Mager, *Auf den Spuren des Heiligen Geistes*, (Lüneburg, 1999), Cover

2 D. Martin Lloyd-Jones, *Vollmacht, Telos-Taschenbuch* Nr. 385, Marburg 1984, p. 72

3 E. G. White, *The Coming of the Comforter* (Hagerstown, 1949), p. 94

4 Editor Helmut Haubeil, *Missionsbrief Nr. 34* (Bad Aibling, 2011), Seite 3

UTANGULIZI KWA VIONGOZI WA SASA
NA WA SIKU ZIJAZO

KUZIDISHA MAVUNO

Mpendwa Kiongozi,

Je unataka eneo lako kukua kiroho na kuongezeka idadi ya waumini? Lakini:
hili linawezekana kweli leo? Ndiyo, hakika linawezekana. Kwa namna gani?

*“Kile unachokusudia, hutakifanisha kwa nguvu
ya jeshi wala kwa uwezo wa kibinadamu:
Hapana, roho yangu itafanikisha!*

*Ninaahidi, BWANA Mungu Mwenyezi.”
(Zek.4:6)*

Jambo hili linapaswa kufanyika namna gani? Ninafikiri sote bado tunapaswa kujifunza hapa. Je tunataka pia kujifunza kutokana na uzoefu wa watu wengine? Ninaamini hivyo. Hebu Bwana atuongoze kupitia Roho wake.

Uzoefu wa pamoja kupitia kitabu cha “Hatua za Uamsho Binafsi” [Hatua Za Uamsho Binafsi] unaonyesha kwamba kitabu hiki kinaweza kuwa na msaada wa thamani. Lakini ukuaji wa kiroho na kuongezeka idadi kunahitaji juhudzi zaidi ya kusoma hiki kitabu mara moja au kukisambaza. Moyo wako unapaswa kuhusika. Nathubutu kusema: eneo lako litafanya kama vile utakavyofanya. Hakuna anayeweza kumwongoza mwagine, isipokuwa yeche mwenyewe ameipitia njia hiyo. Maisha yetu, maombi yetu, shuhuda zetu, mazungumzo yetu, mvuto wetu, na mahubiri yetu vitatumiwa na Mungu. Kwa kweli, usomaji wa mara kwa mara unaonekana kuwa muhimu: Utafiti wa elimu umeonyesha kwamba ni muhimu kusoma mada muhimu kama hiyo katika maisha yetu mara sita mpaka mara kumi kabla hatujai lewa vyema. Jaribu hata mara moja. Matokeo yatakushawishi.

Shuhuda mbili kutoka kwa mchungaji na Kiongozi wa Idara katika Unioni, sasa amestaafu, huko Marekani:

1. Ushuhuda— ... Nimesoma kitabu chako cha “Hatua za Uamsho Binafsi” mara tatu. Kamwe sikufikiria kama ningepata maarifa mapya kama hayo kuhusu maombi. Maombi ambayo yamejengwa juu ya ahadi za Mungu kama ulivyoelezea. Tangu hapo, **Mungu amepata ushindi maishani mwangu ambao sikufikiria kama inawezekana.** – Nimealikwa kuhubiri katika mukutano wa makambi. Kitabu chako kimenipatia mada. June 26, 2017 – F. S. Imefupishwa T

2. Ushuhuda— ... Tangu nilipoanza kusoma kitabu chako (Nimekisoma mara 6 kulingana na ushauri uliopo ndani ya kitabu) na kujifunza jinsi ya kuomba kwa ahadi, maisha yangu yamebadilika.... Bwana aliniongoza kuandaa hubiri kwa ajili ya mukutano wa makambi juu ya mahitaji yetu makuu, baraka ziburudishazo za Roho wa Mungu. **Katika miaka yote niliyojitoa katika huduma, kamwe sijawahi kuhisi nguvu ya Roho Mtakatifu ikiwa ndani ya watu kama iliyokuwamo ndani ya wale watu 3,000.**— Mke wangu aliona badiliko kamilifu ndani yangu. Hata mimi mwenyewe ninashangaa. Julai 25, 2017 – F. S. imefupishwa

Wazo la siku 40- kutoka washiriki 17 mpaka washiriki 65

Kanisa dogo lililoko Cologne-Kalk, Ujerumani, lilikuwa na washiriki 17 wa jamii ya Kijerumani, Kihispania na Wareno. Mchungaji J. Lotze aliwaalika kutekeleza wazo la siku 40. Walisoma Kitabu cha Siku 40 katika makundi ya watu wawili wawili, kila mmoja aliomba kila siku kwa watu waliokuwa hawajafikiwa na wakaanzisha mahusiano binafsi pamoja nao. Katika siku ya 40 walikuwa na sabato ya wageni na baada ya hapo kukawepo na mahubiri ya hadhara ya siku 14. Waliweza kubatiza watu 13 ndani ya muda mfupi. Walirudia wazo la siku 40 mara kadhaa na wamekuwa na washiriki 65 ndani ya miaka 4. (Angalia vitabu vya Siku 40 kwa ajili Siku 40 Concept na nenda kwenye “Experiences No. 19” ili kupata maelezo Zaidi kutoka mji wa Cologne.)

Lugano, Eneo la Uswisi wanakozungumza Kiitaliano– lina misingi ya kidunia sana

Mchungaji Mathias Maag alikuwa na uzoefu mzuri kama mmishenari huko Afrika ya Kusini pamoja na vitabu vya 40 Days vilivyoandikwa na Dennis Smith. Aliporejea Uswisi, alianza mara moja kufanya kazi wazo hili. Kulikuwepo na ubatizo wa watu 15 katika mwaka wa kwanza [jambo ambalo si la kawaida katika eneo hili]. Mwanamke mmoja alikuwa mgeni wa kila siku katika kanisa hilo kwa miaka 15. Wakati wa programu ya 40 Days aliamua kubatizwa.

Kijana – Jina langu ni Alina van Rensburg. Ni Mkurugenzi wa Vijana Wakubwa katika Konferensi ya Kusini mwa Queensland [yenye washiriki 12,200 huko Australia]. Dada mmoja alinipatia kitabu cha ‘Hatua za Uamsho Binafsi’ mwanzoni mwa mwaka huu na nilishangaa kabisa. Kinalezea hasa somo ambalo Mungu aliweka moyoni mwa mume wangu na moyoni mwangu: kumfufua Roho Mtakatifu maishani mwetu!!- Ningeweza kukusimulia visa vingi sana, lakini kimsingi, tumebarikiwa sana na kitabu hiki kidogo! Greg Pratt [Mkurugenzi wa Discipleship and Spiritual Development SQC] alikuwa na nakala 300 zaidi ambazo nilizigawa kwa viongozi wangu vijana katika vikao vyetu nya uongozi mwanzoni mwa mwaka huu na matokeo yamekuwa ya kushangaza. – Hivyo kwa sasa ningependa kutafuta vingine 150 kuwapatia vijana wakubwa katika Kambi Kubwa mwaka huu, ili kujifunza wakati wa Vipindi nya “Life Group Sessions”.

Ubatizo wa watu 366 + watu 35 katika darasa la ubatizo

Katibu wa Unioni ya Burundi, Paul Irakoze, [washiriki 130,000, nakala 100,000 “Hatua za Uamsho Binafsi” kwa lugha ya Kirundi], alisema kwamba washiriki wote **320 wa zamani walirejea kupitia ushawishi wa kitabu hicho**. Walikubaliwa kwa ubatizo mpya mwezi Machi 2017.

Viziwi walikisoma kitabu mara tatu – Kisha walisimulia uzoefu wao kwa watu wengine wenye changamoto ya kusikia (viziwi): Matokeo: Mwezi Machi 2017, tulibatiza viziwi 25.

Wafungwa – Tilitawanya kitabu kwa washiriki wetu wa kanisa kwenye Gereza la Mpimba. Waliguswa na Roho Mtakatifu na wakaanza kuwaambia wengine juu ya imani yao. Sabato ya mwisho, wafungwa 21 walibatizwa na wengine 35 wanajiandaa kwa ubatizo. Haya ni matunda ya kitabu cha Hatua za Uamsho Binafsi. Imefupishwa.

Muda wa Kujifunza/Wiki ya Maombi

Unioni ya Burundi ilikuwa na wiki ya maombi kwa ajili ya washiriki wao 130,000 mwezi Novemba 2017 wakitumia “Hatua za Uamsho Binafsi” kwa mara nyingine tena. Masomo ya Katibu wetu juu ya mada hii pia yalirushwa kwenye redio ya Waadventista kila siku jioni.

Wanafunzi – Mchungaji Dwight Nelson, Mchungaji Kiongozi wa Chuo Kikuu cha Andrews, alisema kwamba, maisha yake yalibadilishwa kupitia kitabu hiki. Mnamo Septemba 2, 2017, alianza mfululizo wa semina uliokwa na kichwa

kisemacho: "Ground Zero and the New Reformation: How to be baptized with the Holy Spirit?" Anaonyesha na kunukuu kutoka kwenye kitabu na kukipendekeza kwa wengine. Hilo lilipelekea kupakuliwa (downloads) mara 4000 katika semina tatu. Angalia katika mahubiri haya: <https://www.pmchurch.tv/sermons>

Wazo—kutoka Marekani—Nilisikiliza mfululizo wa masomo kutoka kwa Dwight Nelson jana. Nitakapokuwa nikikielezea kitabu cha "Hatua za Uamsho Binafsi" kanisani kwangu Sabato hii, nitaelezea kwa muda wa dakika tano za kwanza kwa matumaini kwamba ushuhuda wake kuhusiana na kitabu utaamsha shauku za baadhi ya watu. Baada ya kuona kuwa kimekubalika, kwa ruhusa ya Wachungaji wangu, tutaonyesha masomo yaliyobakia kwa wale watakaokuwa tayari! D.W.

Uinjilisti – Dwight Nelson anaandika katika blogu yake Oktoba, 11. 2017 (Imefupishwa na kuhaririwa)

"Wageni" tisini na moja (ndivyo wanavyowaita) walijiunga na Kanisa la Waadventista Wasabato Zagreb katika program ya jioni ya dakika tisini ...Binafsi na kwa shukrani ya pekee kwa maombezi yako, ninahitaji kutoa ushuhuda **sijawahi kuona mahubiri ya hadhara ya kiinjilissti kama haya ya Zagreb katika miaka yote niliyojihusisha na uinjilisti**. Kama nilivyomwambia mchungaji hapa Pioneer, nina uhakika kabisa yalikuwa na yatabakia kuwa matunda ya kuingilia kati kwa Roho Mtakatifu mchana na usiku katika mji ule kulingana na maombi yale ya pamoja. Nakukumbusha, wengi wetu mnamo mwezi Septemba tulianza kumtafuta Mungu kwa ajili ya ubatizo wa kila siku wa Roho Mtakatifu (Kama Kristo anavyotualika kufanya katika Luka 11:13). Ndiyo maana nina ujasiri kuhusianisha kile nilichokiona na kushuhudia huko Zagreb na kazi yake moja kwa moja. Yote ambayo hayasemi lolote kuhusu mimi— bali husema kila kitu kuhusu uhakika wa ahadi ya Yesu— "**Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu ...**" (Matendo 1:8). Hivyo chochote tunachofanya, hebu tusiache kutafuta ubatizo mpya uletao nguvu wa Roho wa Mungu, kila siku asubuhi.

Upatanisho: Iko mifano mizuri ya watu na familia (angalia uzoefu na. 2/17; 3/31; 3/35; 3/40; 4/52; 4/56). Mifano ya makanisa yote kuanzia migogoro, mapigano, migawanyiko, majeraha, kukosekana kwa msamaha, hasira na mashambulizi binafsi mpaka kwenye msamaha wenye mani na upatanisho (uzoefu no. 1/10; 7/84).

Mama Kijana – Watoto – Hakika, ninajisikia kuwa na wajibu mkubwa kukuza watoto wadogo watatu wa kiume. Nimekuwa na ninaweza kuona tumaini pekee nililo nalo ni kuomba Roho Mtakatifu kila siku kuwa ndani yangu kila

siku. Tangu nimesoma kitabu chako, nimeona tofauti iliyofanya katika tabia ya watoto wangu. Nina uvumilivu wakati ambapo kwa kawaida nisingekuwa nao, nina upendo na huruma mahali ambapo kawaida ningekuwa na hasira. Na wao mara nydingi hujibu si kama hapo mwanzo kwa moyo wa unyenyekevu. Hakika tunaendelea kukua, lakini ninashukuru sana kuelewa ukweli rahisi wa jinsi Yesu anaweza kuishi ndani yangu! D.W.

'Unawezaje kuamsha shauku?' Katika mada hii unapata mapendekezo yenye thamani. Jambo moja, ambalo ni rahisi sana kuanza nalo, ni pendekezo la "Usomaji wa Mpangilio." Motisha mkubwa zaidi ni kupitia kuendesha "semina". Unaweza kuiendesha wewe mwenyewe, au uwe na mzungumzaji mwalikwa (au utumie video; inapatikana katika lugha kadhaa.) Unaweza kuongeza uzoefu zaidi ikiwa utakuwa na usomaji wa utaratibu kabla na baada ya semina.

Ombi langu: Naomba – kama kaka mkubwa- nipayendekeze kwako: omba na soma kitabu mara kadhaa pamoja na mtu fulani wa karibu. Hili kwa namna fulani litakuza maendeleo katika kundi lako, kanisa au konferensi.

Hatua inayofuata inaweza kuwa kushiriki na Wachungaji, Wazee na washiriki muhimu kuhusu ujuzi na uzoefu wako. Ni muhimu sana ili kuwafikia na kuigusa miyo yao. Hivyo ndivyo Ethiopia ilivyoanza. Mnamo Julai 2017, wachungaji 500 walipokea kitabu kwa lugha ya Kiamhariki mwishoni mwa juma la uamsho. – Huko Unioni ya kaskazini mwa Ufilipino kitabu kilitolewa katika m Kutano maombi ya Ufilipino kwa wazee wa kanisa 1,500 Juni 2017.

Ushuhuda

Je, wewe binafsi utawaambia wengine ushuhuda wako na kwenye vipeperushi vyetu? Kuna uvuvio mkubwa ndani yake. Kama ni muhimu, shuhuda zinaweza pia kutumika kutoka kwenye tovuti ya www.steps-to-personal-revival.info – Testimonies

Mpendwa Kiongozi!

Hebu tukue ndani ya Roho Mtakatifu. Bwana mwenyewe ametoa amri [MB20.3]:

“Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ujisadi; bali mjazwe Roho.”
(Waefeso 5:18)

Kristo ndani yetu na Roho Mtakatifu hutufanya kuwa “wajumbe wa habari njema” (Isaya 40:9).

Usisahau maneno ya mwisho ya Yesu alipokuwa duniani:

“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu kwa uweza wake [uwezo, kuwezesha, nguvu isiyo ya kawaida].” (Matendo 1:8)

Ndugu Yenu katika Yesu Kristo

Helmut Haubel

ZAWADI YA THAMANI ZAIIDI YA YESU YESU ALIFUNDISHA NINI KUHUSU ROHO MTAKATIFU?

*Je unanafahamu ujumbe
mkunzaidi wa Yesu*

Shuhuda binafsi chache za kwanza:

Turudi kwenye “Upendo wetu wa kwanza”: Dada mmoja aliniandikia: Mimi na rafiki yangu kwa sasa tunasoma kitabu cha “40 Days” kwa mara ya tatu tukikibadilisha na kitabu cha “Hatua za Uamsho Binafsi.” Kabla hatujagundua kitabu hiki usoefu wetu wa kiimani na maisha ya maombi haukuwa kama ulivyokuwa hapo mwanzo. **Tulitamani kuupata “upendo wetu wa kwanza” tena.** Tumeupata! Tunamshukuru Mungu kwa mioyo yetu yote. Inashangaza sana namna ambavyo Mungu wetu mwenye upendo anajibu maombi na kwamba hufunua jinsi ambavyo Roho Mtakatifu hutenda kazi – kwetu na kwa watu tunaowaombea. M. S

Yesu aliingia maishani mwetu: Mtu mwengine aliandika kuhusu vitabu hivi: “...vimekuwa mbaraka mkubwa uliokuwa ukisubiriwa kwa muda mrefu maishani mwangu. Kama washiriki wa kanisa wengine wengi na kama dada

kutoka kanisa letu alivyopata uzoefu, kitu fulani kilikuwa kimekosekana katika uzoefu wa imani na sasa tumekuwa na fursa ya kujua jinsi **Yesu alivyoingia maishani na** ameanza kutubadilisha. Bado anafanya kazi juu yetu na hatua kwa hatua anatusogeza karibu Naye.” S. K

Je wanafunzi wa Yesu waliwahi kujiuliza: Inawezekanaje Yesu anatenda kwa uweza mkuu namna hii? Hili lilikuwa na uhusiano na maisha yake ya maombi? Ndiyo maana walimwuliza: “Bwana, tufundishe sisi kusali.” Yesu alijibu ombi lao.

Fundisho lake kuhusu maombi katika Luka 11:1-13 lina sehemu tatu: Sala ya Bwana, mfano wa rafiki aliyefika usiku nyumbani na kama kilele ombi la kudumu kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

Katika mfano (fungu 5-8) wageni wanafika nyumbani kwa mtu usiku na hana kitu chochote, ambacho angeweza kuwapatia. Kwa sababu ya hitaji lake, mara moja alikwenda kwa jirani yake. Anamweleza kuwa “hana kitu” na anaomba mkate. Anaendelea kuomba mpaka anapewa mkate. Sasa ana mkate – mkate wa uzima – kwa ajili yake na wageni wake. Ana kitu fulani kwa ajili yake mwenyewe na sasa yupo kwenye nafasi nzuri ya kumpatia mgeni wake.

Sasa Yesu anahusisha mfano huu (tatizo: sina kitu) na ombi la Roho Mtakatifu kwa kusema: “Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa.” (Luka 11:9) Kisha inaendelea:

Ombi maalum la Yesu: Hivyo basi ombeni Roho Mtakatifu

Kuna fungu mahususi la Biblia ambalo Yesu anatuamuru kwa msisitizo kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Sifahamu fungu jingine lolote ambalo Yesu kwa upendo anatusihi kuweka jambo fulani moyoni. Mafungu haya yanapatikana katika somo lake la maombi katika Luka 11. Pale anasisitiza mara 10 kwamba tunapaswa kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Luka 11:9-13 NKJV:

“Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Au akimwomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao!”

Katika mafungu haya machache Yesu alitumia kitenzi “omba” mara sita; kisha akabadilisha “omba” na kusisitiza kwa neno “tafuta” mara mbili – kitendo- na mara mbili zaidi kwa “bisha” – pia neno linaloashiria kitendo.

Je hatuonyeshi wazi kwamba tunapaswa kutenda ili kwamba tuweze kujazwa na Roho Mtakatifu? Neno la mwisho “omba” linatumika katika wakati unaoendelea kwa Kiyunani. Hilo linamaanisha kwamba hatupaswi kuomba mara moja tu, bali tunapaswa kuomba daima. Hapa Yesu haonyeshi kuwa kuomba ni suala la linalopaswa kufanya haraka lakini pia anatutarajia tuendelee kulifanya. Kwa hakika pia anataka kuamsha nia zetu kwa ajili ya Roho Mtakatifu kuititia mwaliko huu kutoka moyoni. Huu mwaliko wa haraka unatuonyesha nia ya Yesu kwamba tutakuwa tunapungukiwa kitu fulani cha muhimu, endapo hatutaendelea kuomba kujazwa Roho Mtakatifu. Hakika alikuwa anavuta usikivu wetu kwenye ukweli kwamba hakika tunamhitaji Roho Mtakatifu. Kwa njia hii hutaka tuendelee kupokea mibaraka tele ya Roho Mtakatifu.

Katika kitabu cha Christ’s Object Lessons kinasema: “Mungu hasemi, Ombo mara moja, na utapata. Anatuagiza kuomba. Tudumu katika maombi bila kuchoka. Kudumu katika maombi humleta muombaji katika mtazamo wa dhati kabisa, na humpatia shauku zaidi ya kupokea vitu anavyoviomba”.¹

Kisha Yesu alitoa mifano mitatu, ambayo huonyesha tabia isiyoweza kuonyeshwa hata na baba wadhambi wa kibinadamu. Alitaka katuonyesha kwamba ni jambo lisilowezekana kwamba Baba yetu wa mbinguni asitupatie Roho Mtakatifu pindi tunapomwomba. Yesu anataka tuwe na uhakika kwamba tutapokea Roho Mtakatifu tunapoomba katika njia sahihi. Kwa ahadi hii na ahadi nyingine tunaweza kuomba kwa imani na kufahamu kwamba tayari tumepokea kile tulichokiomba. (1 Yohana 5:14-15; maelezo zaidi yanapatika katika sura ya 5)

Mwaliko huu maalum hutuonyesha kwamba kulingana na Yesu kitu fulani cha muhimu kinakosekana, wakati ambapo hatudumu kuomba Roho Mtakatifu. Anatuleta kwenye usikivu wetu kwamba kwa hakika tunamhitaji Roho Mtakatifu. Anataka tuendelee kupokea baraka tele kutoka kwa Roho Mtakatifu.

Sehemu hii ya somo lake juu ya sala ni mchakato wa kipekee. Roho Mtakatifu ni zawadi kubwa kuliko zote kutoka kwa Mungu—zawadi ambayo huja ikiambatana na zawadi nyingine zote. Hii ilikuwa ni zawadi ya thamani ya Yesu kwa wanafunzi na ushahidi wa wazi wa upendo wake. Nafikiri tunaweza

¹ E. G. White, *Christ’s Object Lessons* (1900), uk. 145.3

kuelewa kwamba zawadi ya thamani kama hiyo si ya mtu kulazimishwa. Hutolewa tu kwa wale ambao huonyesha shauku ya kupata zawadi hii na kuithamini.

Atatolewa kwa wale ambao wametoa maisha yao kwa Yesu; atatolewa kwa wale wanaoishi kwa kujitoa daima. (Yohana 15:4-5) Kujitoa huonyeshwa kwa:

- ▶ Hamu ya Mungu (“*Mtu akiona kiu*”. Yohana 7:37)
- ▶ Mwamini Mungu (“*Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena*” Yohana 7:38)
- ▶ Jitoe kikamilifu kama matokeo ya kumwamini Mungu. “*itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai*” Warumi 12:1)
- ▶ Kumfuata Mungu katika kila jambo (“*wote wamtio*” Matendo 5:32)
- ▶ Kuachilia njia zao wenyewe, kufuata njia ya Mungu na kufanya hili kulingana na mapenzi ya Mungu (“*tubuni mkabatizwe*” Matendo 2:38)
- ▶ Si kupanga jambo lolote baya (“*Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia*”. Zaburi 66:18)
- ▶ Kutambua na kukiri hitaji letu kubwa Luka (“*Sina kitu*” Luka 11:6)
- ▶ Kuendelea kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu (Luka 11:9-13)

Je huwezi kuona wazi wazi katika matarajio haya aliyo nayo Mungu kwa ajili yetu, kwamba hii zawadi ina thamani kiasi gani? Unapofikiria kuhusu hivi vigezo vyote, basi huenda utakuta mapungufu mengi ndani yako.

Nimefanya kuwa tabia yangu kuomba kila siku kwa ajili ya tamanio kwa ajili ya Roho Mtakatifu kulingana na Yohana 7:37NKJV: “*Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe*”.²

Tunaweza kuomba: “Bwana Yesu, hakika ninasema ndio kwa vigezo vyote vya kupokea Roho Mtakatifu. Ninakuomba kwa dhati jambo hilo sasa—kwa leo—uvikamilishe ndani yangu.” Mungu wetu wa ajabu yuko pale kwa ajili yetu kuyajaza mahitaji hayo.

Roho Mtakatifu ni Chanzo cha Maisha Makamilifu

Kulingana na Yesu kwa nini alikuja humu duniani? Alisema:

“*Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.*” (Yohana 10:10 NKJV)

Yesu anatutaka tupate maisha haya mapya sasa na tuendelee kwayo

² Ni muhimu kuomba kwa ahadi. Ikiwa unatka kufahamu Zaidi kuhusu hili, tafadhalii soma sura ya 4.

katika mtazamo tofauti kabisa baada ya kuja kwake mara ya pili kama maisha ya umilele katika ufalme wa Mungu.

Pia hutuonyesha kwamba chanzocha maisha makamilifu ni Roho Mtakatifu: "...*Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.*" Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho ..." (Yohana 7:37-39)

"Mito ya maji yaliyo hai" – Je huo si ulinganifu mzuri kwa maisha makamilifu?

Je Yesu wakati alipokuwa hapa duniani alitupatia mfano?

Tunafahamu kwamba Mariamu alipata mimba ya Yesu kupitia Roho Mtakatifu. (Mathayo 1:18). Tunafahamu kwamba baada ya ubatizo wake aliomba: "Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwilwili, kama hua..." (Luka 3:22) Katika mazingira kama haya ilikuwa ni muhimu kwamba apokee Roho Mtakatifu kila siku? Na nukuu kutoka kwa E. G. White:

*"Kila siku asubuhi aliwasiliana na Baba yake wa mbinguni, akipokea kutoka kwake ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu."*³

Kuna maelezo katika kitabu cha Acts of the Apostles: "Kwa mtendakazi mwaminifu kuna faraja ya pekee katika kutambua kwamba hata Kristo wakati wa maisha yake hapa duniani alimtafuta Baba yale kila siku kwa nguvu mpya ya neema iliyohitajika...."⁴

Hakika Yesu alikuwa mfano kwetu katika hili. Tunapaswa kujuliza sisi wenyewe: Ikiwa Yesu alihitaji kupata nguvu mpya kila siku kutoka kwa Roho Mtakatifu, je ni muhimu zaidi kiasi gani kwako na kwangu?

Mtume Paulo alielewa hakika lengo la Yesu. Katika barua yake kwa kanisa la Efeso, Paulo anathibitisha katika sura ya 1:13 kwamba wametiwa muhuri na Roho Mtakatifu walipomwamini. Katika sura ya 3:16-17 anawatia moyo kuwa na nguvu katika Roho na katika sura ya 5:14 (NKJV) Paulo, kama mtume mwenye mamlaka, anawasihi Waefeso na sisi: "...*tujazwe Roho*" au "*muendelee daima kujazwa Roho*"⁵ Tunaona kwamba hata kama tulipokea Roho Mtakatifu tulipozaliwa upya, tunahitaji nguvu mpya kila siku. Ni muhimu kwa maisha ya kiroho na ukuaji wa Mkristo kujazwa kila siku Roho Mtakatifu.

³ E. G. White, *Signs of the Times*, November 21, 1895, par. 3

⁴ E. G. White, *The Acts of the Apostles*, (1911) uk. 56.1

⁵ Johannes Mager, *Auf den Spuren des Heiligen Geistes*, (Lüneburg, 1999), Seite 101

Muongozo Wetu wa Kujifunza Biblia wa Shule ya Sabato unasema yafuatayo kuhusu Waefeso 5:18: “Inamaanisha nini ‘kubatizwa’ kwa Roho Mtakatifu? Yesu mwenyewe alilielezea hili kwa mfano. Mtu “anabatizwa” kwa Roho Mtakatifu (Matendo 1:5) wakati Roho Mtakatifu ‘alipowajilia’ juu yao (fungu la 8). Kubatizwa humaanisha kuzamishwa kabisa ndani ya kitu—mara nyingi maji. Hili huhusisha mwili mzima wa mtu. Ubatizo wa Roho Mtakatifu humaanisha kuwa katika ushawishi wa Roho Mtakatifu—‘kujazwa’ kabisa

na yeye. Huu si uzoefu wa mara moja, bali ni kitu fulani ambacho kinapaswa kuendelea kurudiwa, kama Paulo alivyoelezea katika Waefeso 5:18b kwa msisitizo wa kitenzi cha Kiyunani ‘kujazwa’.”⁶

Maneno ya Mwisho ya Yesu na Roho Mtakatifu

Katika maneno ya mwisho ya Yesu alionyesha furaha na tumaini kwa kuwaambia kwamba Roho Mtakatifu angekuja badala yake. Yesu anasema kitu fulani cha kushangaza kwa wanafunzi katika Yohana 16:7:

“Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu.”

Suluhihisho Jipyä Lenye Faida

Yesu aliwaambia wanafunzi jambo fulani la kushangaza. *“Yawafaa ninyi mimi niondoke.”* Hii humaanisha kwamba suluhihisho jipyä, kwamba yuko pamoja nasi kupitia Roho Mtakatifu, ni la manufaa sana kuliko Yesu kuwepo kimwili. Kwa njia hii hajafungwa sehemu moja, bali anaweza kuwepo kwa kila mtu, bila kujali mahali alipo kwa wakati huo.

Ushuhuda binafsi kutoka kwa mwalimu na mmojawapo wa wanafunzi wake:

Wakati kitabu cha “Hatua za Uamsho Binafsi” kutoka H. Haubeli kilipoletwa katika kanisa langu mahalia takribani mwaka mmoja uliopita, nilikisoma chote haraka sana. Tayari nilipokuwa nikikisoma nilikuwa na uzoefu zaidi pamoja na Mungu kuliko nilivywahi kuwa hapo awali—hili lilihangaza na kunitia moyo.

⁶ Sabbath School Study Guide July 17, 2014

Katika maelezo ya kitabu hicho nilikuta mapendekezo yafuatayo:
“Utafiti wa kiyakinifu umeonyesha kwamba ni muhimu kusoma au kusikiliza mara sita au mara kumi mada muhimu mpaka tuwe tumeielewa yote.”

Haya maneno ya kutia moyo yaligusa usikivu wangu:
“Jaribu kufanya hivi japo mara moja. Matokeo yatakushawishi.”

Nilitaka kujaribu jambo hilo na tayari katika kukisoma mara ya tatu kilinigusa na nilihihi upendo mkubwa kwa Mwokozi wetu, ambao nimeutamani maisha yangu yote. Ndani ya miezi miwili nilikuwa nimekisoma mara sita na matokeo yake yalikuwa yenye thamani.

Ilikuwa ni kama vile niliweza kuelewa vile ambavyo ingekuwa wakati Yesu anapokuja karibu nasi na tunaweza kutazama katika macho yake ya upole, huruma na yenye upendo. Tangu wakati ule sikutaka kuikosa hii furaha katika Mwokozi wetu.

Nikiamka asubuhi tayari nilikuwa natamani muda wangu wa ibada ya asubuhi ili kwamba niweze kuwa na ushirika pamoja na Mungu na wakati wa mchana niliomba kimya kimya kwamba Roho Mtakatifu anisaidie katika mawazo yangu katika mazungumzo yangu, mfano wangu, nikiwa nafundisha na kuwasiliana.

Wakati mtoto alipotamani usikivu na kutenda ipasavyo, Mungu alinipatia nguvu na busara ya namna ya kushulikia jambo hilo.

Tangu hapo siku zangu za kazi zimejazwa na uwepo wa Muumbaji. Hakika ananisaidia katika maisha yangu ya kila siku. Tangu hapo ninaomba asubuhi na nyakati za mchana kwa ajili kujazwa Roho Mtakatifu. Ni kama vile uko karibu na mbingu na tayari unaweza kuonja kuwa pale itakuwaje.

Wakati nikiwa nasoma kitabu wazo likanija kwamba wanafunzi wangu shuleni wanapaswa pia kushiriki usoefu huu. Ninafundisha watoto wa umri wa miaka 10-15 katika shule yetu ya Kiadventisha ya Elijah iliyoko Vorarlberg, Austria. Hivyo nilimwomba Mungu anipatie fursa. Mapema sana baadaye nilikuwa na mojawapo ya usoefu wangu wa kushangaza wa jinsi Roho Mtakatifu anavyoweza kufanya kazi ndani ya mioyo ya vijana wadogo.

Kijana mtukutu wa miaka 13 na Roho Mtakatifu

Uzoefu ulianza *mwaka mmoja kabla sijasoma kitabu juu ya Roho Mtakatifu*. Mwanafunzi mpya alikuja shuleni kwetu na ndani ya siku chache kisiwa chetu chenye amani kilibadilishwa na kuwa chumba cha ugomvi. Kijana wakati huo alikuwa na miaka 13—alikuwa mvulana mkubwa kuliko watoto wote na alikuwa na nguvu sana. Mambo mengi yaliyokuwa yamejifunzwa shuleni na yaliyokuwa yameleta matokeo mazuri yalionekana kupotea ndani ya muda mfupi.

Hebu asimulie yeje mwenyewe: "Nilipofika katika shule yangu ya sasa, sikufahamu kile kilichokuwa kikiningoja. Siku yangu ya pili shulenii niliruhusu mimi mwenyewe kuchokozwa, nikakasirika, na kupigana na mmojawapo wa mwanafunzi mwenzangu. Nilimpiga japokuwa alikuwa dhaifu kuliko mimi, nilimkemea na kumwambia kuwa sikutaka kumuona tena kamwe.

Baadaye niligundua kosa langu na kuomba msamaha, kama ambavyo nimekuwa nikifanya huko nyuma. Baada ya hapo nilikuwa na mazungumzo pamoja na mwalimu mkuu. Katika miezi iliyofuata mchakato ukaanza ndani yangu. Inashangaza kwamba mchakato huu ulikuwa unaanza sasa tangu nilipokuwa mtoto wa mchungaji. Nilianza kutumia muda wangu mwingi pamoja na Yesu."

Nikafikiri kwamba kijana huyu mdogo angehitaji uanganlizi maalum wa ziada. Alitambua mapungufu yake, alijuta na kujaribu tena, lakini hakuwa na mafanikio ya muda mrefu kwa nguvu zake mwenyewe. Mwanzoni, ilikuwa ni vigumu siku kuisha bila kupigana, lakini taratibu aliendelea vizuri.

Baada ya miezi sita alisema kuwa alifikiri maombi ndiyo yaliyomleta karibu na Mungu. Kwa wakati huo alikuwa ameanza kuomba kwa ajili ya nguvu asubuhi. Hasira zake na magomvi yakaanza kupungua.

Miezi kumi na moja sasa ilikuwa imepita tangu aje shulenii kwetu na tuliweza kuona mabadiiliko makubwa. Lakini hasira zake, maapizo na magomvi yake hayakuwa yamethibitiwa kabisa.

Lilikuwa ni jambo la kawaida – alijaribu kushinda kwa nguvu zake mwenyewe na kwa uelewa wake mwenyewe, jambo ambalo lilifanikiwa wakati fulani na nyakati zingine ilishindikana. *Maombi yetu yalikuwa yamefanikisha kiasi fulani, lakini akili yake haikuwa sawa na uwezo ubadilishao wa Roho Mtakatifu ulikosekana.*

Inasaidia nini, wakati watu wanapogundua makosa yao, kujaribu kuzuia hasira zao na muda unaofuata hushindwa tena? Kama wakati ambao niligundua kwamba nilikuwa katika wakati wangu mbaya kabisa, nilipokea kitabu kilichotajwa hapo juu. Kisha nikagundua kile tulichokua tunakikosa. Ilikuwa ni nguvu ya Roho Mtakatifu. Hatukuwa hata tumemuomba atusaidie!

Kwa kuwa nilikuwa nimeguswa na ujumbe wa "Hatua za Uamsho Binafsi" Nilipata ujasiri wa kumuuliza kijana kama amewahi kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Hapana – kamwe hajawahi. Kisha nikajaribu kuamsha shauku yake katika kitabu hicho. Hata hivyo sikumpatia. Anapaswa kukihitaji. Na mara akaomba kile kitabu.

Kwa mara nyingine tena kwa maneno yake mwenyewe: "Mwezi Novemba 2012 mwalimu wangu alinipatia kitabu" Hatua za Uamsho Binafsi" Nikaanza

kukisoma kwa shauku. Katika wakati ulesikuwa nikiifahamu vizuri kazi ya Roho Mtakatifu."

Katika siku ya kwanza alikuwa amemaliza kusoma mada mbili na kisha akaniuliza nilikuwa nimekisoma mara ngapi. Haraka alianza kusoma sura hizo tena na akataka kufanya kile ambacho kile kitabu kilikuwa kimeshauri: kukisoma mara 6-10.

Tangia hapo mambo mengi yamebadilika. Tangu Disemba 2012na kuendelea hakukuwepo na mapigano wala ugomvi – ilikuwa vigumu kwangu kuamini. Wavulana aliokuwa akiwapiga kila siku wakawa rafiki zake na wakawa wakielewana sana.

Amebadilika kabisa– ni mpole na hata kujitolea na amani imechukua nafasi ya hali yake ya asili ya hasira. Wanafunzi wenzake wanaweza kuthibitisha kwamba Mungu alikuwa kazini. Unaweza kuona matokeo kila siku. Kwa utukufu wa Mungu ninataka kusema kwamba kijana aliamua kubatizwa mwezi Juni 2013. Kama huyo hakuwa Roho Mtakatifu.

Wakati wote nimekuwa nikifikiri kwamba ningeweza kumuongoza mtoto na kumfanya aone sababu. Uvumilivu, kumpatia usikivu na mazungumzo mengi yangeweza kufanya jambo hilo, lakini hayakufanikiwa kwa muda mrefu. Mungu aliingilia kati na akanifundisha kwamba ni Roho wake Mtakatifu, ambaye hufanya mambo yasiyowezekana yawezekane.

Siku moja wakati kijana huyu akiwa mbinguni, basi nitajua kwamba Mungu alililetu. Wakati nilipokuwa nimepungukiwa busara zangu na mwishoni kuelewa kwamba nisingeweza kumuongoza, basi Mungu alianza kumfanyia kazi. Ilinitia moyo kuona kwamba hakuna jambo lisilowezekana kwa Mungu. C. P

Ombi: Baba wa mbinguni, asante kwa ajili ya mwaliko wa haraka wa Yesu wa kuomba Roho Mtakatifu. Nisamehe kwa hasara nilizopata kwa sababu ya kukosa Roho Mtakatifu. Ninahitaji msaada wa kimbingu ili kwamba Yesu aweze kuniongoza. Ninahitaji msaada wake katika kila sehemu ya maisha yangu. Asante kwamba Roho Mtakatifu anaweza kubadilisha tabia yangu na kunifanya nifae kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Ninajisalimisha kikamilifu mimi mwenyewe kwako pamoja na vyote nilivyo navyo na jinsi nilivyo. Asante kwa kunipokea na kunipatia baraka zako. Nisaidie kukua katika maarifa kuhusu Roho Mtakatifu. Amina.

NI NINI KIINI CHA MATATIZO YETU?

*Je kuma chanzo chochote cha
kiroho kwa matatizo yetu?*

Je chanzo ni ukosefu wa Roho Mtakatifu?

SABABU ZA UKOSEFU HUU

Jibu la Biblia ni hili: “*Wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi! Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya* (kwa kuufuata mwili Warumi 8:5-7), *ili mvitumie kwa tamaa zenu.*” (Yakobo 4:2-3 NKJV)

Bwana wetu Yesu alitualika kwa upendo na kusisitiza tuombe kwa ajili ya Roho Mtakatifu (Luka 11:9-13). Tunaelewa kwamba tunapaswa kuendelea kufanya hivi. Katika sura ya tatu tutaangalia jambo hili kwa undani.

*“Wanazungumza kuhusu Kristo na kuhusu Roho Mtakatifu, lakini hawapokei faida yoyote. Hawatoi nafsi iongozwe na kutawaliwa na mawakala wa kimbingu.”*⁷

Tumekuwa tukiomba kwa ajili ya uamsho kwa muda sasa. Hili ni jambo la thamani sana. E. G. White alisema: “Ni ubatizo huu wa Roho Mtakatifu ambao

⁷ Ellen G. White, *The Desire of Ages*, (1898), uk. 672

kanisa linauhitaji leo.”⁸ “Kwa nini tusiwe na njaa na kiu kwa ajili ya Roho, kwa kuwa hii ndio njia ambayo tunaweza kupokea nguvu? Kwa nini tusizungumze juu yake, tuombe juu yake, tuhubiri juu yake?”⁹

Ni vizuri kwamba tuombe kwa ajili ya uamsho, lakini hatupaswi kuomba tu, bali – kama Mark Finley alivyosema – ni “**kama tunavyofanyia vitendo mambo ya uamsho wa kibiblia.**”¹⁰ Ninaweza kukualika kuchukua hatua kwa ajili ya uamsho binafsi? Kwa watu wengi hili litaongoza kwenye maisha yenye nguvu zaidi na yaliyojitosheleza.

Kwa kuanza, tunataka kulichambua tatizo. Tunataka kulifanya hili kwa umakini; vinginevyo iko hatari kwamba hatutalichukulia badiliko kama lina umuhimu au la muhimu. Baada ya hapo tunataka kuangalia katika suluhisho la Mungu, ambalo hutupatia mibaraka mingi na mwisho, jinsi tuavyoweza kulitekeleza hili na kulitumia.

Ukosefu wetu wa Roho Mtakatifu haumaanishi kwamba kila kitu ambacho tumefanya na tunachofanya hakina maana. Ilikuwepo na ipo mipango mingi mizuri sana na vipindi vingi. Hakika Bwana amebariki juhudzi zetu za kibinadamu. Lakini matokeo yangekuwa makubwa kiasi gani na hali ingekuwa nzuri kiasi gani, kama tungeishi au kuishi kwa ukaribu na Roho Mtakatifu – Ni Mungu pekee anayelifahamu hilo.

Ingeelekea upande huu na ingeелеека upande huu kwa siku zijazo kama ambavyo Henry T. Blackaby aliliezea hili:

“Yeye (Mungu) angeweza kufanya mambo mengi kwa muda wa miezi sita na watu ambao wamejitoa kikamilifu kwake, kuliko ambavyo tungeweza kufanya kwa miaka sitini pasipo yeye.”¹¹

Ni suala la kwenda upesi katika njia sahihi chini ya uongozi wa Mungu na hivyo kuwa na ufanisi mkubwa zaidi (utendaji bora). Ndivyo inavyokuwa tunapojazwa na Roho Mtakatifu.

Mfano: Mtu fulani anahubiri. Amemaliza kuzungumza – huenda hakuna hata mtu mmoja, wachache, wengi au wote huupokea ujumbe. Kama wengi au wote wakiupokea ujumbe na kuufanya kazi, basi huu ni ufanisi mkubwa. Hili ni jambo mbalo Roho Mtakatifu hutoa.

⁸ E. G. White, *Manuscript Releases Vol. 7* uk. 267

⁹ E. G. White, *Testimonies for the Church Vol. 8* (www.egwwritings.org), uk. 22

¹⁰ Mark A. Finley, *Revive us again*, uk. 25

¹¹ Henry T. Blackaby, *Den Willen Gottes erkennen und tun (Experiencing God: Knowing and Doing the Will of God)*, (Kassel, 2002), uk. 31

MAKUNDI MATATU YA WATU NA MAHUSIANO YAO BINAFSI NA MUNGU

Neno la Mungu hutofautisha makundi matatu ya watu kuhusiana na mahusiano yao binafsi na Mungu. Kwa kila mojawapo ya makundi haya kuna tabia nyingi tofauti kulingana na mafunzo kutoka kwa wazazi, tabia, mafunzo binafsi, umri, tamaduni, elimu, n.k. lakini pamoja na tofauti hizo zote kuna **mitazamo mitatu mikuu tu kwa Mungu:**

- ▶ Hakuna mahusiano – Biblia huliita jambo hili mwanadamu wa tabia ya **asili**.
- ▶ Mahusiano makamilifu na ya uhakika – Biblia huita jambo hili mtu wa **kiroho**.
- ▶ Mahusiano yenye kugawanyika au ya kuigiza –Biblia huelezea haya kama mtu wa **tabia au mwilini matendo ya mwilini**.

Maneno “mtu wa asili”, “mtu wa rohoni” na “mtu wa tabia ya mwilini” katika Neno la Mungu si tathmini katika habari hii. Yanaelezea tu uhusiano binafsi wa mtu na Mungu.

Haya makundi matatu yameelezwa katika 1 Wakorintho 2:14-16 na1 Wakorintho 3:1-4. Kwa sasa tunataka kugusia kwa juu juu tu somo la mtu wa asili. Anaishi duniani. Kwa mtazamo wa haraka katika makundi mawili ndani ya kanisa utatusaidia kutambua tatizo limejificha wapi hasa. Jambo la muhimu zaidi kutambua ni kuwa wewe uko kundi gani. Hivyo uchunguzi wetu pia husaidia uchunguzi binafsi. Tunataka kuangalia maisha yetu wenyewe na si maisha ya watu wengine.

Ni vigezo vipi kwa ajili ya kuwepo kwenye kundi mojawapo au jingine? Tutaangalia kwamba katika makundi yote matatu kuwepo katika makundi hutokeea kulingana na mahusiano yao binafsi na Roho Mtakatifu.

Mwanadamu wa Tabia ya Asili

“Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.” (1 Wakorintho 2:14 NKJV)

Mwanadamu wa tabia ya asili hana uhusiano kabisa na Roho Mtakatifu. Anaishi ulimwenguni na haulizii habari za Mungu kabisa au mara chache sana huuliza habari za Mungu.

Watu wa Kiroho na wa Tabia ya Mwilini wamo ndani ya Kanisa

Makundi haya mawili yameelezewa katika 1 Wakorintho 2 na 3 na vile vile katika Warumi 8:1-17 na Wagalatia 4 na 6. Tunatakiwa kutambua kwamba **kigezo kwa makundi haya mawili ni mahusiano yao na Rofo Mtakatifu.** Hii iko hivyo, kwa sababu Mungu ameeleza wazi kwamba Roho Mtakatifu ndiye muunganishi wetu mkuu na mbingu. (The Desire of Ages, uk. 322; Mathayo. 12:32) “Moyo unapaswa kuwa tayari kupokea ushawishi wa Roho, vinginevyo mbaraka wa Mungu hauwezi kupokelewa.”¹²

Mshiriki wa Kanisa wa Kiroho

Tusome 1 Wakorintho 2:15-16:

“Lakini **mtu wa rohoni** huyatambua yote, wala ye ye hatambuliwi na mtu.

Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimitshe? (Isaya 40:13) Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.” (NKJV)

“Lakini **mtu wa rohoni** huyatambua yote, wala ye ye hatambuliwi na mtu. Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimitshe? “Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.” (NIV)

Mtu wa Kiroho ndiye Mkristo wa kweli. Anaitwa “wa Kiroho” kwa sababu amejazwa na Roho Mtakatifu. Hapa pia, mahusiano pamoja na Roho Mtakatifu ni kigezo cha kuitwa mtu wa kiroho. Ana mahusiano mazuri yanayokua pamoja na Roho Mtakatifu. Yesu ni “*kiini cha maisha yake.*”; tunasema pia wakati mwininge kwamba Yesu anatawala ndani ya miyo yetu. Mtu wa kiroho amejikabidhi mwenyewe kikamilifu kwa Yesu na kama kanuni ya msingi hili huthibitishwa kila siku kwa kujitoa ye ye mwenyewe kwa Yesu kila asubuhi kwa jinsi alivyo na kwa kila alichu nacho. Katika ujumbe wa Laodikia anaitwa “moto”, katika mfano wa wanawali 10 anaitwa “*mwenye busara*”. Warumi 8:1-17 na Wagalatia 5 husema mengi zaidi juu yake. Anapata uzima “*tele*” (Yohana 10:10) au kama Paulo alivyosema: “*Mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu*”. (Waefeso. 3:19; Wakolosai. 2:9)

Mshiriki wa Kanisa wa Tabia ya Mwilini

Mtu anaweza kuwa mshiriki wa kanisa kwa muda au kwa miaka mingi na bado akawa Mkristo wa mambo ya kimwili. Kama kwa mshangao wako unaweza

¹² Steps to Christ, 95.1 (egwwritings.org)

kujikuta kwamba wewe ni Mkristo wa kimwili wakati huu, basi furahi, bali furahi, kwa sababu una uwezekano wa kuibadilisha hali hiyo mara moja. Utakuwa na furaha kubwa kuishi maisha yaongozwayo na Roho Mtakatifu. Ninashawishika kwamba Wakristo wengi wa kimwili bila kujitambua wako katika hali hii na wanatamani kupatia zaidi uzoefu wa imani zao. Kutojitambua kwao mara nyingi si kosa lao. Fikiria: utapata furaha kubwa kuititia maisha pamoja na Kristo moyoni mwako kuititia Roho Mtakatifu. (Yesu katika Yohana 15:11: “*na furaha yenu itimizwe.*”) Kuititia badiliko hili utapata uzoefu wa uzima tele hatua kwa hatua (Yesu katika Yohana 10:10 – zaidi kuhusu mada hii baadaye) nawe utakuwa na tumaini thabitia la uzima wa milele.

Ombi: Baba wa mbinguni, naomba unifanye niwe tayari kuijuliza mwenyewe swalii hili. Ikiwa mimi ni Mkristo wa tabia ya mwilini, basi naomba unisaidie kutambua hili jambo mapema. Nifanye niwe tayari kujiandaa kwa ajili ya kila kitu unachotaka. Tafadhali niongoze kwenye maisha ya furaha ya Kikristo – kwenye maisha yaliyoahidiwa kwa wingi na kwa uzima wa milele. Tafadhali uumbe upya moyo wangu. Asante kwa kujibu maombi yangu. Amina.

Tusome kile ambacho mtume Paulo alisema kwa washiriki wa kanisa wa tabia ya mwilini katika 1 Wakorintho 3:1-4 (NKJV): “*Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu? Maana hapo mtu mmoja asemapo, Mimi ni wa Paulo; na mwingine, Mimi ni wa Apolo, je! Ninyi si wanadamu wa tabia ya mwilini?*”

Je unaweza kuona hapa kwamba kigezo cha kuwekwa katika kundi hili ni uhusiano binafsi na Roho Mtakatifu? Katika mafungu haya machache mtume Paulo anataja mara nne kwamba hawa ni watu wa tabia ya mwilini. Je kuwa wa mtu wa tabia ya mwilini humaanisha nini? Humaanisha: huyu mtu anaishi kwa nguvu ya kimwili, hiyo ni nguvu na uwezo wa kawaida wa kibinadamu.

Zaidi ya hayo, humaanisha kwamba hajajazwa na Roho Mtakatifu au hana Roho Mtakatifu wa kutosha.

Baadhi ya watu hufikiri kwamba kundi hili linajumuisha watu tu amba wanaishi dhambini wazi. Lakini hilo ni moja tu kati ya mambo mengi ya kundi hili. Ninataka kusisitiza kwa mara nyingine tena kwamba ziko tofauti nyingi katika makundi haya yote.

Paulo anaelezea watu wa tabia ya mwilini kama “*wapenzi*”. Hili huonyesha kwamba alikuwa anashughulika na **washiriki** wa kanisa. Paulo hakuweza kuzungumza nao “*kama na watu wa tabia ya rohoni*.” Hili humaanisha kwamba: **Hawakuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu**. Alipaswa kuongea nao kama “*kama watoto katika Kristo*.” Hili humaanisha kwamba hawakuwa wamekua katika imani kama walivyopaswa kuwa. Mtu anaweza kuwa na uelewa mkubwa wa kibiblia na bado asikue kiroho. Ukuji wa kiroho unapaswa kuendana na kujitoa kwetu kikamilifu kwa Yesu na maisha ya kila siku ndani ya Roho Mtakatifu.

Wakristo wengi wa tabia ya mwilini huhisi kutoridhika, kukata tamaa, kutokuwa na malengo au huhisi kuwa kila siku wako chini ya juhudzi za kila siku katika maisha yao ya kiroho.

Washiriki wengine wa kanisa wa tabia ya mwilini wamezoea kuwa katika hali hii au wameridhika na hali hii. Wanaweza kusema: “Sisi ni wadhambi tu! Hatuwezi kufanya jambo lolote kuhusu hili!”

Tena Wakristo wengine wa tabia ya mwilini wanaweza kuwa na shauku. Wanafurahi kwamba wanafahamu ukweli wa Kibiblia. Washiriki wa kanisa wa tabia ya mwilini wanaweza kuwa wenye kujituma sana na hata kuwa na nyadhifa za uongozi katika kanisa mahalia au hata katika uongozi wa kanisa. Wanaweza hata kufanya mambo mengi kwa ajili ya Mungu.

Mathayo 7:22-23 (NKJV): “Wengi wataniambia siku ile, ‘Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?’ Ndipo nitawaambia dhahiri, ‘Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu!’”

Tatizo lilikuwa wapi? Yesu alisema kwamba hakuwajua. Hawakuwa na uhusiano halisi na Kristo, bali ulikuwa ni uhusiano wa kuigiza tu. Huenda hakukuwepo na kujitoa kikamilifu au uhusiano huo hakuendelezwa. Yesu hakuishi ndani ya miyo yao kupitia Roho Mtakatifu. Hivyo hawakuwa na uhusiano binafsi na Kristo. “Hivyo inawezekanakukawepo na mahusiano ya juu

“Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenyе maana.”

juu na Kristo....”¹³ Ni wakati upi ambao Yesu hayumo ndani yetu? Ninasoma maneno yenyе nguvu kuhusu hili. Kabla sijayatamka, ninataka kutaja kwamba tunaweza kuwa huru kutoka kwenye haya mambo yafuatayo kama tukiishi maisha pamoja na Roho Mtakatifu:

“Roho aliye kinyume na Roho wa Kristo angemkana, bila kujali kazi yake. Wanadamu wanaweza kumkana Kristo kwa kuzungumza uovu, kwa kuzungumza upumbavu, kwa maneno ambayo si ya kweli au si ya wema. Wanaweza kumkana kwa kutokubeba masumbufu ya maisha, kwa kufuata starehe za dhambi. Wanaweza kumkana kwa kuufuta ulimwengu, kwa tabia isiyo na kiasi, kwa kupenda mawazo yao wenywewe, kwa kutetea ubinafsi, kwa kufuata mashaka, kuwa na matatizo, na kuishi gizani. **Katika njia zote hizi wanatangaza kwamba Kristo hayumo ndani yao.**”¹⁴

Hili kwa haraka linaweza kubadilika kwa neema ya Mungu. Tutarudi katika hili katika sura ya tatu na ya tano.

Kwa nini kusalimisha maisha yetu na kuweka ahadi kwa Mungu ni muhimu?

Neno la Mungu linasema: “Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenyе maana.” Warumi 12:1 NKJV

“Mungu anatamani kutuponya, kutuweka huru [kutoka kwenye dhuluma ya ubinafsi wetu na utumwa wa dhambi]. Lakini kwa kuwa hili linahitaji mabadiliko kamili, kufanywa upya kwa hali yetu nzima ya asili, ni lazima tujitoe kikamilifupi kwake.”¹⁵ Ubinafsi wetu huchukizwa, wivu, kukereka, kukasirika, nk. Mungu anataka kutuweka huru na tabia hizi.

13 E. G. White, *The Desire of Ages*, (1898), uk., S. 676

14 E. G. White, *The Desire of Ages*, (1898) uk.357.2 - Das Leben Jesu, 349 [357]

15 E. G. White, *Steps to Christ* (1892), uk. 43.2

“Yeye [Mungu] hutualika tujitoe kwake, ili atende mapenzi yake ndani yetu. Inabaki kwetu kuchagua kama tutawekwa huru kutoka kwenye utumwa wa dhambi, kushiriki uhuru wenyewe utukufu wa wana wa Mungu.”¹⁶

Mungu anajibu kujitoa kwetu kikamilifu kwa kuzaliwa upya (Yohana 3:1-21). Baada ya hapo inapaswa kuendelea kuwepo kwa kuendelea kujitoa (Yohana 15:1-17). Tataliongelea jambo hili Zaidi katika sura ya tatu.

Morris Venden anasema kuhusu kujitoa maisha yetu kwa Mungu:

“Hakuna jambo la kujitoa nusu nusu. Haiwezekani kabisa kujitoa nusu nusu kuliko iwezekanavyo kuwa mjamzito kiasi. Ni kwamba umejitoa kikamilifu au hujajitoa kabisa. Hakuna kuwa katikati.”¹⁷

Ellen White alisema maneno yafuatayo kuhusu kujitoa kila siku:

“Ni wale tu watakaokuwa watenda kazi pamoja na Kristo, wale tu watakao-sema, Bwana, jinsi nilivyo na vyote nilivyo navyo ni Vyako, watakaokubaliwa kama wana na binti za Mungu.”¹⁸

Hivyo mtu anaweza kuwa kanisani na bado akapotea. Inatisha kiasi gani! (Mfano wa wanawali kumi na ujumbe kwa kanisa la Laodikia pia hueleza hili.)

Kwa nini ni vigumu sana kuutambua Ukristo wa tabia ya mwilini?

Kwa kuwa maisha ya mtu wa tabia ya mwilini yamejazwa na “dini”, mara nyingi hatambui kwamba anakosa kitu fulani muhimu: uhusiano wa karibu na unaookoa pamoja na Mungu. Kama Kristo hajaruhusiwa kuongoza maisha yetu yote, basi amesimama mbele mlangoni akibisha (Ufu. 3:20). Na anasema: kama hali hii haibadiliki, basi nitakutapika.

Na kuna kitu kingine tena ambacho huhusika. Kupitia msingi wetu imara wa kimafundisho ambao umejengwa kwenye Biblia, tuna misimamo thabiti (Wakati huo huo tunahitaji kuwa tayari kupokea mawazo mapya.) Tunao uhakika kwamba tunauamini ukweli; hilo hutusisimua. Tuna maarifa mengi mazuri. Tunasema mambo sahihi. Hii ndiyo hufanya iwe vigumu zaidi kutambua tatizo la kuufuata mwili. Je haihusiki kwa namna yoyote endapo kiukweli nimewahi kuwa na Roho Mtakatifu? Kama sivyo, basi je ninaweza hata kutambua tofauti?

16 E. G. White, *Steps to Christ* (1892) uk. 43-4

17 Morris Venden, *95 Theses on Righteousness by Faith* (Pacific Press, 1987), uk. 63

18 E. G. White, *Desire of Ages*, uk. 523

Mchungaji fulani aliandika: "Nimepokea simu kutoka kwa dada, ambaye anashiriki katika kipindi chetu cha maombi ya muda wa siku 40. (Maelezo juu ya maombi ya muda wa siku 40 yanapatikana katika sura ya 5) alisema kwamba yamebadilisha maisha yake. **Alikuwa akishangaa maisha yake yote ni kitu gani kilichokuwa kimekosekana katika maisha yake ya kiroho na sasa alifahamu – Roho Mtakatifu.** Natamani ungeweza kusikia ushuhuda wake. Alisema kwamba aligundua kwa mara ya kwanza katika maisha kwamba alikuwa na mahusiano na Mungu. ...Wengine tayari walikuwa wamegundua badiliko lililokuwa limetokea maishani mwake." ¹⁹ Tunaweza kuona kwamba mtu anaweza kugundua kuwa kitu fulani hakipo, lakini hajui ni kitu gani. Wengi wanatamani mambo mengine zaidi lakini hawajui nini au namna ya kuyapata.

Ninashukuru kwamba i Wakorintho 3:3-4 inatumia maneno "*hata sasa*" mara tatu. "*Hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini.*" Hili hutuonyesha kwamba inawezekana kwa mtu wa tabia ya mwilini kuwa mtu wa kiroho. Hakuna mtu anayepaswa kubakia mtu wa tabia ya mwilini. Kwa kuwa yuko kanisani ana uwezekano mkubwa wa kutambua hili na kulibadilisha. Tutazungumza baadaye kuhusu namna unavyoweza kuwa mtu wa kiroho.

Jambo lingine la kufikiri ni husuda na fitina au kama Biblia inavyosema: "*ikiwa kwenu kuna husuda na fitina.*" Hii tabia huthibitisha kwa Paulo kwamba washiriki wa kanisa wa tabia ya mwilini hawaishi kwa nguvu ya Roho wa Mungu, bali hutenda kulinganana tabia ya mwilini – kama watu wengine. Wanaweza kutenda kama watu wa tabia ya asili; ingawa katika vazi la kidini. Je hili humaanisha kwamba mivutano ndani ya kanisa husababishwa na washiriki wa kanisa wenye mtazamo wa tabia ya mwilini? (Angalia Yuda fungu la 19). Je Mafarisayo na Masadukayo hawakushindana wao kwa wao wakati wa Yesu? Hili humaanisha kwamba tayari tangu huko nyuma kulikuwepo na mivutano kati ya watu wasiopenda mabadiliko na wale wanaopenda mabadiliko. Kundi moja lilikuwa na la waangalifu sana na lingine lilichukulia mambo kirahisi tu. Lakini makundi yote mawili yalikuwa na uhakika kwamba walikuwa na tafsiri na mtazamo sahihi juu ya Biblia. Lakini Yesu alituonyesha kwamba makundi yote mawili yalikuwa na tabia ya mwilini, ikimaanisha kutokujazwa na Roho Mtakatifu kunaweza pia kutufanya kuwa Wakristo wa tabia ya mwilini. Jambo kama hilo pia linawezekana leo. Wakristo wenye misimamo mikali wanaweza pia kuwa Wakristo wa tabia ya mwilini.

¹⁹ Email an H. Haubeil – received on February 15, 2012

Bahati Mbaya, watu leo hutazama katika miwani ya “watu wenyewe msimamo mkali au wale wasio na msimamo mkali”. Faida ya jambo hili ni kwamba mtazamaji huona kila kitu ni sahihi. Hata hivyo, kwa mgawanyo wa Kibiblia wa “mtu wa tabia ya mwilini au wa rohoni” tunapewa changamoto ya kufuata tathmini ya kiroho. Tunapaswa kufanya hili kwa manufaa yetu wenyewe. Fikiri kile ambacho Mungu hutwambia wazi katika Wagalatia 6:7-8 NKJV:

“...chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele.”

Mtu wa mwilini anataka kumfuata Yesu na kumpendeza Yeye, lakini hajajitoa kikamilifu maisha yake yote kwa Yesu au ikiwa amejitoa basi kwa kiasi fulani amerudi nyuma. (Wagalatia 3:3; Ufunuo 2:4-5). Hilo humaanisha kwamba yeye, labda kwa kutokujitambua, anataka kuishi kulingana **na mapenzi ya Mungu** na matamanio yake mwenyewe **kwa wakati mmoja**. Lakini hilo haliwezekani. Hatimaye anayachukua maisha yake mwenyewe mikononi mwake. Kama methali hii isemavyo, kuna nafsi mbili zinaishi kifuanini mwake. Je Mungu anaweza kumtuma Roho Mtakatifu katika hali kama hiyo? Yakobo 4:3 NKJV hutoa jibu hili: *“Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya.”* Nimefikia kwenye hitimisho kwamba hii humaanisha kuomba kwa mtazamo wa tabia ya mwilini. Je jibu kwa ombi kama hilo halitaongeza hali ya kujisikia? Vile vile, huyu mshiriki wa kanisa anaishi kwa nguvu na uwezo wa kawaida wa kibinadamu. Katika Ufu.3:16 hali hii inaitwa “vuguvugu” na katika Mathayo 25 “mpumbavu.”

Kwa nini Yesu anawaita washiriki wa kanisa wa tabia ya mwilini vuguvugu?

Kwa nini Wakristo wengi wanakosa uzoefu na Roho Mtakatifu? Ili kuweza kujibu swali hili, kwanza tutapaswa kuangalia suala la laodikia. Kwa nini Yesu anaita waumini katika kanisa la Laodikia vuguvugu? Anatupatia ishara ya wazi: *“Tazama nasimama mlangoni nabisha.”* (Ufu.3:20) Yesu hakuwa kiini cha maisha ya waumini, bali alikuwa nje. Alikuwa amesimama nje ya mlango. Kwa nini hakuingia ndani? Kwa sababu hakuwa amekaribishwa. Halazimishi kuingia ndani, kwa sababu anaheshimu uhuru wetu wa maamuzi.

Kwa nini waumini humuacha Yesu nje mlangoni? Kuna sababu tofauti kwa jambo hili. Baadhi hufuata uwezo wao wa akili na utambuzi wao katika maisha yao ya kiroho kama mwaandishi Nikodemus na hawaelewi maisha ya Kikristo ikoje. (Linganisha na Yohana 3:1-10.) Kwa wengine “bei” ya kuwa mwanafunzi

ni juu mno, wana mambo mengi mno watatakiwa wayaache, kama yule kijana mwenye mali mengi. (Linganisha na Mathayo 19:16-24) Kumfuata Yesu kunahitaji kujikana nafsi na utayari wa kubadilisha maisha yake (Linganisha na Mathayo 16:24-25) na kujitoa kikamilifu kwa Mungu. (Warumi 12:1). Kumuacha Yesu nje kunawenza kusababishwa na upuuziaji wa hali ya juu—kutokuwa na muda wa kutosha katika ushirika binafsi na Yesu.

Ninarudia: sababu ya uvuguvugu katika Ufu. 3:20 ni: “*Tazama ninasimama mlangoni.*” Yesu hayuko kwenye kitovu cha maisha yao, bali yuko nje au pemberi. Hivyo uvuguvugu unahuusu uhusiano binafsi na Kristo. Katika maeneo mengine mtu anayehusika sio lazima awe vuguvugu

Kwa mfano: mume anaweza kujikita sana kwenye kazi yake lakini wakati huo huo akampuuza mke wake. Amejitoa kwenye kazi yake, lakini ni vuguvugu katika mahusiano yake ya ndoa. Mtu anaweza kuwa hata mshiriki wa kanisa aliyejitoa, kiongozi makini au mchungaji au kiongozi mkuu wa kanisa na bado akawa vuguvugu katika uhusiano wake na Kristo. Mtu huyo amejitoa sana kukamilisha kazi nyingi, kiasi kwamba anapuuzia uhusiano wake binafsi na Kristo. **Huu ndiyo uvuguvugu ambao Yesu anataka uondolewe.** Ni hatari kwamba mtu anaweza kujishughulisha sana na kazi ya Mungu (ndani ya kanisa na kazi ya kimishenari) kiasi kwamba anampuuza Bwana wa kazi.

MFANO WA WANAWALI KUMI

Mfano wa Yesu wa wanawali kumi hutuambia nini kuhusiana na washiriki wa kanisa wa kiroho na wenye tabia ya mwilini?

- ▶ Wote 10 walikuwa wanawali
- ▶ Wote walikuwa na Imani safi ya kibiblia
- ▶ Wote walikuwa na taa
- ▶ Wote walikuwa na Biblia
- ▶ Wote walikwenda kumpokea bwana arusi
- ▶ Wote walitazamia kuja kwa mara ya pili
- ▶ Wote walilala
- ▶ Wote walisikia sauti na kuamka
- ▶ Wote waliandaa taa zao
- ▶ Taa zote zilikuwa zinawaka
- ▶ Nusu yao waligundua kuwa taa zao zilianza kuzimika

Wote waliandaa taa zao **na taa zao zote zilikuwa zinawaka;** lakini taa zinazowaka **zinahitaji mafuta. Nishati ilitumika.** Baada ya muda mfupi watano

katiyao *waligundua kuwa taa zao zilianza kuzimika*. Taa za wanawali wapumbavu ambazo ziliwaka kwa muda mfupi tu hutuonyesha kwamba walikuwa na kitu fulani kutoka kwa Roho Mtakatifu. Lakini hakikutosha. Kulikuwa na mafuta kidogo sana. *Hiyo ndiyo tofauti pekee iliyoukwepo.*

Wakati wale watano [wapumbavu] walipoomba kuingia ndani, Yesu alijibu: “*Siwajui ninyi.*” Walikuwa wamechelewa mno kupata mafuta, Roho Mtakatifu. Mlango ulibaki umefungwa.

Kauli ya Yesu hutuonyesha kwamba uhusiano wetu binafsi na yeYe hutegemea Roho Mtakatifu. Yeyote ambaye haruhusu kuongozwa na Roho Mtakatifu hatakubaliwa na Yesu. Katika Rum. 8:8-9 imeandikwa: “*Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.... Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.*”

Kwa kweli, tunakuwa *tu* na mahusiano binafsi halisi na Yesu kupitia Roho Mtakatifu.¹ Yohana 3:24 inasema: “*Na katika hili tunajua ya kuwa [Yesu] anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.*” Hili humaanisha kwamba uhakika nilio nao kwamba nimejazwa na Roho Mtakatifu ni uhakika huo huo kwamba niko ndani ya Yesu na yeYe ndani yangu.

Huu ndiyo usoefu hasa ambaeo huyu dada alikuwa nao, yule aliyeshiriki muda wa siku 40 za maombi. Kupitia uwepo wa Roho Mtakatifu maishani mwake alipata usoefu wa mahusiano yake na Mungu katika uelekeo tofauti kabisa na wengine waligundua badiliko maishani mwake. Dada mmoja kutoka Ujerumani ya kusini aliandika haya baada ya kusoma hichi kitabu: “Pamoja na kitabu cha “40 Days – Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming’ kilichoandikwa na Dennis Smith na kitabu hiki vimekuwa mbaraka mkubwa na uliosubiriwa kwa muda mrefu maishani mwangu. Kama ilivyo kwa washiriki wengine wengi wa kanisa na dada kutoka kanisa letu walivyopata usoefu, kitu fulani kilikuwa kinakosekana wakati wote katika usoefu wetu wa imani na sasa tuna fursa ya kufahamu jinsi Yesu alivyoingia maishani mwetu na ameanza kutubadilisha. Bado anafanya kazi ndani yetu na hatua kwa hatua anatusogeza karibu naye.”²⁰

Kaka mmoja aliandika yafuatayo: Kitabu cha *Hatua za Uamsho Binafsi* kimenigusa sana. Sura inayozungumzia wanawali kumi na hasa Warumi 8:9b: ‘*Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake*’ imenishtua sana. Ghafla, sikuwa na uhakika kama nilikuwa na Roho Mtakatifu na kama alikuwa anafanya kazi ndani yangu, kwa sababu ninakosa kwa uchungu “matunda” maishani mwangu. Sabato hii mchana nimemaliza kusoma kitabu

²⁰ Email from March 31, 2013

chote na huzuni kubwa imenitawala. Kisha nikasoma ombi katika ukurasa wa 108 na shauku kuu ikaamshwa ndani yangu ya kupokea Roho Mtakatifu, kwamba moyo wangu ungebadilishwa na kwamba Mungu Baba angenibadilisha kulingana na mapenzi yake. Asante kwa kitabu na maneno, ambayo yamenigusa kabisa.” A. P.

Hatarı kubwa sana kwa Mkristo wa tabia ya mwilini ni kwamba hataweza kuupata uzima wa milele kama hali yake haitabadilika. Warumi 8:9b: “*Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.*”

Kwa muhtasari: Tofauti kuu kati ya mshiriki wa kanisa wa kiroho na wa tabia ya mwilini ni Roho Mtakatifu. Mkristo wa kiroho amejazwa na Roho Mtakatifu. Mkristo wa tabia ya mwilini hana au hajajazwa na Roho Mtakatifu kwa kiwango cha kutosha.

Ukigundua kuwa wewe ni Mkristo wa tabia ya mwilini usikasirike. Mungu anakupatia tiba: Roho Mtakatifu

Katika makundi mengine Roho Mtakatifu anasisitizwa kupita kiasi; kwa upande mwingine, katika makundi mengine anapuuzwa. Mungu atuongoze katika njia sahihi ya Biblia.

ULINGANIFU: KANISA LA AWALI NA KANISA LA NYAKATI ZA MWISHO

Tunapolinganisha kanisa la awali na kanisa la sasa, tunagundua kwamba kanisa la awali lazima lilikuwa kwa kiasi kikubwa limeundwa na watu wakiroho. Kitabu cha Matendo huonyesha kwamba hii ilikuwa sababu kwa ya maendeleo yao chanya naya haraka. Hawakuwa na msaada mwingine. Lakini walikuwa na Roho Mtakatifu. Tuna misaada mingi imejaa tele. Lakini tuna ukosefu wa Roho Mtakatifu.

Kumbuka kile alichokisema A. W. Tozer: “Kama Roho Mtakatifu angeondolewa kanisani kwetu leo, asilimia 95% ya kile tunachokifanya kingeendalea na hakuna mtu ambaye angegundua tofauti. Ikiwa Roho Mtakatifu angeondolewa kwenye kanisa la awali, basi asilimia 95% (hii humaanisha karibu kila kitu) kile walichokuwa wanakifanya kingesimama na kila mtu angegundua tofauti.”²¹

²¹ Dr. S. Joseph Kidder, *Anleitung zum geistlichen Leben* (Andrews University), PPP Folie 2

**Je tumejifunza kuishi bila ya Roho Mtakatifu?
Je kanisa leo lina idadi kubwa ya Wakristo
wa tabia ya mwilini tu?**

Matokeo yake, mara nyingi hatuna nguvu na kwa kiwango kikubwa hatuna ushindi? Je mtazamo wa mtu wa tabia ya mwilini unahusiana na ukweli kwamba tuna ukuaji dhaifu tu wa kanisa katika sehemu nyingi? Je matatizo makubwa mengi katika maeneno mengi hutokana na mitazamo ya tabia ya mwilini? Tutaendelea kugundua zaidi kwamba tatizo letu binafsi na kuu ni ukosefu wa Roho Mtakatifu. Katika eneo la mtu binafsi tunaweza kulibadilisha kwa haraka kwa msaada wa Mungu.

Maelezo yafuatayo kwa ajili ya wachungaji kwa kawaida hutumika kwa kila mmoja.

Johannes Mager anasema. "Paulo hutofautisha kati ya Wakristo wa kiroho na wale wa tabia ya mwilini, kati ya wale waliojazwa na Roho Mtakatifu na wale ambao hawana nafasi kwa ajili ya Roho Mtakatifu maishani mwao: waliobatiwa na Roho Mtakatifu, lakini hawajazwa na Roho Mtakatifu.

Kwa wachungaji hili humaanisha kwamba: Ninaweza kuwa na mafunzo mazuri ya kiteologia, kuwa na uelewa mzuri wa lugha za kibiblia na kufasili kwa ufasaha maandiko matakatifu; Ninaweza kuwa nimepokea kweli kuu za kibiblia kiakili na kuzielewa na kuwa na uelewa mzuri wa theologia ya imani ya kanisa ya karne mbalimbali; ninaweza kuwa na ustadi mzuri wa kuhubiri na kuhubiri masomo yenye manufaa na yenye uhalisia – na pamoja na maarifa yangu yote nisijazwe na Roho Mtakatifu. Vitabu, elimu, vifaa vizuri vya kufundishia, hata haiba ni mbadala kwa ajili ya maisha yaliyojazwa na Roho Mtakatifu ambayo yanakosekana.

Kuhubiri, kuomba kwenye mikusanyiko ya watu, kuongoza maisha ya kanisa, kuandaa vipindi vya kiinjilisti, kutoa mashauri ya kichungaji–haya yote mtu anaweza kujifunza na pia kuyatenda pasipo Roho Mtakatifu. Ellen G. White anaelezea uwezekano huu wa kutisha kama ifuatavyo: "Sababu inayofanya kuwepo na kiwango cha chini cha udhihirisho wa Roho wa Mungu ni kwamba wachungaji hujifunza kufanya kazi bila Yeye" (E. G. White, *Testimonies for the Church*, Volume 1, (1868), uk. 383.1).

Johannes Mager alikuwa mchungaji, mwinjilisti na profesa wa theologia ya utaratibu kwa miaka mingi. Mwisho alifanya kazi kama katibu wa idara ya huduma za kichungaji ya Divisheni ya Ulaya na Afrika (kwa sasa: Divisheni ya Ulaya na Kati) huko Bern, Uswisi. Kwa sasa amestaafu na anaishi huko Friedensau, Ujerumani²²

22 Johannes Mager, *Auf den Spuren des Heiligen Geistes (Following the Steps of the Holy Spirit)*,

Kufupisha: Kuwa mtu wa tabia ya mwilini humaanisha kuishi kwa uwezo na nguvu za kawaida za kibinadamu pasipo Roho Mtakatifu au kuwa na kiwango cha kutosha cha Roho Mtakatifu.

KIZUIZI KIKUU KATIKA UKRISTO WA TABIA YA MWILINI

Kanuni kuu za Biblia – kumpenda adui yako, kusamehe watu kwa kila jambo, kushinda dhambi, n.k. – zinaweza tu kufikiwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, si kwa juhudhi za kibinadamu. Hili hutuonyesha kuwa tatizo kubwa katika Ukristo wa tabia ya mwilini ni maisha yaliyojengwa katika uwezo wa kibinadamu tu. Hatuwezi kufanya mapenzi ya Mungu peke yetu kwa nguvu zetu wenyewe. Tusome mafungu machache ya Biblia katika mada hii:

Isaya 64:6 : “*na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi.*”

Jeremia 13:23 NKJV: “*Je! Mkushi aweza kuibadili ngozi yake, au chui madoadoa yake? Kama aweza, ndipo na ninyi mwaweza kutenda mema, ninyi mlizoea kutenda mabaya.*”

Ezekieli 36:26-27 NKJV: “*Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu... Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda.*”

Warumi 8:7 NKJV: “*Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.*” Tafsiri nyingine: “*Nia iliyogozwa na mwili inamchukia Mungu; haijifuati sheria ya Mungu, na haiwezi kufanya hivyo.*”

Ellen White alisema wazi kabisa na kwa usahihi:

“*Yeye anayejaribu kufika mbinguni kwa matendo yake mwenyewe kwa kuishika sheria, anafanya jambo lisilowezekana. Mwanadamu hawesi kuokolewa pasipo utii, bali matendo yake hayapaswi kuwa ya kwake mwenyewe; Kristo anapaswa kufanya kazi ndani yake kuwa tayari na kufanya matendo yake mema.*”²³

(Lüneberg, 1999), pages 102-103.

²³ E. G. White, *Review and Herald*, July 1, 1890

Nafikiri nukuu hizi zinaonyesha nya kutosha kwamba hatuwezi kufanya mapenzi ya Mungu pasipo Roho Mtakatifu. Jambo kubwa linalotusumbua ni kwamba mara nyingi tunahitaji kufanya uamuzi kwa ajili ya mapenzi ya Mungu na kwamba Mungu hutupatia nguvu ya kuutekeleza. Ufahamu huu wa fundisho la haki kwa imani ni muhimu sana na hutupatia uhuru. Hatahivyo hatuwezi kulielezea kwa undani hapa.

NINI KINACHOWEZA KUTOKEA, WAKATI WATU FULANI WANAPOJARIBU KUFANYA JAMBO LINALOZIDI UWEZO WAO?

Ninihutokea kila mara ninapogundua: Siwezi kufanya hivyo! Sasa nimeanguka tena! Nifakiri kwamba kwa kiwango fulani huwa tunakata tamaa.

Nafikiri tatizo hili ni kubwa zaidi kwa vijana kuliko watu wazima. Watu wazima wamezoea kuwa na hali ya kujituma, utii ndani ya familia, shule, na biashara. Hivyo hawasumbuliwi kirahisi na masikitiko kama ilivyo kwa vijana. Lakini tatizo lipokwa wote vijana na watu wazima. Ila kijana huligundua zaidi. Kusafiri njia ya imani kwa nguvu zao wenyewe ni tatizo la kwanza la kila Mkristo wa tabia ya mwilini, awe anafahamu hilo ama la.

Ni kwa namna gani tunajaribu kutatua tatizo hili? Mtu mmoja anaweza kuomba sana kwa ajili ya msaada wa Mungu na kuamua kujaribu kwa bidii. Mtu mwagine anaweza kufikiri kwamba hatupaswi kuwa na mtazamo finyu kiasi hicho. Sasa huanza kuchukulia mambo kwa kubahatisha na kujiona huru zaidi. Lakini bado mwagine anaweza kuachana na imani yake kabisa na hata anaweza kujihisi vizuri. Tatizo pekee ni kwamba ufumbuzi huu wote ni wa uongo, kwa sababu hakika madhara yatakuja upesi au baadaye. Njia sahihi ni kuzichukulia sheria za Mungu kwa umakini, kwa sababu zilitolewa kwa upendo na zipo kwa faida yetu. Hata hivyo tunahitaji uweza wa Mungu kwa ajili ya hili. Njia sahihi ni kuishi kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kwa furaha, hamasa, nguvu, kuzaa matundana ushindi.

TATIZO KUU

Nafikiri tumegundua kwamba hili hasa linahusiana na Ukristo wa tabia ya mwilini. Je haiko wazi zaidi na zaidi kwa nini Yesu hataki wafuasi vuguvugu? Hawana uzima tele kama Mungu anavyotaka kutupatia na ni mfano mbaya japokuwa wengi wao hawafahamu hilo. Tatizo ni kubwa zaidi kuliko tunavyofikiri. Wakristo walioongoka nusu nusu ni wabaya kuliko wasioamini; kwa maneno yao ya uongo na hali yao ya kutokujitoa huongoza wengi katika upotevu.”²⁴

²⁴ ECW Letter 44, 1903, quoted in *Adv. Bible Commentary*, Vol.7, uk.963 on Rev. 3:15-16

Katika kitabu kiitwacho Christ our Righteousness kilichoandikwa na Arthur G. Daniells tunasoma yafuatayo: "Lakini kushika desturi ni kitu kidanganyifu sana na kiharibifu sana. Ni jabali lililojificha, lisilotarajiwa, ambalo limetishia kuliharibu kanisa mara nyangi katika karne zote. Paulo alituonya kwamba hii 'mfano wa utauwa' (2 Timotheo 3:5) pasipo uwezo wa Mungu [bila kujazwa na Roho Mtakatifu] ingekuwa mojawapo ya hatari za siku za mwisho na kutuonya tusidanganywe na mtazamo huu wa kuridhika na unaodanganya nafsi."²⁵

Baadhi ya sababu zinazoongoza kwenye Ukristo wa Tabia ya Mwilini

Sababu au mambo yafuatayo huweza kuongoza kwenye Ukristo wa tabia ya mwilini:

1. **Ujinga** – Hatujajitoa kikamilifu kwenye mada ya "maisha pamoja na Roho Mtakatifu" au hatujapata ufunguo wa kuiweka mada hii katika vitendo.
2. **Kutokuwa na Imani au kuwa na Imani Kidogo** – Kujazwa na Roho Mtakatifu kuna sharti la kuyatoa maisha yetu kikamilifu kwa Yesu Kristo. Hili pia linaweza kutokea kwa sababu ya kuwa ujinga, au labda kwa sababu tunaogopa kwamba Bwana atatuongoza tofauti na tunavyotaka. Hili humaanisha kwamba hatuamini nya kutosha upendo na hekima ya Mungu
3. **Dhana Potofu** – Mtu anaweza kufikiri kwamba amejazwa na Roho Mtakatifu, japo kuwa kiuhalisia hajajazwa au wamejazwa kwa kiasi cha kutosha. Hili huonekana kuwa tatizo linalojitokeza mara kwa mara.
4. **Kuwa na Shughuli Nyingi** – Watu wametingwa na shughuli nyangi sana kiasi kwamba wanafikiri hawana muda kabisa au hawana muda wa kutosha wa kudumisha mahusiano na Kristo. Au wana muda, lakini hawapigi hatua yoyote kuijunganisha na Mungu.
5. **Dhambi za Siri**, huenda ulipaji fidia – Hii ni kama mkato wa mzunguko wa umeme, ikimaanisha hakuna muunganiko pamoja na nguvu ya Mungu.

²⁵ Arthur G. Daniells, *Christ our Righteousness*, uk. 30, - Christus unsere Gerechtigkeit (Hamburg 1962), S.20

6. Mara nyingi kutenda kulingana na hisia zao. Neno la Mungu linasema: “*Mwenye haki ataishi kwa imani*”. Je ninafanya maamuzi kwa kumwamini Mungu au kulingana na hisia zangu? Maelezo haya kutoka kwa Roger Morneau yamenigusa sana: “*Roho [mapepo] zingewahamasisha watu kusikiliza hisia zao badala ya Neno la Kristo na manabii wake. Hakuna njia yenyehu uhalika zaidi ambazo roho zingepata kudhibiti maisha ya watu pasipo watu kutambua kile kilichokuwa kinatokea.*”²⁶

Kwa nini ninapaswa kuomba Roho Mtakatifu, japokuwa tayari nimejazwa na Roho Mtakatifu?

Kwa upande mmoja, Roho Mtakatifu alitolewa kwetu ili aakee pamoja nasi. Kwa upande mwengine, tunapaswa kuendelea kuomba kwa imani kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Tunatatua vipi utata huu ulio wazi?

Kwa upande mwengine:

Yesu alisema katika Yohana 14:17: “*Maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.*” Matendo 2:38 inasema: “*Petro akaawaambia, Tubuni mkabatizwe ... kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*”

Kwa upande mwengine:

Wakati Yesu alipofundisha kuhusu maombi, alisema katika Luka 11:9-13: “... ombeni nanyi mtapewa; je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao warmwombao?” Waefeso 5:18 inasema: “... mjazwe Roho.” Katika pande zote mbili katika maandishi ya awali ya Kiyunani, ni ombi linaloendelea.

Suluhihisho:

E. G. White anasema: “Utendaji wa Roho wakati wote hupatana na Neno la Mungu. Kama katika ulimwengu wa asili, ndivyo iliyivo katika ulimwengu wa kiroho. Maisha ya asili huhifadhiwa kila wakati kwa uweza wa kiungu; hata hivyo hayaendelezwi kwa muujiza wa moja kwa moja, bali kuititia matumizi ya mibaraka iliyowekwa ndani ya uwezo wetu. Hivyo maisha ya kiroho yanaendelezwa kwa kutumia njia ambazo Mpaji amezitoa. Endapo mfuasi wa Kristo angekua na’kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo’ (Waefeso 4:13), ni lazima ale mkate wa uzima na kunywa maji ya wokovu. Ni lazima akeshe na kuomba na kufanya kazi, katika mambo yote akiyafuata maagizo ya Mungu ndani ya neno lake”²⁷

²⁶ Roger Morneau, A Trip into the Supernatural, Review and Herald 1982, uk. 43

²⁷ E. G. White, *The Acts of the Apostles*, (1911), uk. 284.2

Tulipokea uhai tulipozaliwa. Ili kuendeleza maisha haya tunapaswa kula, kunywa, kufanya mazoezi n.k. ndivyo ilivyo katika maisha yetu ya kiroho. Tunaye Roho Mtakatifu kuititia ubatizo wetu kwa njia ya majina Roho (kuzaliwa upya) ili kwamba haya maisha ya kiroho yabaki maisha yetu yote. Ili kuyaendeleza haya maisha ya kiroho ni muhimu kutumia mbinu za kiroho ambazo Mungu ametupatia: Roho Mtakatifu, Neno la Mungu, maombi, usuhudla wetu, n.k.

Yesu alisema katika Yohana 15:4: “*Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu.*” E. G. White anasema hivi kuhusu jambo hili: Kukaa ndani ya Kristo humaanisha kuendelea kupokea Roho wake, maisha ya kujitoa kikamilifu kwa kazi yake.”²⁸

Ndiyo maana tunahitaji kila siku kuomba Roho Mtakatifu kwa imani na kujitoa wenyewe kwa Bwana kila asubuhi kwa kila tulicho nacho na jinsi tulivyo.

NINASIMAMA WAPI?

Sasa jambo kubwa la muhimu ni kuamua nipo katika kundi gani. Ninasimama wapi?

Wakati mama yangu mpendwa alipokuwa na umri wa miaka 20 alimjibu mtu fulani kwa kusema kwamba hakuvutiwa na imani. Kisha yule mtu alimjibu: Na kama ukifa usiku wa leo? Neno hili likamgusa sana. Lakini lilikuwa na athari chanya. Lilimuongoza kufanya maamuzi kwa ajili ya Yesu na kanisa lake. Huenda swali hili litakusaidia pia na wewe:

*Chukulia...umekufa leo...! (mshtuko wa moyo? ajali?) Je una uhakika wa uzima
wa milele pamoja na Yesu Kristo?
Usibaki bila uhakika.*

Jambo la Kutisha

Nina hofu sana kwa kuwa nimeanza kuelewa ukubwa wa tatizo hili. Nimetafakari na kuomba kama kweli ninapaswa kuongeza aya hii. Ninajaribu kwa kuwa hili ni suala la furaha katika maisha haya na uzima wa milele na hasa kwa sababu lina mvuto kwenye ndoa na kwenye familia na vile vile kanisani na kazini. Sijui linamhusu nani. Lakini ninataka kuwa wa msaada kwa watu wanaohusika, kwa kuwa mimi pia nimesaidiwa. Ni muhimu kwamba kila mtu ambaye ana tabia ya mwilini atambue jambo hili; vinginevyo hawezikubadilika kwa msaada

²⁸ E. G. White, *The Desire of Ages*, (1898), uk. 676.2

wa Mungu. Mungu kwa upendo wake anataka kutubariki zaidi kwa kuwa na uhusiano wa karibu sana na Yesu Kristo kuitia Roho Mtakatifu. Matokeo yake hasara kubwa inaweza kuepukwa na mbaraka usiopimika unaweza kupokelewa. Na jambo la kushangaza ni kwamba tunawenza kurekebisha hali hii upesi kwa msaada wa Mungu. (Kwa maelezo zaidi sura ya 3 na ya 5)

Tatizo la Ukristo wa tabia ya mwilini limeelezwa ndani ya Biblia kwa namna mbalimbali. Makundi ya watu na watu ndani ya makundi wanaweza kuwa na mitazamo tofauti kabisa, lakini tatizo kuu ni lile lile. Maelezo tofauti ni:

- ▶ “**Watu wa mwilini au wa tabia ya mwilini**” – Warumi 8:1-17; 1 Kor. 3:1-4, Gal. 5:16-21 na mafungu mengine
- ▶ “**mpumbavu**” – mfano wa wanawali kumi Matt. 25:1-13
“Hali ya Kanisa iliyowakilishwa na wanawali wapumbavu, pia huzungumzwa kama hali ya Laodikia.”²⁹
- ▶ “**vuguvugu**” – barua kwa Laodikia Ufu. .3:14-21
“Ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto.”(Ufu. 3:15). Je si jambo jema? Yesu anapendelea baridi kuliko vuguvugu. Sababu zake ni zippi katika hili? “Wakristo waliojitoa nusu nusu ni wabaya kuliko wasioamini; kwa maneno yao ya uongo na kutokujitoa kwao huongoza wengi katika upotevu. Asiyeamini huonyesha makosa yake. Wakristo vuguvugu hudanganya pande zote. Yeye si mwema kidunia wala si Mkristo mwema. Shetani humtumia kufanya kazi kuliko mtu ye yote anavyoweza kufanya.”³⁰
- ▶ “**kutokuzaliwa mara ya pili**” au kutobaki katika hali hii ya kuzaliwa mara ya pili – Yohana 3:1-21
“Kuzaliwa upya ni uzoefu wa nadra katika zama hizi za ulimwengu. Hii ni sababu kwa nini kuna mkanganyiko mwingu makanisani. Wengi, wengi sana, wanaotumia jina la Kristo hawajatakasika na si watakatifu. Wamekwisha batizwa, lakini walizikwa wakiwa hai. Nafsi haikufa, na kwa hiyo hawakufufuka katika upya wa uzima ndani ya Kristo.”³¹
- ▶ **mfano wa utauwa** – “*Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake*”. 2 Tim 3:5 Arthur G. Daniells anasema manano yafuatayo kuhusu hili:
“... Lakini kushika desturi ni kitu kidanganyifu sana na kiharibifu sana. Ni jabali lililojicha, lisilotarajiwa, ambalo limetishia kuliharibu kanisa mara nydingi katika

²⁹ E. G. White, *Review and Herald*, Aug. 19, 1890

³⁰ E. G. White, Letter 44, 1903, quoted in the *Seventh Day Adventist Bible Commentary*, Vol.7, p. 963 on Rev. 3:15,16

³¹ E. G. White, MS 148, 1897, quoted in the *Seventh Day Adventist Bible Commentary* Vol.6, uk. 1075 Many buried alive

karne zote. Paulo alituonya kwamba huu ‘mfano wa Utauwa’ (2 Tim 3:5) bila nguvu za Mungu [pasipo kujazwa na Roho Mtakatifu] utakuwa mojawapo ya hatari za siku za mwisho na anatuonya tusidanganywe na huu mtazamo wa kuridhika, unaodanganya nafsi.”³²

Na pia kuna maelezo ya kushtusha katika machapisho ya Ellen White:

► **Wachache, wachache sana**

“Kwenye ndoto yangu askari (mlinzi) alisimama kwenye mlango wa jengo muhimu, na alimuuliza kila mmoja aliyekuwa akiingia, ‘Je umepokea Roho Mtakatifu.’ Kamba ya kupimia ilikuwa mkononi mwake, na ni wachache tu, wachache sana walioruhusiwa kuingia ndani ya jengo.”³³

► **Hakuna hata mtu mmoja kati ya watu ishirini aliye tayari**

“Ni maneno ya pekee ambayo ninaliambia kanisa, kwamba hakuna hata mtu mmoja kati ya watu ishirini ambao majina yao yapo katika vitabu nya kanisa ambao wamejiandaa kufunga historia yao ya duniani, na hakika watakuwa pasipo Mungu na bila tumaini ulimwenguni kama mdhambi wa kawaida.”³⁴

► **Kwa nini tumelala sana?**

“Kwa nini maaskari wa Kristo wamelala sana na hawajali? Kwa sababu wana muunganiko halisi kidogo sana pamoja na Kristo; kwa sababu wana upungufu mkubwa sana wa Roho wake.”³⁵

► **Hatari kubwa**

“Sitatumia muda mwingi hapa kuelezea ufupi na kutotabirika kwa maisha; lakini ipo hatari kubwa – hatari ambayo bado hajaeleweka vizuri – kwa kuchelewa kujitoa kwa sauti inayosihi ya Roho Mtakatifu, kwa kuchagua kuishi dhambini; kwa kuwa ndivyo kuchelewa huku kulisyo hasa.”³⁶ Ni kitu gani kipo kwenye kiini cha dhambi? “Kwa sababu hawani amini mimi.” (Yohana 16:9) Ishara inayoonyesha kwamba kwa kweli tunamwamini na kumtumaini Yesu ni kuwa tunajitoa kwake kikamilifu. Inahusu kujitoa kwetu kikamilifu; utayari wetu wa kumfuata Yeye katika kila jambo.

Ninataka kusema hili kwa mara nyingine: Nitatumia fursa ya kuongeza hii aya muhinu sana, kwa sababu inahusiana na furaha yetu binafsi maishani na uzima wetu wa milele, na pia na mvuto wetu hasa katika ndoa zetu, familia zetu na makanisani kwetu.

³² A. G. Daniells, *Christ our Righteousness*, uk. 20

³³ E. G. White, *Selected Messages*, Vol. 1 (1958), uk. 109.2

³⁴ E. G. White, *Christian Service* (1925), uk. 41.1

³⁵ E. G. White, *The Great Controversy* (1911), uk. 507.3

³⁶ E. G. White, *Selected Messages*, Vol. 1 (1958), uk. 109.2

Maswali na Maswali Zaidi

Swali muhimu ni kama umejazwa na Roho Mtakatifu au la. Lakini ni wakati gani mtu anajazwa na Roho Mtakatifu? Ni yapi masharti ya muhimu? Yapi matokeo chanya ya maisha pamoja na Roho Mtakatifu? Kitu gani hutokea, wakati gani unapofikiri kimakosa kuwa umejazwa na Roho Mtakatifu?

Shukuru kwa Ishara

Mshukuru Mungu kwamba tunajitoa zaidi kwa ajili ya mada ya uamsho. Ninafikiri kwamba Mungu wetu mkuu na wa kustaajabisha ana sababu muhimu kwa kutupatia wakati huu msukumo wa Roho Mtakatifu kwa ajili ya uamsho. Je zifuatazo zinaweza kuwa sababu?

- ▶ Anataka kuondoa udhaifu wetu na kutunasua kutoka kwenye hali yetu inayofanana na ya Ulaodikia.
- ▶ Anataka kutuandaa kwa ajili ya ujio wa Yesu mara ya pili ambaao ni karibu na kipindi maalum kabla tu hilo halijatokeea.
- ▶ Anataka kuleta uamsho mkuu wa mwisho (Ufu.18:1-2) ulimwenguni kupitia wale, “*wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu*” (Ufu. 12:17 NKJV) na wana “*imani ya Yesu.*” (Ufu.12:17 NKJV)

Pia tumshukuru Mungu kwamba kila Mkristo wa tabia ya mwilini kwa haraka anaweza kuwa Mkristo wa kiroho. Na kwamba kila mmoja anayeishi ndani ya Roho Mtakatifu anaweza kukua katika utimilifu wa Kristo. Hii sasa ni kazi yetu inayofuata. Sasa kwa ajili ya uzoefu mwingine zaidi mwisho wa sura hii.

Motisha Mpya na Furaha ya Ndani

“Dada mmoja kanisani alinipatia kitabu ‘*Hatua za Uamsho Binafsi.*’ Niliguswa sana na maelezo yaliyokuwa ndani ya kitabu. Kwa muda mrefu nimekuwa nikitafuta kitu fulani kama hiki na mwishowe nimekipata. Kisha nikaanza kupanga maisha yangu ya kiroho na ndipo nilipotambua kwamba nilipaswa kufanya kitu fulani: Nilijitoa kikamilifu kwa Yesu. Tangu hapo na kuendelea Bwana aliniamsha asubuhi na mapema na kunipatia muda wa kufanya ibada binafsi. Kila siku nilisoma sura ndani ya kitabu cha Siku 40. Niligundua wazi kwamba uhusiano wangu pamoja na Yesu ulikuwa na kuongezeza. Ukawa wa kina zaidi na wa binafsi zaidi. Roho Mtakatifu alikuwa akifanya kazi ndani yangu. Baada ya kitabu cha Siku 40, nilisoma kitabu cha pili cha Siku 40. Tangu

hapo nimesoma kila kitabu kati ya hivi mara nne. Siwezi kufanya chochote isipokuwa kila siku kuomba ushirika pamoja na Mungu. Matokeo haya ni mazuri, kwa sababu motisha yangu mpya na furaha yangu ya ndani haiwezi kubakia isitambulike. Katika kipindi hiki nimekuwa naupendeleo wa kuwa na uzoefu mwingi pamoja na Mungu. Pia nimetafuta fursa kuwaambia wengine uzoefu wangu. Uhusiano wa karibu pamoja na Yesu hufanya mambo mengi kutokuwa na umuhimu na mahitaji yasiyo ya maana hupatiwa ufumbuzi. Ninategemea na kuomba kwamba watu wengi watakuwa na uzoefu huu ambao nimependelewa kuwa nao.” H. S.

JE MATATIZO YETU YANATATULIKA – JINSI GANI?

*Tunawezaje kuhuna na kuwa Wakristo
wenye furaha na imara?*

*Je Roho Mtakatifu anawezaje kuyajaza
maisha yetu?*

Yesu alisema:

“Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu.” (Yohana 15:4)

*“Kukaa ndani ya Kristo humaanidha upokeaji endelevu wa Roho wake,
maisha ya kujitoa kikamilifu kwa ajili ya huduma yake.”³⁷*

Suluhisho hili la kimbingu lenye sehemu mbili kwa tatizo letu kuu kwa wakati huo huo ni njia kuyaenda maisha ya furaha ya Kikristo. Kwa nini? Yesu alitoa maoni katika maneno haya: *“Hayo nimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe.”* (Yohana 15:11). Kupitia hatua hizi mbili (kuendelea kupokea Roho Mtakatifu na kujitoa kikamilifu) Kristo hukaa ndani yetu na ni njia ya kupata furaha kamili. Wakolosai 1:27 huzungumia utukufu wa utajiri:

³⁷ E. G. White, *The Desire of Ages* (1898), uk. 676.2

Kristo ndani yenu. Je si jambo la ajabu kwamba Yesu aliunganisha huu mfano wa mzabibu katika ahadi ya Roho Mtakatifu katika Yohana 14 na kazi ya Roho Mtakatifu katika Yohana 16?

Jambo la muhimu ni kwamba sisi (kama kanuni) tunajitoa kikamilifu kwa Mungu pamoja na jinsi tulivyo na kila kitu tulicho nacho na kwamba tunaomba pia kila siku na kupokea kwa imani kujazwa kwa Roho Mtakatifu.

KWA NINI NI LAZIMA TUJITOE KWA YESU KILA SIKU??

Yesu alisema katika Luka 9:23: “Akawaambia wote, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake **kila siku**, anifuate.”

Yesu alisema kwamba uanafunzi ni uuala la kila siku. Kujikana nafsi humaanisha kumpatia Yesu udhibiti wa maisha yangu. Kubeba msalaba haimaanishi kwamba tutakuwa na magumu kila siku. Maana yake: Kukana njia za kibinagsi kila siku na kujitoa kwa furaha na kwa hiari kwa Yesu – Kama Paulo alivyosema kuhusu yeye mwenyewe: “Ninakufa kila siku.” Mtu alipokuwa akibeba msalaba wakati wa Yesu, basi alikuwa amehukumiwa kifo na alikuwa akielekeaa sehemu ya kuuliwa. Hivyo inahusiana pia na kukubali shida, zinazotokana na kumfuata Yesu.

Tulipokea maisha yetu ya kimwili wakati wa kuzaliwa. Ili kuweza kuendelea na maisha yetu, nguvu na afya tunakula kila siku. Tulipokea maisha yetu ya kiroho tulipozaliwa upya. Ili tuweze kuyaweka maisha yetu ya kiroho kuwa yenye nguvu na yenye afya ni muhimu pia kuihudumia utu wa ndani **kila siku**, ikiwa hili halitafanyika katika maisha yetu ya kimwili na pia katika maisha yetu ya kiroho, basi tutakuwa dhaifu, wagonjwa na hata kufa. Hatuwezi kula chakula kabla na kukihifadhi wala kuweka hifadhi ya Roho Mtakatifu.

Katika kitabu cha *The Acts of Apostles* kuna ushauri wa thamani juu ya hili: “Kama ilivyo katika ulimwengu wa asili, vivyo hivyo katika ulimwengu wa kiroho. Maisha ya asili yanalindwa kila wakati kwa uweza wa kiungu; lakini bado hili halifanyiki kwa muujiza wa moja kwa koja, bali kuititia matumizi ya mibaraka iliyowekwa ndani ya uwezo wetu. Hivyo maisha ya kiroho yanaendelezwa kwa kutumia mali hizo ambazo Mpaji ametoa.”³⁸

³⁸ E. G. White, *The Acts of the Apostles*, (1911), uk. 284.2

Maoni haya katika kitabu cha *The Desire of Ages* yalinivutia sana: "Tunapaswa kumfuuta Yesu siku kwa siku. Mungu hatoi msaada kwa ajili ya kesho."³⁹

Ellen White alisema:

"Kumfuata Yesu huhitaji badiliko la moyo wote mwanzoni, na kujirudia rudia kwa badiliko hili **kila siku**...."⁴⁰ "Hata hivyo kujiweka kwetu wakfu hata kama kulikuwa ni kwa ukamilifu kiasi gani wakati wa kuongoka, hakutatusaidia kitu chochote mpaka kutakopofanyika **kila siku** ... "⁴¹ "Jiweke wakfu kwa Mungu asubuhi; fanya hii kuwa kazi yako ya kwanza. Ombi lako liwe "Nichukue, Ee Bwana, niwe wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni pako. Nitumie leo katika huduma yako. Kaa nami, na kazi yangu yote itimizwe ndani yako." Hili ni suala la kila siku. Kila siku asubuhi jitakase kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Kabidhi mipango yako yote kwake, ili kuitekeleza au kuachana nayo kulingana na ufunuo wa mapenzi yake. Hivyo siku kwa siku useme unaweka maisha yako mikononi mwa Mungu, na hivyo maisha yako yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo."⁴²

Morris Venden alisema:

"Ikiwa hujagundua ulazima wa badiliko la kila siku, huu unaweza kuwa ni ugunduzi mkubwa maishani mwako. *Thoughts From The Mount of Blessing*, uk 101, hutoa ahadi hii: 'Ikiwa utamtafuta Bwana na kubadilishwa kila siku... manung'uniko yako yote yataondoka, shida zako zota zitaondolewa, matatizo yote yenye kukanganya yanayokusumba sasa yatatatuliwa.'"⁴³

Kubakia ndani ya Yesu kwa kufanya upya kujitoa kwetu kila siku ni muhimu kama ilivyokuwa wakati tulipomwendea hapo awali.

idi kwamba: "Uhusiano wa kuwa na Mungu kila siku huongoza katika kujitoa daima, kumtegemea Yeye kila wakati."⁴⁴

Tunaweza kuwa na uhakika kwamba: tunapojitoa kwa hiari yetu wenyewe kwa Yesu kila siku asubuhi, basi tunafanya kile anachotutarajia sisi tufanye, kwa sababu alisema: "*Njooni kwangu...*" (Mathayo 11:28 NKJV) na: "... *wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.*" (Yohana 6:37 NKJV)

³⁹ E. G. White, *The Desire of Ages* (1898), uk. 313.4

⁴⁰ Editor Francis D. Nichol, *Adventist Bible Commentary Vol. 1* (Review and Herald, 1976), uk. 1113

⁴¹ E. G. White, *Review and Herald*, Jan. 6, 1885

⁴² E. G. White, *Steps to Christ* (1892), uk. 70.1

⁴³ Morris Venden, *95 Theses on Righteousness by Faith* (Pacific Press, 1987), uk. 96

⁴⁴ Morris Venden, *95 Theses on Righteousness by Faith* (Pacific Press, 1987), uk. 233

“Bwana yuko tayari kufanya mambo makubwa kwa ajili yetu. Hatuwezi kupata ushindi kupitia hesabu, bali kwa kusalimisha kikamilifu nafsi kwa Yesu. Tunapaswa kusonga mbele kwa nguvu yake, tukimtumaini Mungu mwenye nguvu wa Israeli ...”⁴⁵

Mvuto mkubwa ambao Mungu anaweza kuufanya kupitia kwetu tunapojoitoa kwake kikamilifu umeelezwa na John Wesley kama ifuatavyo: “Mungu anaweza kufanya mambo makubwa kupitia mtu mmoja, ambaye amejitoa kwa Mungu asilimia 100, kuliko anavyoweza kwa jeshi la watu wote, waliojitoa asilimia 99 kwa Mungu.”⁴⁶

Ellen White aliandika:

“Ni wale tu ambao watakuwa watendakazi pamoja na Kristo, ni wale tu ambao watasema, Bwana, yote niliyo nayo na vyote nilivyo ni vyako, watakaotambulika kama wana na binti za Mungu.”⁴⁷ “Wote watakajitakasa nafsi, mwili, roho kwa Mungu wataendelea kupokea nguvu mpya ya kimwili na kiakili... Roho Mtakatifu hutoa uweza wake wa kiwango cha juu kutenda kazi moyoni na akilini. Neema ya Mungu hukuza na kuongeza uwezo wao wa kiakili, na kila ukamilifu wa asili ya uungu huja kama msaada wao katika kazi ya kuokoa roho...Na katika udhaifu wao wa kibinadamu wanawezeshwa kutenda matendo ya “Mwenyezi Mungu.”⁴⁸

Kuna mengi sana kuhusu mada ya “utakaso” au “kujitoa” au “kutoa maisha yako” au “kubadilika”.

Kwa nini mtu anapaswa kuomba ubatizo wa Roho Mtakatifu kila siku?

Ombi la kujazwa na Roho Mtakatifu ni ombi kwa Yesu kukaa na mimi. Kwa sababu anaishi ndani yangu kupitia Roho Mtakatifu. Lakini kwa nini kila siku?

E.G. White alisema katika kitabu cha *The Acts of the Apostles*: “Kwa mtendakazi aliyejitakasa kuna faraja ya ajabu kufahamu kwamba hata Kristo wakati wa maisha yake duniani alimtafuta Baba yake **kila siku kwa ajili ya kupatiwa mahitaji ya neema inayohitajika...** Mfano wake mwenyewe ni uhakika kwamba maombi

⁴⁵ E.G.White, *Sons and Daughters of God*, uk. 279

⁴⁶ Dr. S.Joseph Kidder, Anleitung zum geistlichen Leben (Andrews University), PPP slide 14

⁴⁷ E.G.White, *The Desire of Ages* (1898), uk. 523.1

⁴⁸ E.G.White, *The Desire of Ages* (1898), uk. 827.3

ya dhati, ya ustahimilivu kwa Mungu kwa imani-imani ambayo huongoza kumtegemea Mungu kabisa, na kujitakasa kwa usahihi katika kazi yake-itasaidia kuwapatia watu msaada wa Roho Mtakatifu katika vita dhidi ya dhambi.”⁴⁹

Kama hili lilikuwa hitaji la Yesu la kila siku, basi ni muhimu kiasi gani kwetu.

Katika 2 Wakorintho 4:16 NKJV kuna maelezo ya muhimu:

“...lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku.”

Utu wetu wa ndani unahitaji matunzo ya kila siku. Huku kufanywa upya kila siku hutokeaje? Kulingana na Waefeso 3:16-17,¹⁹ NKJV hutokea kupitia Roho Mtakatifu: “Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo akae miyonini mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo ... mpare kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.”

Matokeo yake:

- ▶ Kama kanuni ni muhimu kuomba kila siku kwa ajili ya kufanywa upya kwa Roho Mtakatifu.
- ▶ Matokeo yake Kristo huishi ndani yetu.
- ▶ Hutupatia uwezo kulingana na utajiri wa utukufu wake kwa ajili ya utu wetu wa ndani. Uwezo wa Mungu ni uwezo upitao akili [usio wa ulimwengu huu].
- ▶ Hivyo upendo wa Mungu huwekwa ndani ya mioyo yetu.
- ▶ Na ni njia ya maisha ya “utimilifu wote wa Mungu.” (Angalia Yohana 10:10; Wakolosai 2:10)

Fungu lingine la muhimu linapatikana katika Waefeso 5:18 NKJV: “.... bali mjazwe Roho.” Zingatia kwamba hili ni zaidi ya ushauri. Ni amri ya kiungu. Mungu wetu anatarajia tuwe na shauku ya kuishi na Roho Mtakatifu. Wataalam wa Kiyunani walisema kwamba fungu hili hueleza kwa uwazi zaidi – na ninamnukuu Johannes Mager: “Hebu kila wakati mzidi kujazwa upya na Roho Mtakatifu.”⁵⁰

Muongozo wetu wa kujifunza Biblia unasema: “Ubatizo wa Roho Mtakatifu humaanisha kuwa chini kabisa ya ushawishi wa Roho Mtakatifu – ‘kujazwa’ kabisa na yeze [Roho Mtakatifu]. Huu si uzoefu unaotokea mara moja, bali kitu ambacho kinapaswa kuwa cha kuendelea kujirudia, kama Paulo alivyoelezea katika Waefeso 5:18 kwa kutumia kitenzi cha Kiyunani ‘kujazwa’.”⁵¹

⁴⁹ E. G. White, *Acts of the Apostles*, (1911), uk. 56.1

⁵⁰ Editor Werner E. Lange, *Unser größtes Bedürfnis* (Lüneburg, 2011), uk. 42

⁵¹ Sabbath School Study Guide July 17, 2014

Mtume Paulo anaandika hili katika Waefeso sura ya 5, japokuwa aliandika yafuatayo katika sura ya 1:13: "...Nanyi pia katika huyo mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu." Waefeso hakika walikuwa tayari wamempokea Roho Mtakatifu. Hata hivyo, ilikuwa ni muhimu kwao "kufanywa imara kwa nguvu kuititia Roho wake" na "kujazwa na Roho" na "na kufanywa wapya katika roho ya nia zenu". Katika Sura ya 4:30 anatuonya tusimhuzunishe wala kumtukana Roho Mtakatifu.

Ellen White alisema:

"Kwa ajili ya ubatizo wa **kila siku** wa Roho kila mtendakazi anapaswa kupeleka ombi lake kwa Mungu."⁵²

"Ili tuweze kuwa na haki ya Kristo, tunahitaji kubadiliswa kila siku na mvuto wa Roho, kuwa washirika wa tabia ya uungu. Ni kazi ya Roho Mtakatifu kukuza hamu, kutakasa moyo, kumuadilisha mtu katika hali yake yote".⁵³

Bwana alizungumza mahali fulani kuititia kwake. "Wale wote waliovutwa na Maandiko Matakatifu kama sauti ya Mungu, na wanatamani kufuata mafundisho yake, wanapaswa kujifunza **kila siku**, kupokea uwezo na **nguvu za kiroho kila siku**, ambao umetolewa kwa kila muumini wa kweli katika kipawa cha Roho Mtakatifu."⁵⁴

Zaidi ya hayo alisema: "Tunapaswa kumfuata Kristo siku kwa siku. Mungu hatoi msaada kwa ajili ya kesho."⁵⁵

Na mahali pengine "Mawasiliano na mawakala wa kiungu kila wakati ni muhimu kwa maendeleo yetu. Tunaweza kuwa tumepata kipimo cha Roho wa Mungu, lakini kwa maombi na imani tunaendelea **kumtafuta zaidi Roho**".⁵⁶

Pia nimepata nukuu hizi za kupendeza: "**Unahitaji ubatizo wa upendo wa kila siku** ambao katika siu za mitume uliwafanya wote kunia mamoho."⁵⁷

Warumi 5:5 hutuonyesha kwamba upendo wa Mungu unajazwa miyoni mwetu na Roho Mtakatifu. Tunapata jambo kama hilo katika Waefeso 3:17. Ubatizo wa kila siku pamoja na Roho Mtakatifu (kujazwa na Roho Mtakatifu) husababisha kutokea kwa wakati mmoja ubatizo wa kila siku wa upendo (kujazwa na Upendo wa Mungu wa Agape). Kwa kuongezea inasema katika Wagalatia 5:16 kwamba matokeo yake nguvu ya dhambi huvunjwa.

⁵² E.G. White, *The Acts of the Apostles* (1911), uk. 50.2

⁵³ E.G. White, *Selected Messages 1*, (1958), uk. 374.1

⁵⁴ E.G. White, *The Signs of the Times March 8, 1910*, par. 1

⁵⁵ E.G. White, *The Desire of Ages* (1898), uk. 313.4

⁵⁶ E.G. White, *The Review and Herald*, March 2, 1897, par. 5

⁵⁷ E.G. White, *Testimonies to the Church* (1904), vol. 8, uk. 191

“ Ili tuweze kuwa na haki ya Kristo tunapaswa kubadilishwa kila siku kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, ili kuwa washiriki wa tabia ya uungu.

UMUHIMU WA IBADA BINAFSI

Ibada binafsi ina umuhimu gani, ikiwa ni muhimu kiasi hicho kwamba kila siku ninajitoa kwa Yesu na kuomba kujazwa na Roho Mtakatifu?

Ibada ya kila siku na utunzaji wa Sabato ni msingi wa maisha ya kiroho.

Tayari tumesoma mafungu ya Biblia na nukuu mbalimbali. Zinatuonyesha kwamba utu wa ndani hufanywa upya siku kwa siku. **Hili hutoa mwanga wa kutosha kuhusu umuhimu wa ibada zetu binafsi za kila siku.**

Msingi mzima wa huduma ya ibada katika hema ya kukutania ulikuwa ni sadaka ya kuteketezwa ya asubuhi na jioni. Siku ya Sabato kulikuwepo na sadaka ya kuteketezwa ya ziada ya siku ya Sabato (Hesabu 28:4,10). Sadaka ya kuteketezwa ilikuwa na umuhimu gani?

“Sadaka ya kuteketezwa iliwakilisha kujitoa kikamilifu kwa mdhambi kwa Bwana. Hapa watu hawakuficha kitu chochote, bali kila kitu kilikuwa cha Mungu.”⁵⁸

“Masaa yaliyokuwa yamewekwa kwa ajili ya kafara ya asubuhi na jioni yalichukuliwa kuwa matakatifu, na yaliuja kutunzwa kama muda maalumu wa ibada katika taifa lote la Kiyahudi.... Katika desturi hii Wakristo wana mfano wa maombi ya asubuhi na jioni. Wakati Mungu huchukia mzunguko wa sikukuu za kawaida, bila roho ya ibada, anaangalia kwa furaha kubwa wale wanaompenda, wakisijudu asubuhi na jioni kutafuta msamaha wa dhambi zilizotendwa kupeleka maombi yao kwa mibaraka inayohitajika.”⁵⁹

Je unatambua kwamba ibada ya kila siku inahusiana na Sabato kama msingi kwa ajili ya maisha yetu ya kiroho? Kwa kuongezea, je inaweza wazi kwamba inahusiana na kujitoa kwa Yesu Kristo kila siku, ambaye anaalikwa kupitia Roho Mtakatifu kuishi ndani yetu?

Je umeifanya kanuni muhimu zaidi ya kiroho kuwa yako: T Kumpa Mungu kipaumbele juu ya kila kitu kila siku?

⁵⁸ Fritz Rienecker, *Lexikon zur Bibel* (Wuppertal, 1964), uk. 1017

⁵⁹ E. G. White, *Patriarchs and Prophets* (1890) uk. 353-3

Yesu alisema katika Hubiri Mlimani:

“Bali utafutaeni kwanza ufalme wa mbinguni na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa.” Mathayo 6:33 NKJV

Ufalme wa Mungu ni pale ambapo unaye Kristo moyoni mwako sasa. Hii ndio sababu ni kwa nini tunahitaji kila siku kujitoa na kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu wakati tunapofanya ibada. Wakati wa kufanya maamuzi utakuwa pindi tutakopokuwa tumesimama mbele za Mungu: Je tulikuwa na uhusiano binafsi uokoao na Kristo na je tulikaa ndani yake? (Tazama Yohana 15:1-17) Je huhitaji zaidi – kwa ajili ya utimilizwaji mkuu wa imani yako?

Wale wote wanaotumia muda kidogo au kukosa muda wa utulivu pamoja na Mungu au kukosa muda wa kutosha wa ibada huenda watatiwa nguvu kwa ibada yao mara moja au mara mbili kwa wiki. Hiyo ni sawa na mtu ambaye hula mara moja tu kwa wiki. Kufanya ulinganifu: Je lisingekuwa jambo la kipuuzi kutaka kula mara moja tu kwa wiki? Je hili halimaanishi kwamba Mkristo bila ibada ni mtu wa kimwili?

Hili pia humaanisha kwamba kama akikaa katika hali hii basi hataokolewa. Tunapokuwa Wakristo wa tabia ya mwilini ibada inaweza kuwa kama kutimiza wajibu. Tunapokuwa watu wa kiroho basi ibada huwa kitu cha muhimu zaidi kila siku.

Miaka kadhaa iliyopita nilisoma kitabu kilichoandikwa na Jim Vaus: *Nilikuwa Gangista*. Alikuwa mhalifu, aliyebadilika. Alikiri dhambi zake kwa moyo wake wote – kwa mfano kusema uwongo, wizi, n.k. aliuona uingiliaji kati wa Mungu wa hali ya juu. Hili lilynigusa. Nilisema moyoni mwangu: ninafanya vizuri karibu katika kila kitu, lakini sina uzoefu kama huo. Kisha nikamuomba Bwana: “Baba wa mbinguni, mimi pia ninataka kukiri dhambi zote zinazojulikana na dhambi zangu zote utakazonionyesha. Zaidi ya hayo, nitaamka saa moja kabla kuomba na kusoma Biblia. Kisha ninataka kuona kama pia utaingilia kati maisha yangu.”

Mungu asifiwe aliingilia kati maisha yangu. Tangia hapo, hasa ibada yangu ya asubuhi kuhusiana na Sabato, imekuwa kiini cha maisha yangu pamoja na Mungu.

Kupitia kujitoa kila siku na kupitia kujazwa kila siku Roho Mtakatifu maisha yetu yatabadilishwa kuwa ya manufaa. Hili hutokea wakati wa ibada yetu binafsi.

KUABUDU KATIKA ROHO NA KWELI

Hebu tutafakari dhumuni la ibada. Katika ujumbe wa Mungu wa mwisho kwa wanadamu inahusiana na kumwabudu muumbaji dhidi ya kumwabudu mnyama. (Ufu. 14:6-12) Ishara ya nje ya ibada ni Sabato (kumwabudu muumbaji). Hali ya ndani ya ibada ni Sabato (kumwabudu muumbaji) hali ya ndani ya kuabudu imeonyeshwa katika Yohana 4:23-24: “*Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli.* Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu.”

Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli! Waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli; kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.”

Kuabudu katika roho kwa hakika humaanisha kuabudu kufahamu moyoni, lakini pia kujazwa na Roho Mtakatifu. Kuabudu katika kweli humaanisha kuishi kwa kujitao kikamilifu kwa Yesu, yeye ambaye ni kweli katika nafsi, Yesu alisema: “*Mimi ni kweli.*” (Yohana 14:6) Na humaanisha kupitia kwa Yesu kukaa ndani yetu ili kuishi kulingana na neno la Mungu na maagizo yake, kwa sababu alisema: “*Neno lako ni kweli.*” (Yohana 17:17) na Zaburi 119:142 inasema: “*Sheria yako ni kweli.*” Ikiwa hatuna ibada ya kweli sasa, je hatuko kwenye hatari ya kuanguka wakati wa changamoto kubwa? Hili litakuwa ni tatizo kubwa kwa Wakristo wote wa kimwili.

Ninadhani sote tunataka kupiga hatua kwa msaada wa Mungu na kuongezeka katika maarifa. Inaweza kuwa imani potofu kilikuwa kikwazo kwa baadhi ya watu kusonga mbele.

UBATIZO NA ROHO MTAKATIFU

Baadhi ya watu wanafikiri kwamba wamejazwa na Roho Mtakatifu kwa sababu wamebatizwa na hivyo kila kitu kiko sawa ma hawahitaji kufanya kitu chochote zaidi. D. L. Moody ameetoa maelezo juu ya hili: “Wengi wanafikiri kwamba kwa sababu wakati fulani walijazwa basi wamejazwa milele. Oh rafiki yangu, sisi ni vyombo viharibikavyo; ni muhimu kwetu kuendelea kubakia kwenye kijito cha maji ili tuweze kujazwa.”⁶⁰

⁶⁰ D. L. Moody, *They Found the Secret*, uk. 85, 86; quoted in “*10 Days – Prayers and Devotions ...*” by Dennis Smith, uk. 23

Joseph H. Waggoner alisema:

“**Katika nyakati zote, ubatizo unapoonekana kama kithibitisho kwa ajili ya karama ya Roho Mtakatifu, mdhambi aliyetubu hudanganywa kwenye ulinzi wa tabia ya mwilini.** Huamini kabisa kwenye ubatizo wake kama ishara ya neema ya Mungu. Ubatizo na **si Roho moyoni** mwake utakuwa ishara yake au ‘ushuhuda’ ...”⁶¹

Ubatizo kwa hakika ni uamuzi muhimu; na huendana na mapenzi ya Mungu. Una na utaendelea kuwa na umuhimu mkubwa. Lakini hatupaswi kuangalia nyuma kwenye tukio la wakati uliopita kama kithibitisho kwamba tumejazwa na Roho Mtakattifu. Badala yake tunapaswa kutambua **sasa** na kuwa na uzoefu **sasa** kwamba tumejazwa na Roho Mtakatifu.

Baadhi ya watu walipokea Roho Mtakatifu **kabla** hawajabatizwa – kwa mfano Kornelio na nyumba yake au Sauli. Wengine walipokea Roho Mtakatifu **baada** ya kubatizwa – kwa mfano Wasamaria au wale watu 12 wa Efeso. Lakini yote ni sawa ikiwa mtu atapokea Roho Mtakatifu **kabla, wakati au baada** ya ubatizo: cha muhimu ni kwamba tulimpokea Roho Mtakatifu wakati fulani na kwamba bado tunaye ndani ya mioyo yetu **sasa**. Kilichotokea wakati uliopita si muhimu sana bali hali ikoje sasa – leo.

Ninataka kukukumbusha tena: Tulipokea maisha yetu ya kimwili wakati wa kuzaliwa. Maisha yetu hudumishwa kila siku kwa chakula, maji, mazoezi kulala, n.k. vinginevyo tusingeishi muda mrefu. Kanuni hiyo hiyo pia hutumika katika maisha yetu ya kiroho kama iliyyo kwa maisha yetu ya kimwili. Tulipokea maisha mapya kupitia Roho Mtakatifu, wakati tulipojisalimisha kabisa kwa Kristo. Maisha yetu ya kiroho yanaendelezwa kupitia Roho Mtakatifu, maombi, neno la Mungu, n.k. E. G. White alisema: “Maisha ya asili hulindwa siku kwa siku kwa nguvu ya kimbingu; lakini bado hayaendelezwi kwa muujiza wa moja kwa moja, bali kupitia matumizi ya mibaraka iliyowekwa ndani ya uwezo wetu. Hivyo maisha ya kiroho huendelezwa kwa matumizi ya vitu ambavyo Mpaji amevitoa.”

⁶²

Si maisha ya kimwili wala ya kiroho huendelea yenye ndani yetu. Ni muhimu kutumia vitu ambavyo Mungu ametupatia.

Hili humaanisha: Tunapozaliwa upya Roho Mtakatifu hutolewa kwetu akae kwetu. Lakini ili kwamba yeye aweze kukaa inategemea matumizi ya kila siku ya njia, ambazo Bwana ametupatia. Tunaweza kutarajia matokeo gani ikiwa hatutumii “njia” hizo?

⁶¹ Joseph H. Waggoner, *The Spirit of God* (Battle Creek, Michigan 1877), uk. 35f, quoted in Garrie F. Williams, *Erfüllt vom Heiligen Geist* (Lüneburg, 2007), S. 58

⁶² E.G.White, *The Acts of the Apostles* (1911), uk. 284.2

Roho Mtakatifu ndiye wa muhimu kupita “njia” zote hizi. Na zaidi, maombi ni muhimu sana, kuunganishwa na Mungu kuititia neno lake, kushiriki katika ibada na mambo mengine.

Ninadhani tunaweza kukubaliana kwamba kama kanuni ni muhimu pia kuutunza utu wa ndani *kila siku*. Ikiwa hatutafanya hivyo, basi tutapata matokeo ya kuhuzunisha. Hatuwezi kutangulia kula wala kuweka akiba ya Roho Mtakatifu. “Mungu hatoi msaada kwa ajili ya kesho.”⁶³ INadhani iko wazi kabisa kwamba kujisalimisha kila siku kwa Yesu ni muhimu na kwamba tunapaswa kumwalika Roho Mtakatifu kila siku maishani mwetu.

Mambo haya yote mawili huelezea jambo lile lile – ni pande mbili za sarafu moja; kuwa na uhusiano wa karibu pamoja na Kristo. Ninajitoa kwake kuititia kujisalimisha na kwa kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu ninamkaribisha ndani ya moyo mwangu. Kati ya mafungu mengine ya Biblia 1 Yohana 3:24 (angalia pia Yohana 14:17,23) hutuonyesha kwamba Yesu huishi ndani yetu kuititia Roho Mtakatifu: “*Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.*”

MATOKEO YA ROHO MTAKATIFU

Wakati Roho Mtakatifu anapokuwa ndani yangu, hutimiza ndani yangu kile ambacho Kristo alikitimiza. Warumi 8:2 inasema: “*Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti.*” Tunawenza kuiezea“sheria ya Roho” kama namna ambayo Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani ya moyo uliojisalimisha kikamilifu kwa Mungu. Ni Roho Mtakatifu pekee anayeweza kuweka uzima ndani yangu kwa kile Kristo alichofanya. E. G. White huelezea vyema: *Roho alipaswa kutolewa kama wakala wakuzaliwa upya, a pasipo hili kafara ya Kristo ingekuwa haina maana...* Ni Roho ambaye huwezesha iwezekane kile kilichotolewa na Mkombozi wa ulimwengu. Ni Roho ambaye moyo hufanywa kuwa safi. Kuititia Roho muumini huwa mshiriki wa tabia ya uungu... Uweza wa Mungu hungojea uhitaji wao na ukubali wao.”⁶⁴

Thomas A. Davis huelezea mchakato huu kama ifuatavyo: “Hili humaanisha kwamba hata ufanisi wa kazi ya Kristo kwa ajiliwatu unategemea Roho Mtakatifu. Pasipo Yeye [Roho Mtakatifu] kila kitu Yesu alichokifanya hapa duniani – pale Gethemane, juu msalabani, ufufuo wake na huduma yake ya kikuhanu huko

⁶³ E. G. White, *The Desire of Ages*, (1898), uk.313.4

⁶⁴ E. G. White, *The Desire of Ages*, (1898) uk. 671.2 and 672.1

mbinguni-visingefanikiwa. Matokeo ya kazi ya Kristo yasigekuwa ya muhimu zaidi kuliko yale ya viongozi wakuu wa kidini au wa kimaadili. Lakini ijapokuwa Kristo alikuwa zaidi ya hawa, asingeweza kumwokoa mwanadamu kuitia mfano [wa maisha yake] na mafundisho yake pekee. Ili kuwabadilisha watu ilikuwa ni muhimu kufanya kazi ndani yao. Kazi hii hufanywa na Roho Mtakatifu, ambaye alitumwa kufanya hili ndani ya miyo ya watu, jambo ambalo Yesu alifanya liwezekane.”⁶⁵

Je hii peke yake si sababu ya kutosha kuona kwamba umejazwa na Roho Mtakatifu?

“Wakati Roho wa Mungu anapotawala miyoni mwetu, hubadilisha maisha. Mawazo ya dhambi huondolewa, matendo mabaya huachwa; upendo, uvumilivu, na amani huchukua nafasi ya hasira, kijicho, na migogoro. Furaha huchukua nafasi ya huzuni, na uso huakisi nuru ya mbinguni.”⁶⁶

Yako matokeo mengine ya thamani kutokana na maisha ya Roho Mtakatifu, lakini pia kuna mapungufu makubwa na hasara pasipo yeye. Tofauti kati ya maisha pamoja na pasipo Roho Mtakatifu yataelezewa zaidi katika sura ya 4

JE NIMEJAZWA NA ROHO MTAKATIFU?

Tafadhalii jiulize mwenyewe maswali yafuatayo kuhusu kujazwa na Roho Mtakatifu:⁶⁷

- ▶ Je kuna matokeo ya wazi ya Roho Mtakatifu maishani mwangu? Kwa mfano, je amemfanya Yesu kuwa halisi na mkuu kwako? (Yohana 15:16)
- ▶ Je ninaanza kuisikia na kuilewa sauti ya ndani ya Roho Mtakatifu? Je anaweza kuniongoza katika maamuzi makubwa na madogo maishani mwangu? (Warumi 8:14)
- ▶ Je aina mpya ya upendo kwa wanadamu wenzangu imeamshwa ndani yangu? Je Roho Mtakatifu ananipatia moyo wa huruma na wa kujali sana kwa ajili ya watu, ambao kwa kawaida nisingewachagua kama marafiki zangu? (Wagalatia 5:22; Yakobo 2:8,9)
- ▶ Je ninapitia uzoefu wa mara kwa mara jinsi Roho Mtakatifu anavyonisaidia kushughulika na wanadamu wenzangu? Je ananipatia maneno sahihi kuifikia moyo wa mtu, ambaye ana mashaka na masumbufu?
- ▶ Je Roho Mtakatifu hunipatia nguvu kuwaambia wengine habari za Yesu na kuwaongoza kwake?

⁶⁵ Thomas A. Davis, *Als Christ siegreich leben*, (HW-Verlag), Seite 43 / How to be a victorious Christian, R&H.

⁶⁶ E.G. White, *The Desire of Ages*, (1898), uk. 173,1

⁶⁷ Catherine Marshall, *Der Helfer* (Erzhausen, 2002), uk. 24

- ▶ Je ninapitia uzoefu wa namna anavyonisaidia katika maisha yangu ya maombi na kunisaidia kueleza hisia zangu za ndani ya moyo kwa Mungu?

Tunapoya fikiria maswali haya, tunaona ni hitaji kubwa kiasi gani tulilo nalo kukua katika Roho Mtakatifu, kuweza kumjua sana Yeye na kumpenda Yeye zaidi.

Ndugu mmoja aliandika: Baba yangu na mimi tume patana. Baada ya kujifunza kitabu cha *Step to Personal Revival* na vitabu vya *40 Days* cha kwanzza na cha pili, nimepata uzoefu wa kushangaza jinsi Roho Mtakatifu anavyotenda kazi na anavyotaka kutenda kazi katika kila eneo la maisha yangu.

MAPATANO KATI YA BABA NA MWANA

Uhusiano wangu pamoja na baba kwa namna fulani ulikuwa mgumu. Matarajio yangu na maombi yangu wakati wa utoto na ujana wakati wote yalikuwa kwamba niwe na mahusiano mazuri na baba yangu. Lakini yaliendelea kuwa mabaya. Miaka mingine sita mpaka saba ilipita. Mungu aliweka upweke mkubwa moyoni mwangu. Wakati nikijifunza na kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu mke wangu pamoja na mimi tulipata uzoefu mkubwa pamoja na Mungu. Tuliomba kwa ajili ya familia yetu na hasa kwa ajili ya baba yangu. Katika kipindi hiki nilipokea nguvu mpya ya kumpenda baba yangu. Niliweza kumsamehe kwa kila kitu ambacho hakukifanya vyema katika mahusiano yetu tangu utoto wangu. Baba yangu pamoja na mimi sasa ni marafiki. Pia ameanza kuwa mtu wa kiroho zaidi na pia ameanza kuwaambia watu wengine kuhusu Mungu. Sasa, miaka miwili baadaye, mahusiano na baba yangu bado ni mazuri sana. Ninamshukuru Mungu kwa uzoefu huu. Nilikuwa nikihisi kukosa nguvu na mara nydingi mpweke. Lakini tangu nimeanza kuomba kila siku kwa ajili ya Roho Mtakatifu, ninaona aina mpya na nzuri ya maisha na uhusiano pamoja na Mungu. (Jina linafahamika na mhariri).

Ombi: Bwana Yesu, ninakushukuru kwamba unataka ubaki ndani yangu kupidia Roho Mtakatifu. Asante kwamba kwa kujisalimisha kila siku imani yetu na upendo unazidi kukua. Bwana, nisaide nipate kumfahamu Roho Mtakatifu na kazi yake vyema. Ninatamani kujuua kile anachotaka kufanya kwa ajili yangu, familia yangu pamoja na kanisa langu na jinsi tunavyoweza kuwa na uhakika kwamba tunaweza kupokea Roho Mtakatifu tunapoomba kila siku. Asante kwa hili. Amen

MAELEZO YA ZIADA KWA WAEFESO 5:18 – “KUJAZWA ROHO!”

Tayari tunaweza kuona katika fungu la Kiingereza katika Waeleso 5:18 kwamba ombi hili limefanywa kuwa amri. Zaidi ya hilo, tunaweza kuona kwamba amri hii imeelekezwa kwa kila mtu. Na unaweza kuona pia kwamba ni wajibu wetu kutafuta ukamilifu wa Roho Mtakatifu. Lakini fungu la awali la Kiyunani hulifanya liwe wazi zaidi.

Johannes Mager anatoa maoni katika hili: “Katika barua za agano lakale kuna aya moja tu, ambayo huzungumzia moja kwa moja kuhusu kujazwa na Roho Mtakatifu: ‘Mjazwe na Roho.’(Waeleso 5:18) Katika kitabu cha Matendo tunakuta kujazwa na Roho Mtakatifu ni karama, ambayo hutumika kutenda kazi kwa nguvu katika hali maalum. Hata hivyo, Paulo huelezea kujazwa na Roho Mtakatifu kama amri, ambayo inajitegemea kutoka katika hali ya maisha na hutumika kwa wafuasi wote wa Yesu. Hii amri fupi, lakini muhimu ina vipengele muhimu vinne.

1. Kitendezi ‘jaza’ (*plerein*) hutumika katika hali ya umuhimu. Paulo hatoi mapendekezo hapa au hatoi ushauri wa kirafiki. Hatoi pekendekezo, kwamba mtu anaweza kukubali au kukataa. Anaamuru kama mtume mwenye mamlaka. Amri mara zote hutaka utayari wa mtu. Kama Mkristo atajazwa na Roho Mtakatifu, basi inategemea kwa kiasi kikubwa [utayari wake] mwenyewe. **Wakristo wako chini ya amri ya kufanya bidii kujazwa na Roho Mtakatifu.** Huu ni wajibu wetu kama watu wanaopaswa kujazwa na Roho Mtakatifu.
2. Kitendezi kinatumika katika wingi. Amri haielekezwi kwa mtu mmoja ndani ya kanisa, wale ambao wana kazi maalum. Kujazwa na Roho Mtakatifu si upendeleo kwa watu wachache waliopendelewa. **Wito unatumika kwa kila**

mtu aliyeko ndani ya kanisa – wakati wote na kila mahali. Hakuna ubaguzi.

Kwa Paulo ilikuwa ni kawaida kwamba Wakristo wanapaswa kujazwa na Roho Mtakatifu.

3. Kitenzi kiko katika wakati unaoendelea. Hakisemi: 'Jijaze na Roho!', bali 'Mjazwe na Roho!'. Hakuna mtu anayeweza kujijaza mwenyewe na Roho Mtakatifu. Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu pekee. Hapa ndipo ulipo utawala wake. Lakini **mtu anapaswa kuandaa mazingira ili Roho Mtakatifu aweze kumjaza. Pasipo utayari wake Roho Mtakatifu hawezি kufanya kazi ndani yake.**
4. Kwa Kiyunani mkazo uko wakati uliopo. Mkazo huu wa wakati uliopo huelezea tukio ambalo linaendelea kujirudia tofauti na mkazo wa wakati uliopita, ambao unaelezea tendo linalotokea mara moja. Kulingana na hili, kujazwa na Roho Mtakatifu si uzoefu unaotokea mara moja, bali ni tendo linalojirudia na linaloendela. **Mkristo si kama chombo ambacho hujazwa mara moja kwa ajili ya wakati wote, bali anapaswa kuendelea 'kujazwa'.** Sentensi inaweza kuelezw na namna hii: 'Mjazwe upya daima na mara kwa mara na Roho!'

Kujazwa na Roho Mtakatifu, ambaye alitolewa kwetu wakati wa ubatizo [uwe ni ubatizo ndani ya maji na Roho pamoja kujitoa kikamilifu] **kunaweza kupotea ikiwa ukailifu ambao ultolewa kwetu hautatunzwa**. Kama ukipotea, unaweza kupatikana tena. Kujazwa na Roho Mtakatifu ni lazima liwe tendo linalojirudia ili kwamba Roho Mtakatifu aweze kuchukua nafasi yote ya maisha yetu na maisha yetu ya kiroho kukosa nguvu. Kujazwa na Roho hakumaanishai kwamba tunakuwa naye kwa kiasi kikubwa, bali ni kwamba Roho anakuwa na sisi zaidi na zadi. **Ndio sababu Paulo aliwaamuru waumini wote kuendelea kujazwa na Roho.** Hii ni hali ya kawaida kwa Wakristo. Ubatizo mmoja lakini, lakini kujazwa mara 'nyingi.'⁶⁸

Bwana mwenyewe ametoa amri:
Mjazwe upya daima na mara kwa
mara na Roho!⁶⁹

⁶⁸ Johannes Mager alikuwa mchungaji, mwinjilisti na kwa miaka mingi akifundisha katika chuo kikuu juu ya theolojia ya utaratibu. Hivi karibuni, alikuwa kiongozi katika idara ya huduma za kichungaji katika Division ya Ulaya na Africa, huko Bern, Switzerland (sasa inajulikana kama Division ya Ulaya na Kat). Kwa sasa amestaafu na anaishi Friedensau. Nukuu inatoka kwenye kitabu chake. Auf den Spuren des Geistes, (Lüneburg, 1999) page 100-101 (kwa ruhusa kutoka kwenye ofisi ya uchapaji)

* E. G. White, Mount of Blessing, MB 20.3 (egwwritings.org)

** Johannes Mager, Auf den Spuren des Heiligen Geistes (Lüneburg, 1999), Seite 101

TOFAUTI GANI TUNAYOWEZA KUTARAJIA?

*Tuna faida gani tukiwa na maisha yaliyojazwa na
Roho Mtakatifu?*

*Tunakosa kitu gani tusipoomba kwa ajili ya Roho
Mtakatifu?*

ULINGANIFU KATI YA UKRISTO WA KIMWILI NA KIROHO

Madhara ya Ukristo wa tabia ya mwilini kwa mtu mmoja mmoja tayari yameelezewa kwa kiasi fulani. Baadhi ya madhara yanajieleza yenyewe kama ifuatavyo:

- ▶ Mtu huyu haokolewi katika hali hii. (Warumi.8:6-8; Ufu. 3:16)
- ▶ Upendo wa Mungu—upendo wa agape—haumo ndani ya mtu huyu (Warumi. 5:5; Wagalatia 5:22); Hutumainia tu upendo wao wa kibinadamu; Tamaa ya mwili haijavunjwa. (Wagalatia 5:16)
- ▶ Mtu huyu hajatiwa nguvu kupitia uweza wa Roho Mtakatifu. (Waefeso 3:16-17)
- ▶ Kristo hayumo ndani ya mtu huyu. (1 Yohana 3:24)
- ▶ Mtu huyu hajapokea nguvu ya kushuhudia kwa ajili ya Kristo. (Matendo 1:8)
- ▶ Mtu huyu hutenda kwa namna ya kibinadamu (1 Kor. 3:3) ambako kwa urahisi sana huweza kusababisha mashindano na mvutano.
- ▶ Kama kanuni ni vigumu kwa mtu huyu kupokea maonyo
- ▶ Maisha yao ya maombi yanaweza kuwa hayajakamilika.
- ▶ Mtu huyu ana uwezo wa kibinadamu tu wa kusamehe na kutokuwa na kinyongo.

Mkristo wa tabia ya mwilini hutenda wakati mwagine kama mtu wa tabia ya asili. Paulo anasema: "... *Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu*" (1 Wakorintho. 3:3). Wakati mwagine matendo yake ni kama yale ya mtu wa rohoni, japokuwa anaishi kwa nguvu na uwezo wake mwenyewe

Mkristo wa kiroho anapata utimilifu wa Mungu

'Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo acae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingu, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu. Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina. Waefeso 3:16-21 NKJV

ATHARI ZA UKRISTO WA TABIA YA MWILINI

Ninasikitika kwa hasara iliyopatikana katika familia yangu na kwa kanisa langu nilipofanya kazi kama mchungaji kama matokeo ya mimi kukosa Roho Mtakatifu. Katika eneo hili ni kweli pia kwamba hatuwezi kumwongoza mtu mbali kuliko tulipo sisi wenyewe. Tunapaswa pia kutambua kwamba ukosefu binafsi wa Roho Mtakatifu kwa mtu mmoja mmoja huongezeka au huzidi ndani ya familia na kanisa.

Watoto na Vijana

Ukristo wa tabia ya mwilini sehemu ya mazalia kwa maisha ya Mkristo ambaye hafungwi na kanuni za kimaadili. Watu kwa kutokujua hujaribu wakiwa na nia njema kufanya kile wasichowenza kufanya na kisha kutafuta njia ya kutokea. Je hii ndiyo sababu tunapoteza vijana wetu wengi? Je sisi kwa kutokufahamu au kwa sababu nyingine tumeweka mfano kwa watoto wetu na vijana wadogo wa Ukristo wa tabia ya mwilini? Matokeo yake, wamekuwa Wakristo wa tabia ya mwilini na kisha kuteseka na kukata tama? Je hii ndiyo sababu kwa nini wengi hawalichukulii umuhimu wake au hawaji kanisani tena au wameliacha kanisa?

Muda si mrefu uliopita kaka mzee aliliambia kanisa lake: "Iko sababu kwa ajili ya matatizo tuliyu nayo leo maishani mwetu na katika maisha ya vijana wetu: vizazi vya zamani vimeshindwa kuelewa kazi ya Roho Mtakatifu na kujazwa na yeze."⁶⁹

Naomba niwakumbushe tena juu ya madhara ya kuwa katika hali ya uvuguvugu (kutokujisalimisha kwa Kristo kikamilifu): "Wakristo waliojitoa nusu nusu ni wabaya kuliko wasioamini: kwa maneno yaoya udanganyifu na hali yao ya kutojitoa huongoza wengi upotevuni. Wasioamini huonyesha rangi zao. Mkristo vuguvugu hudanganya pande zote [waaminio na wasioamini]. Yeye si mwana wa ulimwengu wala Mkristo. Shetani humtumia kutenda kazi ambayo hakuna hata mtu mmoja anayeweza kuifanya."⁷⁰

Hata hivyo, kama tukiishi kiroho, tunaweza kuwaonyesha watoto wetu njia ili kupata msaada wa Mungu. Ellen White anasema kitu fulani cha kushangaza sana:

"Wafundishe watoto wako kwamba ni upendeleo kwoa kila siku kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mruhusu Kristo akupatie mkono wake wa msaada kutimiza makusudi yake. Kwa maombi unaweza kupata uzoefu ambao utaifanya huduma yako kwa ajili ya watoto wako kuwa mafanikio halisi."⁷¹

Tuliwafundisha watoto wetu kuomba. Lakini je tumewafundisha kuomba kila siku kwa ajili ya Roho Mtakatifu? Au sisi wenyewe hatukulitambua hilo? Wakati huo mke wangu pamoja na mimi hatukulifahamu hilo. Ninamshukuru Mungu kwa kuwa hakutazama wakati huu tulipokuwa hatuna uelewa. Lakini matokeo yake ni hasara gani ilitokea?

Ni watoto wazuri kiasi gani wazazi wa kiroho wangkuwa nao wakati wanapojikabidhi kila siku kwa Yesu na kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

Hali –

Upendo wa Kiungu au kuwa mwema tu kwa kila mtu??

Kuna tofauti gani katika hali ya ndoa na familia, kanisa na ushirika pamoja na Wakristo wa tabia ya mwilini au wa rohoni, kama uwezo wa Mungu unakosekana kwa maisha yenye nidhamu, kama upendo wa Mungu unakosekana na nguvu ya dhambi haijavunjwa au ikiwa mambo haya yanapatikana kuititia neema ya Mungu?

⁶⁹ Garrie F.Williams, *Erfülltsein vom Heiligen Geist – Wie erfahren wird das?* (Lüneburg 2007), S.8

⁷⁰ EGW Letter 44, 1903, quoted in Adventist Bible Commentary, Vol.7, uk.963 on Rev. 3:15-16

⁷¹ E.G.White, Child Guidance (1954), uk. 69

“Wakati watu wa Mungu ni wamoja katika umoja wa Roho, Ufarisayo wote, na kujihesabia haki kote, ambayo ilikuwa ni dhambi ya taifa la Kiyahudi, vitaondolewa kutoka katika miyo yote.”

Wakristo wa tabia ya mwilini wenye msimamo mkali hujaribu kukosoa. Hili si jambo jema. Japokuwa tunapaswa kuzungumzia maagizo mazuri ya Mungu, tunapaswa kwa wakati huo huo kutambua kwamba badiliko la msingi litatokea wakati ambapo badiliko huanzia ndani.

Watu wenyewe kupendelea mabadiliko hawachukulii mambo kwa umakini na hubadilika kufuatana na njia za kidunia. Mungu hawezi kubariki hili pia.

Joseph Kidder aligundua yafuatayo kuhusu hali ya jumla ya kanisa wakati wa sasa: “Ukosefu wa ari na shauku, kuwa wa juu juu, kupenda dunia, kutokuwa wakarimu, wachungaji wamechoka, vijana wanaliacha kanisa, nidhamu kidogo, mipango isiyo na mwongozo au matokeo halisi, ukosefu wa kudumu wa watu thabiti na waliojitoa.”⁷²

Chanzo cha tatizo letu ni ukosefu wa muunganiko na Yesu (Yohana 15:1-5) na kutegemea sana uwezo wa kibinadamu (Zakaria 4:6). Kidder pia anaona suluhisho katika maisha yaliyojazwa na Roho Mtakatifu (Matendo 1:8).

Yesu alitupatia amri mpya:

“Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.” (Yohana 13:34-35)

Kupenda kama Yesu anavyofanya humaanisha: kupenda upendo wa kimbingu (pendo la agape). Tunaweza kufanya hivi pale tu tunapokuwa tumejazwa na Roho Mtakatifu.

“Upendo mkuu kwa Mungu na upendo usio na ubinafsi kwa wanadamu wenzetu – hii ni zawadi bora kabisa ambayo Baba yetu wa mbinguni anaweza kutoa. Upendo huu sio muhemuko wa ghafla, bali ni kanuni ya kimbingu, nguvu ya milele. Moyo usiowekwa wakfu [kila mtu, ambaye hana Roho Mtakatifu,

⁷² Dr. S. Joseph Kidder, Anleitung zum geistlichen Leben (Andrews University), PPP Folie 3+4

anao] hauwezi kuwa chanzo au kuzalisha [aina hii ya upendo]. Ni katika miyo pekee ambayo Yesu hutawala ndipo [upendo huu] hupatikana.”⁷³

Nafikiri kuna tofauti ikiwa sisi ni wema “tu” kwa kila wenzetu au tukienda mbali zaidi ya hapo na kupenda kwa pendo la Mungu. E. G. White anatupatia dokezo muhimu:

“Kwa kucaa vazi la upole na roho ya ukimya, matatizo tisini na tisa kati ya mia moja yanayofanya maisha kuwa ya uchungu yanaweza kuepukwa.”⁷⁴

Neno la Mungu katika 1 Wathesalonike. 4:3-8 huonyesha kitu fulani kuhusu maisha ya ndoa. Pamoja na mambo mengine mafungu haya huzungumzia kuishi katika utakatifu na heshima ya ndoa. Hupingana hisia za tamaa ya Mataifa. Kwa sababu yanataja maisha ya utakaso mara tatu na pia kuwa na Roho Mtakatifu, tunatambua kuwa maisha pamoja na Roho Mtakatifu yanaweza na yanapaswa kubadilisha mahusiano ya ndoa zetu pia. Mungu alikusudia tuwe na furaha kubwa na utimilifu katika maisha yetu ya ndoa. Je hili halituonyeshi kwamba Mungu anataka kutusaidia kuhusiana kwa upendo wa dhati badala ya tamaa?

Yesu aliomba kwa ajili ya umoja wa wanafunzi wake: “*Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe ulijenituma.*” (Yohana 17: 21 NKJV)

William G. Johnsson anasema: “Waadventista wengi bado wanapaswa kutafakari kile inachomaanisha kuwa wamoja na Kristo. Huko nyuma huenda hatukuweka umuhimu wa kutosha kwenye jambo hili au tuliweka msisitizo mahali pasipostahili.”⁷⁵

Kristo yuko ndani yetu pale tunapoja zwa na Roho Mtakatifu. Ukristo wa Kiroho huchangia maombi yetu kujibiwa na Mungu. E. G. White anasema: “Wakati watu wa Mungu ni wamoja katika umoja wa Roho, Ufarisayo wote, na kujihesabia haki kote, ambayo ilikuwa ni dhambi ya taifa la Kiyahudi, vitaondolewa kutoka katika miyo yote... Mungu atafanya ijulikane siri ambayo ilikuwa imejificha kwa vizazi vingi. Atafunua ‘utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu’ (Wakolosai 1:27).”⁷⁶

⁷³ E.G. White, *Acts of the Apostles* (1911) uk. 551.2

⁷⁴ E.G. White, *Testimonies for the Church*, volume 4, uk. 348.3

⁷⁵ William G. Johnsson, *Adventgemeinde in der Zerreißprobe*, (Lüneburg 1996), uk. 118

⁷⁶ E.G. White, *Selected Messages*, Book 1 (1958), uk. 386.1

Mashauri ya Marudi

Je kutakuwa na matokeo kwenye mashauri ya marudi wakati hayajafanyika au yamefanyika kwa kiasi kidogo cha upendo wa Mungu? Ni maamuzi gani yatachukuliwa na kanisa, ambalo kwa sehemu kubwa limeundwa na Wakristo wa tabia ya mwilini au hata [kanisa hilo] lina mchungaji au mwenyekiti wa tabia ya mwilini? Ninapotafakari huko nyuma kwenye kazi yangu kama mchungaji, basi ninashawishika kwamba washiriki wa kiroho hujaribu kuwarejesha washiriki walioanguka kwenye ukweli. Na wakati mtu anapotubu na kuungama, basi mashauri yametimiza kusudi lake. Wakati mwingine Wakristo wa tabia ya mwilini hujaribu kutumia mashauri kama adhabu na hata kuitumia vibaya kwa kutumia madaraka (Mathayo. 18:15-17; 1 Wakorintho. 3:1-4; 2 Wakorintho. 10:3; Yuda 1:19).

NENO LA MUNGU LA KIUNABII KWA SIKU ZA MWISHO

Mungu ana desturi ya kufunua matukio muhimu kupitia manabii wake (Amosi 3:7). Hivyo alitoa ujumbe muhimu wa kiunabii kwa ajili ya siku za mwisho kupitia kwa Ellen White. Kwa sababu mambo mengi yatakuwa tofauti kabisa kuliko nyakati zilizopita, ilikuwa ni muhimu na lazima kuwa na maelezo mengine ya ziada kutoka kwa Mungu. Leo tungeweza kuita “habari mpya”. Kulingana na Ellen White ujumbe huu ni muhimu mpaka Yesu anapokuja tena. Kwa kuwa ushauri wake hujumuisha badiliko la mtindo wa maisha, maonyo, makaripio, n.k., mtu wa kiroho anaweza kuyapokea kwa urahisi kuliko mtu wa tabia ya mwilini. (Lakini sababu kwamba mtu fulani huyachukulia mashauri haya kwa umakini, haimaanishi moja kwa moja kwamba ni mtu huyo ni wa kiroho.) Ingekuwa ni busara kutafakari maneno kutoka Kumbukumbu la Torati 18:19: “*Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule [nabii] kwa jina langu, nitalitaka kwake.*”

Hili hutuonyesha wazi kwamba ujumbe kutoka kwa nabii wa kweli haupaswi kuhusiana na mtu huyo, bali Mungu mwenyewe. Tunawezaje kutambua kama mtu fulani ni nabii wa kweli? Neno la Mungu hutupatia pointi tano za kumpima. Nabii wa kweli anapaswa kukubaliana na pointi zote tano.

1. Mwenendo wake wa maisha – “Mtawatambua kwa matunda yao.” Mathayo 7:15-20
2. Kutimizwa kwa unabii: Kumb. 18:21-22 (Isipokuwa kwa unabii wenyewe masharti– Kwa mfano Yona.)
3. Wito wa kuwa mwaminifu kwa Mungu (Neno la Mungu). Kumb. 13:1-5
4. Kumtambua Yesu kama nafsi halisi na Mungu wa kweli. 1 Yohana 4:1-3
5. Kukubaliana na mafundisho ya Biblia. Yohana 17:17

Amri zote za Mungu, pamoja na mashauri yake kupitia manabii, ni kwa faida yetu wenyewe. Ndiyo maana yana thamani ya kipekee. Hivyo watu wa kiroho wanaweza kutii kwa uwezo wa Mungu na kwa furaha na kujua kwamba huchangia katika mafanikio maishani. “*Mwaminini Bwana, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika; waaminini manabii wake, ndivyo mtakavyofanikiwa.*” (2 Mambo ya Nyakati 20:2ob NKJV)

Mwogozo wetu wa kujifunza Biblia unasema yafuatayo kuhusu mahusiano kati ya uzima pamoja na Roho Mtakatifu na Neno la nabii wa kweli: “Wale wanaokataa neno la kiunabii, hujifungia wenyewe wasipokee maelekezo ya Roho Mtakatifu. Matokeo ya sasa hayana tofauti na ilivyokuwa zamani—kupoteza uhusiano pamoja na Mungu na kuwa tayari kwa mivuto hasi.”⁷⁷

KUANDAA MPANGO/MKAKATI

Kazi muhimu ni kutafuta suluhisho madhubuti na mbinu bora kwa majukumu yaliyoko ndani ya kanisa na katika kazi ya umishenari. Ni suala la mipango yetu na mikakati yetu. Zaidi sana linahusiana na kuliumarisha kanisa kiroho na kuongoa roho nyingi zaidi.

Nimebatizwa kwa miaka 65 na nimekuwa mchungaji kwa miaka 43. Tumeandaa programu nyingi na mbinu za kuzitekeleza. Tulikuwa na juhudini nyingi sana. Kwa muktadha huu ninapaswa kufikiria tena kuhusu maneno ya Dwight Nelson katika kikao cha Konferensi Kuu mwaka 2005.

“Kanisa letu limeandaa mifumo, mbinu, mipango na programu kwa bidii sana, lakini ikiwa hatutakiri [kuwa tuna] ukosefu wa kiroho [Ukosefu wa Roho Mtakatifu], ambao umewakamata wachungaji wengi sana na viongozi wetu, hatutakwenda zaidi ya Ukristo wetu wa kawaida.”⁷⁸

Kwa mtazamo ule ule Dennis Smith anasema yafuatayo:

“Sipingi mipango, programu au mbinu. Lakini ninaogopa kwamba mara nyingi tunategemea mambo haya kupeleka mbele kazi ya Mungu. Mipango, programu na mbinu havitamaliza kazi ya Mungu. Wahubiri wakubwa, matamasha mazuri ya Kikristo, matangazo kwa njia ya satelaiti hayatamaliza kazi ya Mungu. Roho wa Mungu ataimaliza kazi—Roho wa Mungu anenaye na kuhudumia kupitia kwa waume na wanawake waliojazwa na Roho.”⁷⁹

⁷⁷ Studienanleitung Standardausgabe, Philip G. Samaan, 10.11.1989, to question 8

⁷⁸ Helmut Haubeil (Hrsg.), Missionsbrief Nr. 34, (Bad Aibling, 2011) page 3

⁷⁹ Dennis Smith, *40 Days – Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming*

UBATIZO/KUONGOA ROHO

Biblia hutonyesha kwamba Roho Mtakatifu ni sharti la muhimu katika kuwaleta watu kwa Kristo (angalia kitabu cha Matendo). Ujerumani kwa upande mmoja, tuna makanisa ambayo yanakua na upande mwagine, makanisa ambayo yamedumaa au kusinyaa. Duniani kote idadi ya washiriki kanisani kwetu imekua mara ishirini katika kipindi cha miaka 60. Hakika tunaweza kutaja sababu kadhaa kwa hali hii Ujerumani. Lakini jambo moja liko wazi kwangu: Sababu kuu ni ukosefu wa Roho Mtakatifu. Katika hali ya kawaida tatizo hili limetuzonga kwa kiasi kikubwa. Tumetengeneza au kuwa na mipango na program nyingi. Tumeona kwamba ukosefu wa Roho Mtakatifu katika juhudhi zote hizi umepelekea upotewe wa fedha na muda kwa kuwa tulifuata njia zisizohitajika au zisizo na mafanikio. Nukuu mbili kutoka kwa E. G. White zinaonyesha hali hii:

“Bwana kwa sasa hafanyi kazi ya kuleta roho nyingi kwenye ukweli, kwa sababu ya washiriki wa kanisa ambao kamwe hawajawahi kuongoka na wale ambao walionganoka hapo awali lakini kwa sasa wamerudi nyuma. Ni mvuto gani ambao washiriki hawa wasiotakaswa [Wakristo wa tabia ya mwilini] wangeuleta kwa waongofu wapya?”⁸⁰

“Kama tungeweza kujinyenyikeza mbele za Mungu, na kuwa wakarimu na wapole na wenye huruma na wema, kungekuwepo na waongofu mia moja kwa kila muongofu mmoja tu aliyepo sasa.”⁸¹

Kwa upande mwagine, tuna ubatizo wa watu, ambao hawajaandaliwa vyakutosha. E. G. White alisema:

“Kuzaliwa upya ni uzoefu wa nadra sana katika zama hizi za ulimwengu. Hii ndiyo sababu kuna mkanganyiko mwangi makanisani. Wengi, wengi sana, ambao wanatalaja jina la Kristo hawajatakaswa na si watakatifu. Wamebatizwa, lakini walizikwa wakiwa hai. Ubinafsi haukuwa, na kwa hiyo hawakuinuka katika upya wa uzima katika Kristo.”⁸²

Haya yaliandikwa mwaka 1897. Hali ikoje leo? Tatizo ni kwamba: Yeyote ambaye hajazaliwa upya hajajazwa na Roho Mtakatifu. Yesu alisema: “Yesu

(Wien, 2012), uk. 88

⁸⁰ E. G. White, *Testimonies for the Church* Vol. 6, (1901) uk. 370.3

⁸¹ E. G. White, *Testimonies for the Church* Vol. 9 (1909), uk. 189.4

⁸² E. G. White, MS 148 (1897)

akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu." (Yohana 3:5). Je si kweli kwamba tunashuhudia ukosefu wa Roho Mtakatifu kila mahali?

ROHO MTAKATIFU NA KUHUBIRI

Mungu hutuambia yafuatayo kuhusu na maana ya Roho Mtakatifu na kuhubiri: "Kuhubiri neno hakutakuwa na maana yeote bila kuwepo wakati wote kwa Roho Mtakatifu na bila msaada wake. Huyu ndiye mwalimu pekee mwenye ufanisi wa ukweli wa kimbingu. Ni pale tu ambapo ukweli utaingizwa ndani ya moyo na Roho ndipo utakapogusa nia au kubadilisha maisha. Mtu anaweza kuwasilisha barua ya neno la Mungu, anaweza kufahamu amri na ahadi zake zote; lakini isipokuwa Roho Mtakatifu ameweke kweli moyoni, hakuna nafsi itakayoanguka juu ya Mwamba na kuvunjika. Hakuna kiwango chochote cha elimu, hakuna mali, iwe kubwa kiasi gani, inayoweza kufanya mwale mmoja wa mwanga pasipo ushirikiano na Roho wa Mungu."⁸³

Kuhubiri hakufanyiki wakati wa hubiri tu, lakini pia katika masomo, mafundisho ya Biblia au vikundi vyta kuhudumia watu.

Randy Maxwell anasema:

"Lakini ukweli ni kwamba, tunakufa kwa kiu ya kuwasiliana na Mungu aliye hai!"⁸⁴

Je ukosefu wa Roho Mtakatifu ni chanzo cha hofu pia? Je Emilio Knechtle angeweza kuwa sahihi aliposema: "Kwa nini hatufanikiwi katika kuupindua juu chini ulimwengu huu ulioharibika? Jambo fulani limekosewa katika imani zetu. Tunaogopa migogoro, tunaogopa kukorofishana hasa na watu walioko madarakani, tunaogopa matatizo, tunogopa kupoteza kazi zetu, tunaogopa kupoteza sifa zetu, tunaogopa kupoteza maisha yetu. Hivyo tunanyamaza na kujificha. Tunaogopa kutangaza injili kwa ulimwengu kwa namna ya upendo lakini kwa ushujaa."⁸⁵

Suluhisho kwa tatizo hili linapatikana katika Matendo 4:31: "*Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.*"

⁸³ E. G. White, *The Desire of Ages* (1898), uk. 671.4

⁸⁴ Randy Maxwell, *If my people pray ...* (Pacific Press, 1995), uk.11

⁸⁵ CD *Die letzte Vorbereitung*, Teil 6

ROHO MTAKATIFU NA VITABU VYETU

Yafuatayo yamesemwa kuhusu vitabu vyetu: "Ikiwa mwandishi ana wokovu wa Mungu, roho huyo huyo [wa mwandishi] atamgusa msomaji. Ujumbe ulioandikwa chini ya uongozi wa Roho wa Mungu malaika hutoa kibali, na humgusa msomaji kwa namna hiyo hiyo. Lakini ujumbe ulioandikwa wakati mwandishi haishi maisha makamilifu kwa utukufu wa Mungu, wakati hajajitoa kabisa kwake malaika huhisi ukosefu [wa Roho Mtakatifu] kwa huzuni. Huondoka na hawamgusi msomaji kwa sababu Mungu na Roho wake hawamo ndani yake. Maneno ni mazuri lakini yanakosa mvuto wa Roho Mtakatifu."⁸⁶

Ninataka kusisitiza kwa mara nyingine tena: Kwa kawaida sio kila kitu tulichofanya hakikuwa sahihi. Kwa vyovyote vile hapana. Tumeandaa mambo mema na mazuri sana; Mungu hakika amebariki juhud zetu za kibinadamu kwa kadri inavyowezekana. Lakini swalii la muhimu ni: Je tunafanya hizi kazi kama Wakristo wa tabia ya rohoni au ya mwilini? Jambo moja ni dhahiri: Tunapohangaika kutafuta suluhihisho katika hali ya kimwili, tutawekeza muda mwingi bure; tutafanya kazi nyingi, ambazo hazitakuwa na maana.

ROHO MTAKATIFU: HAKUNA MVUA YA VULI, HAKUNA MVUA YA MASIKA

"Mvua ya masika, kujazwa na Roho Mtakatifu, hutupatia ukomavu muhimu wa kiroho, amba ni wa lazima ili tuweze kunufaika na mvua ya vuli."⁸⁷

"Mvua ya vuli, kuivisha mazao ya nchi, huwakilisha neema ya kiroho mbayo huliandaa kanisa kwa ajili ya kuja kwa Mwana wa Adamu. Lakini isipokuwa mvua ya masika imenesha, hakutakuwepo na uhai; tawi la kijani halitachipua. Isipokuwa manyunu ya kwanza yamefanya kazi yake, mvua ya vuli haiwezi kuifanya mbegu kuwa katika ukamilifu."⁸⁸

ROHO MTAKATIFU NA UTAKASO WA KIBIBLIA

"Kazi hii (utakaso wa kibiblia) unaweza kukamilika kupitia imani katika Kristo pekee, kwa uweza wa Roho wa Mungu aishiye ndani yetu."⁸⁹

⁸⁶ E. G. White, *PH* 016, uk. 29.1

⁸⁷ Dennis Smith, *40 Days – Prayer and Devotions to Revive Your Experience with God*, Book 2, (Vienna, 2013), uk. 175

⁸⁸ E. G. White, *The Faith I live By*, (1958), uk. 333.3

⁸⁹ E. G. White, *The Great Controversy*, (1911), uk. 469.3

UTUME MKUU PASIPO ROHO MTAKATIFU?

Je inawezekana kuwa taasisi kubwa, programu za kiinjilisti zenyе mafanikio na mikakati madhubuti ya kimishenari imeandaliwa pasipo Roho Mtakatifu? Andrew Murray, mmishenari mkuu aliyetumwa Afrika Kusini, alitambua kwamba hali hii iliwezekana, na, kwa kwa hakika, ni hali halisi kwa wengi katika Ukristo alipoandika:

“Ninaweza kuhubiri au kuandika au kutafakari, na kufurahia kujazwa na mambo yaliyomo ndani ya Kitabu cha Mungu na katika Ufalme wa Mungu; na bado nguvu ya Roho Mtakatifu isiwepo kwa kiwango kikubwa. Nina wasiwaswi kwamba ikiwa utachukua mahubiri katika Kanisa lote la Kristo na kuuliza kwa nini kuna, utashangaa! nguvu kidogo sana ya kuongoa katika kulihubiri Neno, kwa nini kuna kazi kubwa sana na mara nyingi mafanikio hafifu kwa ajili ya umilele, kwa nini Neno lina nguvu kidogo sana katika kuwajenga waumini katika utakatifu na katika utakaso – jibu litakuja: Ni ukosefu wa nguvu ya Roho Mtakatifu. Na kwa nini inatokea hivi? Haiwezekani kuwepo sababu nyingine yoyote bali ni kwamba mwili [tazama Wagalatia 3:3] na uwezo wa kibinadamu vimechukua nafasi ambayo Roho Mtakatifu alipaswa kuwa nayo.”⁹⁰

ROHO MTAKATIFU NA AFYA

“Basi, ndugu zangu, nawashihi, kwa huruma zake Mungu, *itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.*” Warumi 12:1

“Hamui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.”¹ Wakorintho 3:16-17

“Au hamui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenywewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.”¹ Wakorintho. 6:19-20 (Tazama pia: Kutoka 15:26)

Watu waliojazwa na Roho Mtakatifu ni hekalu la Mungu. Je umewahi kukaa na kutafakari jambo hili lina maana gani maishani mwako? Hekalu ni mahali anapoishi Mungu. Mungu akamwambia Musa: “*Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao.*” Kutoka 25:8

⁹⁰ Randy Maxwell, *If My People Pray* (Pacific Press 1995), uk. 145

Ikiwa tutachukulia kauli hii kwa umakini, basi kulinda afya zetu na mtindo wetu wa maisha itakuwa sehemu nyeti ya uanafunzi wetu. Miili yetu ni mali ya Mungu. Je unataka kutunza mali ya Mungu kwa uangalifu? Ndiyo, tunataka kuitunza miili yetu kwa uangalifu na kwa hakika kulingana na maagizo ya Mungu! Hili linahitaji kiasi fulani cha nidhamu. Mtu fulani, ambaye amejazwa na Roho Mtakatifu, anaweza na mara nyingi kutekeleza hili kwa furaha. Malipo ni afya njema ya mwili, nafsi na roho. Mtu fulani, ambaye hajajazwa na Roho Mtakatifu, atahangaika na kupata hasara. Mungu anatarajia kwamba tuwe na afya njema ya mwili na roho kwa kadri iwezekanavyo kwa ajili ya utukufu wake, kwa ajili ya huduma yake na kwa ajili ya furaha yetu wenyewe. Katika hili hakuna mbadala wa kujazwa na Roho Mtakatifu. Yesu anapoishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu, basi basi anakuwa “*Bwana akuponyaye.*” (Kutoka 15:26) Uponyaji wakati wote ni bora kwa ajili ya mgonjwa na kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Hili linaweza kuleta swalii. Je daktari wa kimbingu humponya kila mtu?

“Mwanamke mzee wa Kikambodia alikuja kama mkimbizi kwenye hospitali ya kimishenari, ambayo ilikuwa katika kambi ya wakimbizi huko Thailand. Alikuwa amevaa nguo za mtawa wa Kibudha. Aliomba atibiwe na Daktari Yesu. Hivyo wakamwambia kuhusu Yesu. Aliweka tumaini lake katika Yeye na aliponywa mwili na roho. Alipoweza kurudi Kambodia aliweza kuongoa watu 37 kwa Kristo.”⁹¹

Wakati wa ugonjwa wa mfalme mtiifu Hezekia Bwana alimtumia ujumbe: “*Tazama, nitakuponya.*” (2 Wafalme 20:1-11) Lakini kwa nini Bwana hakumponya kwa neno, bali alimpatia kazi ya kuweka mkate wa tini? Je inawezekana kwamba Mungu anategemea ushiriki wetu kupitia uponyaji wa asili au mabadiliko katika milo yetu, mazoezi, mapumziko, n.k.? Kwa nini Mungu hakumponya Paulo na kumuachia “mwiba katika mwili wake”? Paulo mwenyewe anasema: “*Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo.*” (2 Wakorintho 12:7-10) Hata hivyo E. G. White hutwambia: “Mvuto wa Roho wa Mungu ndiyo dawa bora zaidi ambayo mgonjwa mume au mke anaweza kuipokea. Mbingu yote ina afya njema; na kadri ambavyo ushawishi wa kimbingu unapokelewa kwa dhati, ndivyo ambavyo mgonjwa anayeamini atakavyopona kwa uhakika.”⁹²

Je si jambo jema na la muhimu juu kile mfanyakiashara mmoja alichokiandika? Alisimulia jinsi ambavyo semina zote za afya hazikumpatia nafuu yoyote. Lakini

⁹¹ Author unknown, *Our Daily Bread – Worship book* (RBC Ministries), 26. Nov. 1993

⁹² E. G. White, *Medical Ministries* (1932) uk.12.3

tangu alipoanza kuomba kila siku kwa ajili ya Roho Mtakatifu, alikuwa amehamia kabisa kwenye mtindo bora wa maisha na alikuwa ameanza kutumia chakula cha mboga mboga⁹³ Je hili halionyeshi kwamba kujazwa na Roho Mtakatifu kunawenza kutuhamasisha na kutupatia uwezo sambamba na furaha kuupokea mtindo bora wa maisha?

Dada mmoja alisoma uzoefu huu. Aliandika: Kupitia kujisalimisha kwangu kikamilifu kwa Yesu, Mungu amebadilisha maisha yangu kabisa ndani ya muda mfupi. Baada ya ombi langu la kujitoa nilikwenda jikoni na asubuhi iliyofuata, nilisimama kwenye mashine ya kuchemshia kahawa, nikatikisa kichwa changu na kusema moyoni: hapana, sinywi kahawa tena. Huko nyuma jambo hili lisingewezekana kabisa, kwa sababu nilipajaribu kuacha kunywa kahawa, nilikuwa napata maumivu makali ya kichwa kwa siku tano – hizi zilikuwa dalili kuu zilizotokana na kuacha kutumia kahawa. Wakati huu hata sikufikiria ni madhara gani ningeyapata. Nilifahamu tu kwamba sikutaka kunywa kahawa tena. Leo sina hamu tena ya kahawa.⁹⁴ Hili lilikuwa ni badiliko moja tu kati ya mabadiliko mengi maishani mwake. (Ninapendekeza kitabu cha 5 kitiwacho “Andreasbrief” kuhusu ushindi dhidi ya tumbaku na pombe kwa mtu ye yote anayetaka kuwa huru dhidi ya uraibu. Kinaelezea kwa upana jinsi ya kupona kupitia maombi na ahadi (kinapatikana kwa Kijerumani pekee.⁹⁵)

Maisha pamoja na Roho Mtakatifu yata kuza kwa kiasi kikubwa matengenezo ya afya. Ni suala la maelezo ya kiafya yanayoambatana na nguvu ya kubadilisha. Don Mackintosh, Mkurugenzi wa Newstart Global, Weimar, CA, anasema:

“Hitaji kuu la wakati wetu sio tu kuwa na elimu ya afya – tuna maelezo bora kabisa. Kinachohitajika ni maelezo ya afya pamoja na nguvu ya kuyatekeleza, ambayo ni nguvu ya kubadilisha.”⁹⁶

Dkt. Tim Howe anasema:

“Elimu ya afya pekee si kazi ya kimishenari. Elimu ya afya haileti uponyaji wowote kama ambavyo sheria ya Mungu haiwezi kuleta wokovu. Ili kuwa na afya au wokovu nguvu ya Mungu ibadilishayo lazima iwepo.”⁹⁷

Mwisho, ningependa kuuliza swali: Vipi kuhusu uponyaji wa imani? Je lolote linawenza kutarajiwa pasipo kujazwa na Roho Mtakatifu? (Tazama Marko 16:17-18; Yakobo 5:14-16)

⁹³ Email from 7.3.2013

⁹⁴ Email from November 18, 2014 from Sister M.

⁹⁵ Andreasbrief Nr.5, Sieg über Tabak und Alkohol, www.missionsbrief.de – Andreasbriefe. Man kann ihn auch beziehen bei Wertvoll leben, Adventist Book Center und TopLife – Wegweiser Verlag.

⁹⁶ Dave Fiedler, D’Sozo, (Remnant Publications), Forward

⁹⁷ Dave Fiedler, D’Sozo, (Remnant Publications), Forward

MAANDALIZI KWA AJILI KUJA KWA YESU MARA YA PILI

Hakuna mbadala wa ushirika wa karibu pamoja na Yesu kupitia Roho Mtakatifu kama maandalizi kwa ajili ya kuja kwa Yesu Mara ya Pili (au kufariki katika Bwana). Wakati Kristo anapoishi ndani yangu kupitia Roho Mtakatifu, basi niko tayari kupitia neema yake. Maeneo matatu yanaweza kuonyesha hili. (Hili limeelezewa kwa undani katika kitabu cha *Spirit Baptism and Earth's Final Events*, kilichoandikwa na Dennis Smith.)

Uhusiano Binafsi na Kristo

Yesu alisema: “*Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.*” (Yohana 17:3) »Kujua [know]« kuna maana pana sana katika Biblia kuliko ilivyo katika lugha ya Kiingereza leo. Humaanisha kujitoa kwa namna ya ukamilifu, mapatano na upendo. Hupatikana tu katika maisha pamoja na Roho Mtakatifu. Wazo hili huelezewa katika nukuu ifuatayo:

“Ni lazima tuwe na mahusiano hai pamoja na Mungu. Ni lazima tuvikwe na nguvu kutoka juu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, ili tuweze kufikia kiwango cha juu; kwa maana hakuna msaada kwetu kwa namna nyingine yoyote.”⁹⁸ Katika mfano wa wanawali 10 Yesu alisema kwa wapumbavu: “*Siwajui ninyi.*” Sababu ilikuwa nini? Ukocefutu wa mafuta, ambao huwakilisha ukocefutu wa Roho Mtakatifu. (Mathayo 25:1-13). Watu, waliomsulubisha Yesu, walikuwa na uelewa mkubwa wa Agano la Kale. Lakini kwa sababu ya tafsiri yao potofu hawakutafuta mahusiano binafsi pamoja na Yesu

Je tunafahamu kwamba kizazi cha siku za mwisho, kutokana na mazingira ya siku za mwisho, kitahitaji kuwa na mahusiano ya karibu zaidi pamoja na Mungu?

Haki kwa Imani

Ujumbe wa mwisho wa Mungu kwa wanadamu katika ujumbe wa malaika wa tatu unahu suala la kutangazwa kwa “injili ya milele”(Ufunuo 14:6-7). Ujumbe huu una umuhimu gani kiasi kwamba ulimwengu wote unapaswa kuusikia na utausikia? Ni haki kwa neema kupitia imani katika Yesu Kristo pekee (Waefeso 2:8-9). Wale ambao wanautangaza ujumbe huu wa mwisho kwa nguvu, ni lazima wao wenyewe waguswe na nguvu ya ujumbe huu. Wanapaswa kujua na kupitia uzoefu wa haki kwa imani kupitia Yesu pekee kama mtoaji msamaha

⁹⁸ E. G. White, *Review and Herald*, April 5, 1892

na mkombozi kutoka dhambini. Hili linawezekana tu katika maisha yaliyojazwa na Roho Mtakatifu ambayo kuititia Yesu Kristo anaweza kutufanya tuwe watiifu. Yesu kuishi ndani yetu hudhihirishwa na utii kwa amri zote za Mungu. Ulimwengu utaangazwa kwa ujumbe huu (Ufunuo 18:1).

Kuipenda Kweli

Kutakuwa na athari gani maishani mwetu leo tukiwa nayo au hatuna maisha yaliyojazwa na Roho Mtakatifu kuhusu **kupenda kweli, kujifunza neno la Mungu na kutenda kulingana na kweli maishani mwetu?** 2 Wathesalonike 2:10 inasema kwamba "... *hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa.*" Wale ambao hawawezi kudanganywa, wanapenda kweli miyoni mwao. Tunaupataje upendo huu? Tunaweza tu kuwa nao wakati ambapo Yesu Kristo anaishi ndani yetu kuititia Roho Mtakatifu. Warumi 5:5 inasema kwamba upendo ulioko miyoni mwetu hutoka kwa Roho Mtakatifu. Waefeso 3:17 hutwambia kwamba tutakuwa "*shina na msingi katika upendo*" kuititia Roho Mtakatifu. Katika Yohana 16:13 Roho Mtakatifu anaitwa "*Roho wa kweli*". Hili hutuonyesha bayana kwamba ni lazima kuwa Mristo wa kiroho ili kuweza kuwa na upendo kwa ajili ya kweli. Je tuna matatizo leo kuhusu kuipenda kweli, neno la Mungu, maandiko ya kiunabii? Fikiria nyakati zilizopo mbele yetu: "Ni wale tu waliokuwa wanafunzi makini wa Maandiko and walioupokea upendo kwa ajili ya kweli watakaolindwa na udanganyifu mkubwa unaouteka ulimwengu ... Je watu wa Mungu sasa wamejiimarisha kwa uthabiti katika Neno lake kiasi kwamba hawatakubaliana na ushahidi wa akili zao?"⁹⁹

Mungu haulizi ikiwa tumegundua ukweli wote, bali anauliza kama tunaipenda kweli.

TUNDA LA ROHO AU MATENDO YA MWILI

"Mvuto wa Roho Mtakatifu ni uzima wa Kristo ndani ya nafsi. Hatumuoni Kristo na kuzungumza naye, lakini Roho wake Mtakatifu yuko karibu zaidi nasi mahali hapa kama alivyo karibu na mwingine mahali pengine. Hutenda kazi ndani [ya miyoyo] na kuititia kwa kila mtu anayempokea Kristo. **Wale wanaofahamu uwepo wa ndani ya miyoyo wa Roho hudhihirisha matunda ya Roho ...**"¹⁰⁰

⁹⁹ E. G. White, *The Great Controversy* (1911), uk. 625:3

¹⁰⁰ Editor Francis D. Nichol, *Adventist Bible Commentary* Vol. 6 (Hagerstown, 1980), uk. 1112

Wagalatia 5:22: *upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu.*
Waefeso 5:9: *katika wema wote na haki na kweli.*

Wagalatia 5:16-21 Htuonyesha kwamba nguvu ya dhambi itavunjwa ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu.

“... Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka. Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria. (Angalia Warumi 7:23, 8:1) Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, vivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu. (Wagalatia 5:19-21)

KARAMA ZA ROHO

“Katika karama za roho tunamaanisha karama zinazotolewa kwa utendaji wa Roho Mtakatifu, kama zilivyoorodheshwa katika 1 Wakorintho 12:28 na Waefeso 4:11: mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji, waalimu, miujiza, karama za kuponya wagonjwa, masaidiano, maongozi, aina za lugha. Karama hizi zina nafasi katika ‘kuwaandaanwa watakatifu kwa ajili ya kazi ya utume’ ... Huthibitisha ushuhuda wa kanisa na kulipatia uongozi na mwongozo.”¹⁰¹ Roho Mtakatifu pia hutoa talanta zingine kwa kusudi maalum: “katika hekima, na maarifa, na ujuzi, na mambo ya kazi ya kila aina(Kutoka 31:2-6) au ufundi ustadi (1 Mambo ya Nyakati 28:12,19).

Tunapotaka kuwa wanafunzi wa Yesu tunasalimisha kwake kila kitu tulicho nacho na jinsi tuliyyo. Hivyo talanta zetu zote na uwezo wetu, tuliozaliwa nao na pia tulioupata kwa kujifunza, hukabidhiwa kwake ili utumike. Anaweza kutupatia talanta za ziada na/au anaweza kuboresha na kutakasa uwezo wetu wa asili.

Je tunaweza kuwa na karama za roho wakati [huo huo] tuna ukosefu wa Roho Mtakatifu?

CHAGUO LA MUNGU AU CHAGUO LA WATU?

Tuna muundo wa kidemokrasia ndani ya kanisa duniani kote. Lakini kamwe haukuwahi kufikiriwa kama demokrasia ya watu wengi. Lengo halisi la kura zetu

¹⁰¹ Hrsg. Gerhard Rempel, *Schlüsselbegriffe adventistischer Glaubenslehre* (Hamburg), uk. 44

ni kwamba kila mtu aisikilize sauti ya Mungu na kupiga kura kulingana nayo. Kwa kusikiliza sauti ya Mungu huyafanya mapenzi ya Mungu kujulikana kupitia kura. Hakika tunaomba kabla ya kuanza vikao vyovoyote vya baraza la kanisa. Mara kwa mara fursa hutolewa kabla ya kupiga kura kwa ombi binafsi ili kwamba iwe wazi kwa kila mtu jinsi Mungu anavyowataka wapige kura. Nehemia alisema: “*Mungu wangu akanitia moyoni mwangu ...*” (Nehemia 7:5) na E. G. White alisema kuhusu Nehemia sura ya 1: “Naye akaomba, kusudi takatifu lilikuwa limeamshwa akilini mwake...”¹⁰²

Je Mkristo wa tabia ya mwilini ataisikiliza sauti ya Mungu? Ikiwa hajajitoa kwa hiari na kikamilifu kwa Bwana, basi kwa hakika hawezu kupata jibu (Zaburi 66:18; Zaburi 25:12). Ikiwa mtu fulani, ambaye ni Mkristo wa tabia ya mwilini, akipiga kura kwa moyo kwa kadri ya ufahamu wake, basi kibinadamu ni sawa. Lakini wakati makubaliano ya kibinadamu yanapofanyika, hugeuka kuwa udanganyifu na dhambi.

Viongozi wana ushawishi mkubwa katika kazi ya Mungu. Hakika inaleta tofauti kubwa na inaweza kuwa na matokeo makubwa ikiwa ndugu na dada wanaongoza, ambao wameitwa na Mungu au ambao wamechaguliwa kwa kura za mwanadamu.

Wakati nikisoma kitabu juu ya maombi nilitambua kwamba tunaweza kumuomba Mungu atuonyeshe njia tunayopaswa kuiendea. (Zaburi 32:8). Kusikiliza kwa utulivu sauti ya Mungu kumebadilisha maisha yangu yote. Nimeelezea uzoefu huu katika makala inayoitwa “From Business Representative to Pastor” (Inapatikana Kijerumani pekee).¹⁰³ TPia kuna hubiri zuri la kusikiliza kutoka kwa Kurt Hasel “How can I make the right decisions?” (Pia linapatikana Kijerumani pekee)¹⁰⁴ Na pia kuna hubiri zuri la maandishi la miaka mingi iliyopita lilioandikwa na Henry Drummond: “How can I know God’s will?” (Linapatikana katika Kijerumani pekee)¹⁰⁵

Hapa kuna uzoefu ambao ulitokea Oktoba 23, 2014: Kituo cha kimishenari kiitwacho “Country Life Institute Austria” huko Carinthia, Austria (TGMTrainingszentrum fürGesundheitszentrum und Gesundheitszentrum Mattersdorferhof) kilikabiliwa na uamuzi: Je tuongeze jengo zaidi ama la? Kulikuwepo na mambo mengi ya kuunga mkono au kupinga ujenzi wa jingo.

¹⁰² E. G. White, *Southern Watchman* (www.egwwritings.org), March 1, 1904

¹⁰³ www.gotterfahren.info – Gott verändert Leben – Vom Prokurst zum Prediger

¹⁰⁴ www.gotterfahren.info – Wege zum Ziel: Gott erfahren – Gottes Botschaft für unsere Zeit – Thema Nr. 11

¹⁰⁵ Missionsbrief.de – Predigten lesen – Henry Drummond: Wie erkenne ich den Willen Gottes? (Deutsch und Englisch)

Swali la msingi lilikuwa: Mapenzi ya Mungu yalikuwa ni yapi katika jambo hilo? Hatukujadili faida na hasara tena, bali tulioomba kwa siku kumi kwamba Bwana atuandae kuisikiliza sauti yake na kwamba angetupatia jibu lake katika kikao cha maombi mnamo Oktoba 23 (baada ya wageni wa Newstart kuwa wameondoka) ikiwa tulipaswa kujenga jengola ziada ama la.

Mkutano wa maombi ulifanyika ukiwa na zaidi ya watu 20. Baada ya kushiriki katika maombi kila mmoja alimuomba Mungu kimya kimya akimuuliza ikiwa wanapaswa kujenga jengo au la. Majibu kwa kila mtu kutoka kwa Mungu yalishirikishwa kwa wengine kama ifuatavyo: Katika kipande cha karatasi walipaswa kuandika “+” kama walipaswa kujenga, walipaswa kuandika “–” kama hawakupaswa kujenga, walipaswa kuandika “o” kama hawakuwa na majibu na walipaswa kuandika “?” pamoja na alama nyingine ikiwa hawakuwa na uhakika wa jibu. Matokeo yalikuwa ni ishara ya uongozi wa Mungu wa ajabu: Kulikuwepo na “+”¹⁰⁶ (4 kati ya hizi pamoja na “+?”), 6 “o” na 4 vipande vyta karatasi ambavyo havikuandikwa kitu. (Pia kulikuwepo na majibu 2, ambayo hayakuelewaka na hayakuhesabiwa. Kwa hiyo uongozi wa Mungu ulikuwa dhahiri kwamba tulipaswa kujenga. Ninashawishika kwamba tutatafuta moja kwa moja ushauri wa Mungu zaidi na zaidi katika siku za mwisho.

Yoeli 2:28-29 huonyesha hili. E. G. White hutoa ufanuzi ufuatao: “Ni lazima kila mtu amsikie akiongea moyoni. Pindi kila sauti nyingine inaharakisha, na katika utulivu tunamngoea Yeye, ukimya wa nafsi hufanya sauti ya Mungu isikike zaidi. Anatusihi, ‘Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu.’” Zaburi 46:10¹⁰⁶

FEDHA

Kuna tofauti gani iliyopo kati ya Wakristo wa tabia ya mwilini na wale wa tabia ya rohoni kuhusiana na kujipatia na kutumia pesa? Je tunajiona wenyewe kama wamiliki wa mali zetu au kama mawakili wa Mungu? “Kupenda pesa na kujionyesha kumeufanya ulimwengu huu kuwa pango la wezi na wanyang’anyi. Maandiko huelezea kuwa tamaa na unyanyasaji vitashamiri kabla tu ya ujio wa Kristo mara ya pili.”¹⁰⁷

¹⁰⁶ E. G. White, *The Desire of Ages* (1898), uk. 363.3

¹⁰⁷ E. G. White, *Prophet and Kings* (1917), uk. 651.1

MALAIKA WA MUNGU HULINDA WATU WANAOOMCHA MUNGU

Malaika wa Mungu huwalinda watu wanaocha Mungu. "Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa." (Zaburi 34:7). "Malaika mlinzi amewekwa kwa kila mfuasi wa Kristo. Hawa walinzi wa mbinguni huwalinda wenye haki dhidi ya nguvu za waovu."¹⁰⁸ – Inapozungumzia kuhusu watu wanaomcha Mungu, wafuasi wa Kristo na wenye haki kuwa chini ya ulinzi wa Mungu, je hili humaanisha kwamba ni kwa kila mtu anayejiona kama Mkristo? Je hii humaanisha na wale ambao hawajayatoa kikamilifu maisha yao kwa Mungu? Ni kweli kwa watoto wa Mungu, kwa sababu Yesu anasema katika Mathayo 18:10: "Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni." Daudi, ambaye aliyakabidhi kabisa maisha yake kwaMungu, alifahamu kwamba hakuwa na sababu yoyote ya kuogopa. Alisema: "Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, Nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, Nimhofu nani?"(Zaburi 27:1 NKJV)

(Ninapendekeza kwamba usome katika kitabu cha *The Great Controversy* sura ya 31 sehemu inayohusu "The ministry of the good angel" (huduma ya malaika watakatifu). Hii ni furaha kubwa kwa kila mtoto wa Mungu.)

HITIMISHO

Tumepitia sehemu chache tu. Bado yapo maeneo mengi ya maisha na imani ambayo yangeweza kuongezwa. Katika mambo hayo yafuatayo ni kweli:

Tunapozipitia tofauti sasa, basi hakuna hata eneo moja ambalo halina faida kubwa kupitia maisha pamoja na Roho Mtakatifu. Kinyume chake, hakuna eneo hata moja ambalo hatuna hasara kubwa kwa maisha pasipo Roho Mtakatifu. Je hili halipaswi kuwa motisha kubwa kwetu katika kutoa maisha yetu kila siku kwa Mungu na kuomba kujazwa Roho Mtakatifu?

"Miaka kadhaa iliyopita ndege aina ya Boeing 707 ilipaa kutoka uwanja wa ndege wa Tokyo ikielekea London. Ilipaa vizuri. Anga halikuwa na mawingu na jua lilikuwa linawaka. Baada ya muda mfupi abiria waliweza kuona Mlima maarufu wa Fuji ulioko Japan. Ghafla rubani akapatá wazo la kuuzunguka mlima ili kwamba abiria waweze kufurahia mandhari hii nadra sana.

¹⁰⁸ E. G. White, *The Great Controversy*, (1911), uk. 512.2

Aliiacha njia rasmi ya ndege na kuhamia kwenye mfumo wa kuona kwa macho kule aendako “visual flight” [kanuni za usafiri wa anga zinazomruhusu rubani kuendesha ndege katika hali ya hewa isyo na kizuizi cha mawingu au kitu chochote na yenye kumruhusu kuona mahali anapokwenda]. Wakati akiwa katika mfumo huu wa “visual flight” rubani aliacha kufuata waongozaji wa ndege chini na akategemea kabisa kile alichokuwa akikiona. Rubani aliona mlima karibu yake kwa chini. Altimita [chombo cha kupimia urefu juu ya usawa wa bahari] ilionyesha mita 4,000. Kile ambacho hakukiona ni mawimbi na dhoruba ya upepo, ambayo iliuzunguka Mlima Fuji. Ndege ile ya Boeing 707 haikuweza kushindana na upepo. Ndege ilivunjika ikiwa angani, ikaanguka na abiria wote wakafa”¹⁰⁹

Mkristo wa tabia ya mwilini huishi katika hali ambayo haoni wala kuonekena “visual flight mode”. Hufanya maamuzi yote ye ye mwenyewe. Pamoja na nia nzuri aliyo nayo ataanguka. Mkristo wa tabia ya rohoni huishi kupitia Roho Mtakatifu katika mahusiano ya upendo na yenye tumaini pamoja na Bwana Wake, ambaye humuongoza salama mpaka mwisho wa safari

Ombi: Baba wa mbinguni, asante kwamba kukaa kwa Yesu ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu huleta tofauti chanya kiasi hicho ndani yetu na katika kazi zetu. Naomba ufungue macho yangu zaidi ili kutambua kazi ya Roho Mtakatifu. Nipatie utimilifu huu wa maisha kupitia Yeye, ambao Yesu anataka kutupatia. Naomba unisaidie kutambua suluhisho la kutatua tatizo hili katika sura inayofuata na kulifanyia kazi. Asante. Amina.

¹⁰⁹ Kalenderzettel February 17, 1979 by Reinhard Petrik

UFUNGUO KWA UZOEFU WA UTENDAJI

Ninawezaje kutekeleza na kupata uzoefu wa jibu la Mungu kwangu? Ninapaswa kuomba kwa namna gani ili niwe na uhakika wa kuiazwa na Roho Mtakatifu?

MAOMBI NA KUJAZWA NA ROHO MATAKATIFU

Ni muhimu kwamba tuendelee na safari hii kwa imani na kwamba tunaomba kwa imani kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Hilo humaanisha kwamba baada ya kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu tunahitaji kutumaini na kuwa na uhakika kwamba Bwana amejibu maombi yetu na kwamba tayari ametupatia Roho Mtakatifu wakati tungali tunaomba.

Wagalatia 3:14 inasema: "...tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani." Tafsiri nyingine inasema "ili tupate kupokea ahadi ya Roho kwa kumwanini Kristo."

Mungu ametupatia msaada mkubwa ili tuweze kumtumaini kwa urahisi Baba yetu wa mbinguni. Tunaita "Kuomba kwa ahadi".

KUOMBA KWA AHADI

Kwanza, hapa kuna mfano mzuri: Hebu tuchukulie kwamba mtoto wangu hafanyi vizuri katika somo la Kifaransa shulenii. Ninataka kumtia moyo mtoto wangu asome Kifaransa kwa bidii. Ninamuahidi kwamba kama atapata alama nzuri katika ripoti yake nitampa \$20. Mtoto anaanza kusoma kwa bidii. Pia ninamsaidia katika somo la Kifaransa na kweli anapata alama nzuri. Nini kitatokea sasa?

Wakati mtoto anapokuja nyumbani kutoka shule na kupita mlango wa mbele akiita kwa sauti kubwa: "Baba, \$20!" Kwa nini ana uhakika kiasi hicho kwamba atapata \$20? Kwa sababu ahadi ilitolewa na ametimiza masharti. Kwa kweli, hili ni jambo la kawaida kwa watu wengi leo.

Lakini inawezekana kwa wakati ule sina \$20. Je inawezekana kwamba Mungu hana kile kitu alichoahidi? Haiwezekani!

Au yawezezana kwamba nimefuta ahadi yangu na kusema "Nimesoma kitabu kuhusu elimu kwamba haipaswi kuwatia moyo watoto kusoma kwa kutumia pesa. Hivyo siwezi kukupatia \$20." Je Mungu hubadilisha mawazo yake baadaye? Haiwezekani!

Tunaweza kuona kwamba tunapokuwa na ahadi kutoka kwa Mungu nasi tumetimiza masharti, basi kuna uwezekano mmoja tu- kwamba tunaipokea ahadi.

Kupitia ahadi za Mungu anataka kututia moyo kwenda katika uelekeo fulani – kwa mfano kupokea Roho Mtakatifu, ambaye hutupatia nguvu ya Mungu maishani mwetu. Anataka kufanya iwe rahisi kwetu kumtumaini. Kutumaini ndicho kiini cha imani.

Sasa tunataka kusoma baadhi ya mafungu muhimu ya Bibilia katika 1 Yohana 5:14-15 juu ya kuomba kwa ahadi:

"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake atusikia."

Mungu hutoa ahadi ya jumla kwamba anajibu maombi ambayo yanapatana na mapenzi yake. Mapenzi ya Mungu yameelezwu katika amri na ahadi. Tunaweza kuzitegemea [ahadi] katika maombi yetu. Kisha aya ya 15 inasema:

"Na kama tukijua ya kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba."

Tafsiri nyingine (NIRV) inasema:

"Kama twajua kwamba Mungu asikia kile tuombacho, twajua kwamba tumekipokea."

Hiyo humaanisha nini? Maombi yetu kulingana na mapenzi ya Mungu hujibiwa **wakati ule ule tunapoyapeleka kwa Mungu**. Lakini kihisia huwa hatutambui chochote. Maombi yetu hujibiwa kwa imani, si kwa hisia zetu. Hisia zitakuja baadaye.

Kwa kuomba na watu walioathirika na uraibu wa nikotini [sigara, n.k.] na pombe nimejifunza yafuatayo: Wakati wanapoomba kwa ajili ya kupata uhuru [kutoka kwenye utumiaji wa madawa] hawaoni chochote. Wanapokea majibu kwa imani. Lakini masaa machache baadaye wanatambua kwamba hawana tamaa na tumbaku au pombe tena. Kwa wakati huu wamepokea jibu la hakika kwa ombi lao.

Yesu alisema katika Marko 11:24: “*Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea nayo yatakuwa yenu.*”

E. G. White alisema: “Hatuhitaji kutazama uthibitisho wa nje wa mbaraka. Karama imo ndani ya ahadi, na tunaweza kuendelea na kazi zetu tukiwa na uhakika kwamba kile Mungu alichoahidi anaweza kutenda, na kwamba **karama, ambayo tayari tunayo, itaonekana tutakapokuwa tunaihitaji zaidi.**”¹¹⁰

Hivyo hatupaswi kutafuta uthibitisho wa nje. Hapa hakika inamaanisha kutafuta uzoefu wa kihisia. Roger J. Morneau alisema: “Roho [mapepo] wangehimiza watu kusikiliza hisia zao badala ya neno la Kristo na manabii wake. Kwa hakika hakuna njia ambayo roho hizi chafu zingeweza kutawala maisha ya watu pasipo watu kutambua kile kilichokuwa kikiendelea.”¹¹¹

Kuomba kwa ahadi hufungua hazina ya Mungu kwa ajili yetu. Baba yetu mpendwa wa mbinguni hufungua akaunti isiyo na kikomo kwa ajili yetu. “(Wanafunzi) Wanaweza kutarajia mambo makubwa endapo wana imani katika ahadi zake.”¹¹²

MAKUNDI MAWILI YA AHADI

Wakati huo huo ni muhimu kutofautisha kwa umakini kati ya ahadi zilizomo ndani ya Biblia: “Ahadi za kiroho – kwa ajili ya msamaha wa dhambi, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, kwa ajili ya nguvu ya kutenda kazi yake – **zinapatikana wakati wowote** (Pia tazama Matendo 2:38-39). Lakini ahadi kwa ajili ya mibaraka ya kimwili, hata kwa ajili ya uhai wenyewe, hutolewa wakati fulani na huzuiliwa wakati mwингine, kadri Mungu kwa hekima yake anavyoona inafaa.”¹¹³

Mfano: Isaya. 43:2 NKJV “Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza.” Mungu aliiitimiza hii ahadi kwa namna ya

¹¹⁰ E. G. White, *Education* (1903), uk. 258.2

¹¹¹ Roger J. Morneau, *A Trip into the Supernatural*, Review and Herald 1982, uk. 43

¹¹² E. G. White, *The Desire of Ages*, (1898), uk. 668.1

¹¹³ Morris L. Venden, *95 Theses on Righteousness by Faith*, (Pacific Press 1987), uk. 60

ajabu kwa marafiki watatu katika tanuru la moto (Danieli 3). Lakini kwa upande mwengine, wanamatengenezo Hus na Jerome waluuawa kwa kuchomwa moto huko Constance. Tungeweza kusema kwamba maombi yao hayakujibiwa. Lakini hatahivyo, je hayakujibiwa katika namna ambayo hatujaizoea? Kwa nini? Mwandishi wa papa alielezea vifo ya wafia dini hawa kama ifuatavyo: "Wote walikuwa na akili ilio kamilifu saa yao ya mwisho ilipowadia. Walijiandaa kwa ajili ya moto kama vile walikuwa wanakwenda katika sherehe ya arusi. Hawakutoa kilio chochote cha maumivu. Wakati miale ya moto ilipoinuka, walianza kuimba nyimbo; na ni kwa nadra sana ukali wa moto ungeweza kusitisha uimbaji wao."¹¹⁴ Ikiwa watu fulani wanaungua, wanaweza tu kupiga kelele. Tabia yao huonyesha kwamba Mungu aliingilia kat, ila si katika namna ambayo ni rahisi kuelewaka kwetu. Hili hunionyesha kwamba ahadi za kimwili bado zina umuhimu kwa ajili yetu.

KUSHUKURU KWA JIBU

Sasa jambo jingine la muhimu: Wakati maombi yetu yanapokuwa yamejibiwa kwa muda tulioomba, basi yafaa kumshukuru Mungu kwa jibu la ombi linalofuata. **Shukrani zetu kwa wakati huu huonyesha imani yetu kwa Mungu** kwamba amejibu ombi letu na kwamba tunategemea litatimizwa tunapolihitaji zaidi. Baadhi ya waumini hugundua kitu fulani mara tu baada ya kuomba. Lakini kwa waumini wengi uzoefu wao ni sawa na ule wa Eliya: Bwana hakuwemo ndani ya upepo, wala tetemeko la nchi wala kwenye moto, bali katika sauti ndogo, ya tulivu (1 Wafalme 19:11-12). Huu pia ulikuwa uzoefu wangu.

Baada ya muda mrefu nilifikiri kwamba hakuna jambo lililokuwa limetokea. Kisha ghafla nilitambua kwamba mambo mengi yalikuwa yametokea ndani yangu pasipo mimi kutambua.

KUBADILI MTAZAMO WANGU

Hii humaanisha: **Ni muhimu kubadilisha mawazo yangu katika muda huu: "...bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu..."** (Warumi 12:2)

Sasa ni sawa kusema: Asante kwamba umejibu ombi langu. Asante kwa kunipatia tayari kile nilichoomba. Asante kwamba nitakipata katika muda muafaka.

¹¹⁴ E. G. White, *The Great Controversy*, (1911), uk. 109.3 Neander, "Kirchengeschichte", 6. Per., 2. Abschnitt, 2. Teil, §69; Hefele „Konziliengeschichte“ Bd. VI, S.209 f

Huku si kujitawala mwenyewe kwa werevu. Kwa kujitawala mwenyewe kwa werevu ninajaribu kujishawishi mwenyewe. Wakati ninapokuwa nimeomba kufuatana na ahadi, basi nina kigezo cha kimbingu kwa mtazamo wangu uliobadili, kwa sababu tayari kwa imani nimejibowi. Kwa hiyo, ikiwa sitabadilisha mawazo yangu, basi ninamuonyesha Mungu kwamba simwamini, bali ninahisi kuelekezwa. Kwa tabia hii ninamfanya Mungu kuwa mwongo na hivyo sitapokea kitu chochote.

Pia ni muhimu kwamba nitende kulingana na ninavyoamini, hata wakati ambapo sioni ishra yoyote. Wakati wote Mungu hufungamanisha ulazima wa kuamini. Anataka tumtumaini. Fikiria kuhusu kuvuka Mto Yordani. Makuhani kwanza walipaswa kuingia majini na kisha maji yaligawanyika. Naamani alipaswa kujichovya ndani ya maji mara saba kabla hajaponywa.

Huenda unasema: "Siwezi kufanya hivyo. Siwezi hata kufikiria kufanya hivyo." Tafadhalii kumbuka kwamba yapo mambo mengi tusiyoweza kuyaelezea. Mpaka leo hii, hatufahamu umeme ni nini, japokuwa sote tunautumia. Mpaka leo, hatufahamu jinsi watoto wanavyojifunza kuzungumza. Lakini wote wanajifunza kuzungumza. "Katika ulimwengu wa asili wakati wote tumezungukwa na maajabu kupita ufahamu wetu. Je tunapaswa kushangaa kukuta pia katika ulimwengu waroho siri ambazo hatuwezi kuzielezea?"¹¹⁵

Hebu tufikirie kuhusu Mithali 3:5-6: "*Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe, Katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako.*" Hapa tunapata masharti yaliyo wazi kutoka kwa Mungu kwa ajili ya ahadi ya kunyoosha mapito yetu. Pia kila sharti ni amri. Ikiwa hatuna uhakika kwamba tumetimiza masharti, basi tunaweza kuomba kuwa na nia na uhakika kwamba Bwana atatujibu haraka. . "... lakini ikiwa 'uko tayari kufanya kuwa tayari', Mungu ataikamilisha kazi kwa ajili yako"¹¹⁶

Jambo dogo linaloweza kusaidia: Je tunafahamu kile tunachokifanya, wakati tunapokuwa tumeomba kwa ahadi ya Mungu, na kutimiza masharti na kisha kuwa na shaka kujibowi? Tunamfanya Mungu kuwa mwongo. Kwa namna yoyote ile hatutaki kufanya hivyo. Kwa hiyo, omba: Bwana, Ninaamini, nisaidie kutokuamini kwangu. Kisha amini!

Upo ushauri wa thamani juu ya kuomba kwa ahadi katika sura ya "Imani na Maombi" katika kitabu cha "Education" cha E. G. White.

¹¹⁵ E. G. White, *Education* (1903), uk. 170.1

¹¹⁶ E. G. White, *Thoughts from the Mount of Blessing* (1896), uk. 142.1

KUOMBA KWA AJILI YA ROHO MTAKATIFU

Ninafikiri tuna sifa bora kabisa kwa ajili ya kuomba kujazwa na Roho Mtakatifu. Lakini hatupaswi kusahau kwamba haina uhusiano wowote na kumfanya Mungu awe tayari kufanya mapenzi yetu, bali kuamini katika ahadi zake na uaminifu wake.

Ahadi kwa ajili ya Kupokea Roho Mtakatifu

Bwana ametupatia ahadi za ajabu kwa ajili ya kupokea Roho Mtakatifu:

Luka 11:13: "Basi ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vilivyo vyema, je Baba aliye mbinguni hataziadi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao!"

Je hapa Baba yetu wa mbinguni hajafanya ahadi ambayo ni lazima aitimize? Masharti katika ahadi hii ya ajabu ni: omba! Lakini bado Yesu hamaanishi uombe mara moja, bali kuomba daima.

Hata hivyo, ni muhimu sana kuelewa mkutadha hapa. Tunapaswa pia kusoma mafungu mengine, ambayo huzungumzia jambo hili, kwa mfano:

Matendo 5:32: "Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtio."

Sharti hapa ni: **utii!** Tunaweza kuona hapa kwamba hatuwezi kujenga hoja yetu kwa kutegemea fungu moja: pia tunapaswa kufikiria muktadha wa ahadi. Haihusiani na kuwa mtiifu mara moja kwa jambo ambalo linatufurahisha. Bali, inahusu kumtii Yeye: mkombozi wetu wa ajabu na rafiki. Utii huleta furaha. Omba kila asubuhi kwa ajili ya moyo mtiifu. Omba kwamba Bwana akufanye kuwa tayari kutenda kila kitu anachotaka na atakusaidia kukitimiza. Hii hutengeneza mazingira mazuri ya kupokea.

Yohana 7:37: "Mtu akiona akiona kiu, na aje kwangu anywe."

Hapa inahusiana na **nia** kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Ikiwa hauna nia yoyote, au unafikiri unayo kidogo sana, basi unawenza kuomba kwa ajili ya kuwa na nia. Ni sharti kulingana na mapenzi ya Mungu, ambalo litajibiwa

mara moja. Tunapomwomba Baba yetu wa ajabu atatuumbia "nia na ufanisi." Pia tunaweza kuomba kwa ajili ya nia kwa ajili ya mahusiano ya karibu pamoja na Mungu, kumpenda Mungu kwa miyo yetu yote, kumtumikia kwa furaha, kuwa na nia kubwa kwa ajili ya Yesu na kuja kwake upesi na kuwa pamoja katika ufalme wa Mungu, nia ya kusoma neno la Mungu na kujifunza kutoka katika neno, na vile vile kusaidia na kuandaliwa kusaidia waliopotea.

Yohana 7: 38-39: "*Aniaminiye mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye.*"

Hapa kigezo ni: **imani!** Tunaona hapa kwamba imani yetu katika Yesu Kristo, tumaini letu katika Mungu, ni sharti muhimu katika kupokea Roho Mtakatifu. Lakini tunapoomba kulingana na ahadi, basi kuamini ni rahisi.

Wagalatia 5:16: "*Basi nasema, enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.*"

Hapa kwa hakika tunayo ahadi, ambayo imeelezwa kama agizo. Mungu anapotaka nienende katika Roho, basi hiyo humaanisha bayana kwamba anataka kunijaza na Roho Mtakatifu. Na anatuonyesha hapa kwamba tunapoajaza na Roho Mtakatifu, basi hatutawaliwi na tamaa za miili yetu tena. Roho Mtakatifu huvunja nguvu za dhambi ndani yetu (Warumi 8:1-17, hasa aya ya 2). Kupitia Roho Mtakatifu "*matendo ya miili yetu*" hufishwa (Warumi 8:13). Fikiria juu ya Paulo, ambaye alisema juu yake mwenyewe: "*Ninakufa kila siku.*" Ni jambo la thamani sana kutokuwa chini ya matendo ya mwili (Wagalatia 5:18-21), bali kukuza matunda ya Roho (Wagalatia 5:22).

Tunaweza kulinganisha dhambi kushindwa kutawala maisha yetu na mkusanyiko wa darubini. Ili vumbi lisiweze kuingia ndani ya lensi chumba kinapaswa kuwa na presha kubwa. Hii humaanisha kwamba hewa hutoka nje mlango unapofunguliwa. Hakuna vumbi linaloweza kuingia. Kwa namna hiyo hiyo, tunapokuwa tumejazwa na Roho Mtakatifu, "*wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.*" (Maelezo ya ziada juu ya mada hii yapo katika sehemu inayozungumia: "*Je mtu anaweza kuendelea kuwa wa rohoni?*" mwisho wa sura hii)

Waefeso 3:16-17,19: "*Awajalieni, kwa kadri ya utukufu wa wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani, Kristo akae miyoji mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo...mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.*"

Huenda hatuoni nguvu yoyote kwa muda mrefu. Inaweza ikawa ni katika hali ya asili. Wakati wa kipupwe miti haina majani na wakati wa majira ya kuchipua ni ya kijani. Kuna nguvu kubwa ifanyayo kazi katika kuirejesha. Lakini hatuwezi kuiona au kuisikia. Lakini basi tunaona matokeo. Hivyo ndivyo iliyokuwa kwangu. Ninamshukuru Mungu kwani hunipatia nguvu nyingi.

Mfano mwingine: Tumekuwa tukifahamu kwa miongo kadhaa kwamba tuna mawimbi ya umeme ndani ya miili yetu. Yapo humo. Lakini hatuyaoni.

Waefeso. 5:18: “... *bali mjazwe Roho*” au “*muendelee kila siku kujazwa na Roho wakati wote*”.¹¹⁷

Matendos 1:8: “*BLakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; manyi mtakuwa mashahidi wangu... ...*”

Wanafunzi walikuwa na kazi ya kusubiri mpaka nguvu ije. Hawakusubiri bila kufanya kitu. “Waliomba kwa dhati kwa ajili ya kuwezeshwa kukutana na watu katika maisha yao ya kila siku na kuwa na maneno sahihi kuongoza wadhambi kwa Kristo. Waliweka kando tofauti zao na matamano yao yote.”¹¹⁸ Tunaweza kuomba kwa ahadi hii.

HAKUNA MATOKEO CHANYA ...?

“Kijana mdogo alikuwa anatafuta ushauri, kwa kuwa alitaka kujazwa na Roho Mtakatifu. Alikuwa akihangainka sana. Mchungaji alimuuliza: ‘umewahi kusalimisha kikamilifu utashi wako kwa Mungu?’ Sidhani kama nimefanya hivyo.” Vyema, mchungaji alisema, ‘basi haitasaidia kuomba [kujazwa na Roho Mtakatifu], mpaka utakapokuwa umesalimisha kabisa utashi wako kwa Mungu. Je hutosalimisha utashi wako kwa Mungu sasa?’ Siwezi’alijibu. ‘Je uko tayari Mungu afanye hivyo kwa ajili yako?’ Ndiyo’ alijibu. ‘Basi muombe afanye hivyo.’ Akaoomba: ‘Ee Mungu, niondoe kabisa kwenye utashi wangu. Nifanye nijisalimishe kikamilifu kwa mapenzi yako. Ondo utashi [mapenzi] yangu kwa ajili yangu. Ninaomba katika jina la Yesu.’ Kisha mchungaji aksauliza: ‘Je imetokea?’ Lazima itakuwa imetokea’, alisema. ‘Nilimuomba Mungu kitu fulani kulingana na mapenzi yake na ninajua kwamba nimepokea kile nilichoomba (1 Yohana 5:14-15). Ndiyo, imetokea – mapenzi yangu yameondolewa.’ Kisha mchungaji akasema:

¹¹⁷ Johannes Mager, *Auf den Spuren des Heiligen Geistes*, (Lüneburg, 1999), Seite 101

¹¹⁸ *Acts of the Apostles*, 37.1. egwwritings.org

‘Sasa omba kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu[kujazwa na Roho Mtakatifu].’ Akaomba: ‘Ee Mungu, nibatize sasa kwa Roho wako Mtakatifu. Ninaomba katika jina la Yesu.’Na ikatokea mara aliposalimisha mapenzi yake.”¹¹⁹

TOFAUTI KUBWA KABLA NA BAADA

Japokuwa nilikuwa ninafahamu kuomba kwa ahadi kwa muda mrefu na kufanya hivyo katika nyakati maalum na kuona majibu ya ajabu katika maombi, nilifikiri kwa miaka mingi kwamba ilikuwa inatosha ikiwa ningeomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu katika maombi pasipo kutegemea ahadi maalum. Ninajua kwamba wengi wamekuwa na mtazamo kama huo. Sitaki kusema kwamba hili ni kosa. Lakini ninapoangalia nyuma katika uzoefu wangu binafsi, basi ninaweza tu kujutia kwamba niliomba kwa namna hii pasipo ahadi yoyote.Kwa miaka kadhaa sasa nimekuwa nikiomba kila siku kwa ahadi kwa ajili ya Roho Mtakatifu, ili kwamba baada ya kumaliza ombi langu ninao uhakika kwamba sasa nimejazwa na Roho Mtakatifu. Kupitia uzoefu wa Oktoba 28, 2011, nilitambua tofauti kubwa maishani mwangu: kabla na baada.

Tangu nimeanza kuomba kwa ahadi mahusiano yangu na Mungu yamekuwa ya ukaribu sana na Yesu yuko karibu na mimi na amekuwa muhimu sana kwangu. Hii si hisia binafsi tu; ninaweza kuihusianisha na mambo yafuatayo:

- ▶ Wakati ninapokuwa nikisoma Biblia mara nyingi ninakuwa na uelewa mpya na unaotia moyo.
- ▶ Katika mapambano na majoribu ninaweza kubakia mshindi.
- ▶ Muda wangu wa maombi umekuwa wa thamani sana kwangu na hunipatia furaha sana.
- ▶ Mungu hujibu mambo mengi ninayomuomba.
- ▶ Nina furaha kubwa na “*ujasiri*” (Matendo 4:31) kuwaambia wengine habari za Yesu.
- ▶ Nimekuwa na mahusiano mazuri zaidi na marafiki zangu.
- ▶ Ninaishi kwa furaha kupitia neema ya Mungu na ninahisi kuwa salama mikononi mwake.
- ▶ Katika wakati mgumu Bwana alinisaidia kwa namna ya ajabu na aliniimarisha ndani [ya moyo wangu].
- ▶ Nimetambua ni karama zipi za roho ambazo Bwana amenipatia.

¹¹⁹ Reuben A. Torrey, *Der Heilige Geist – Sein Wesen und Wirken* (Frankfurt, 1966), uk. 150

- ▶ Ukosooji umekoma. Ninaposikia watu wengine wakikosoa ninahisi kukosa amani.

Badiliko lilitokea kimya kimya. Kwa mara ya kwanza nililigundua nilipotumia muda fulani kila siku kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu kwa kufuata ahadi za kibiblia. Tangu wakati huo ninaona aina tofauti ya Ukristo. Hapo mwanzo maisha yangu pamoja na Mungu yalikuwa ya kuhangaika na magumu; sasa ninapata furaha na nguvu.

Ninasikitika kwa hasara katika maisha yangu binafsi kwa sababu ya ukosefu wa Roho Mtakatifu, kwa hasara katika ndoa yangu na familia na kwa hasara katika makanisa ambako nilitumika kama mchungaji. Nilipotambua hili nilimuomba Bwana msamaha.

Bahati mbaya ni kweli kwamba katika eneo hili hatuwezi kuwaongoza watu wengine mbali kuliko tulivyo sisi wenyewe. Tunapaswa pia kukumbuka kwamba mapungufu binafsi ya kila mtu mmoja mmoja ndani ya familia na ndani ya kanisa huongezeka au kuzidi.

Li kwamba watu wengine wasiweze kulalamika kwa kosa hilo hilo maishani mwao, ninataka kuongeza maelezo machache.

Katika 2 Petro 1:3-4 inasema kwamba kupitia mahusiano ya karibu na Yesu tunaweza “*tena kwa hayo ...kupitia ahadi kubwa mno za thamani ...mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu*”.

Hii pia humaanisha kwamba Roho Mtakatifu ametolewa kwangu kupitia ahadi. Unaweza kulinganisha ahadi na cheki ya benki. Tunapoonyesha cheki iliyosainiwa kutoka kwa mwenye akaunti, tunaweza kuchukua pesa kutoka kwenye akaunti ya mtu mwingine. Kama watoto wa Mungu (Yohana 1:12) tunaweza kila siku kutoa kwa kutumia cheki (ahadi) iliyosainiwa na Yesu. Haitasaidia chochote kuonyesha cheki zetu wenyewe, hata kama tutakuwa na cheki iliyotengenezwa na mchoraji. Tunahitaji cheki zilizosainiwa na mwenye akaunti.

Pia kuna sababu nytingine, ambayo inaweza kututia moyo kuomba kwa ahadi. Kuna nguvu katika neno la Mungu. Kwa nini Yesu aliomba msalabani mara tatu kwa maneno kutoka Zaburi? Kwa nini alijibu na kumshinda Shetani kwa mafungu ya Biblia wakati wa majoribu ya Shetani jangwani? (Mathayo 4:4,7,10) Alisema: “*Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*”

Yesu, Muumbaji, alijua kwamba kuna nguvu katika neno la Mungu, “Katika kila amri na katika kila ahadi ya neno la Mungu ni nguvu, ya maisha ya Mungu,

ambayo kwayo amri inaweza kutimizwa na ahadi kutambuliwa.”¹²⁰ Maneno mazuri kiasi gani! Nguvu ya Mungu na maisha yake yapo ndani ya kila ahadi. Tunapoomba kwa ahadi tunatumia neno la Mungu katika maombi yetu. Inasema kuhusu neno la Mungu: “*ndivyo litakayokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirudia bure, ...*” (Isaya 55:11 NKJV)

Ninapanga kuomba kwa Roho Mtakatifu kwa ahadi pekee. Ninapoomba kwa ahadi ninajua kwamba baada ya kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu kwamba nimempokea kulingana na ahadi za neno la Mungu katika 1 Yohana 5:15 NKJV: “*Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*” Ninapoomba pasipo ahadi, basi natumaini kwamba ombi langu litajibiwa. Ni vizuri kuwa na muda wa maombi kama huu na kushuhudia siku yenye Baraka, kuliko kulalamika kuhusu kushindwa jioni.

Nilipokea ujumbe wa barua pepe, ambayo uliandikwa kwa furaha kubwa: “Kamwe sijawahi kufikiri kuwa kungeleta tofauti kubwa endapo ningeomba kwa uongozi wa Mungu siku nzima kwa ‘maneno yangu mwenyewe’au ikiwa ningeomba kwa ahadi kutoka kwenye Biblia! Ahadi wakati wote zimekuwa za muhimu sana kwangu. Wakati wote nimekuwa nikiziamini, lakini nimeshindwa kuzidai kila siku. Maisha yangu pamoja na Yesu yamekuwa ya kina, yenye furaha zaidi, ya imani na ya utulivu. Ninamshukuru Mungu kwa hili.”¹²¹

Kwa sababu hii, nimeamua kushirikisha mfano wa ombi kwa ajili ya Roho Mtakatifu kwa kutumia ahadi. Kwa kawaida, linaweza kufupishwa. Ni muhimu kwamba tujifunze kuomba sisi wenyewe moja kwa moja kutoka katika neno la Mungu. Lakini jambo la muhimu ni kwamba imani yetu inaimarishwa kwa ahadi katika namna ambayo baada ya kuomba tuna uhakika kwamba tumepokea Roho Mtakatifu. Tunapokea Roho Mtakatifu wakati tunapoamini juu ya kile tulichoomba

¹²⁰ E. G. White, *Christ's Object Lessons* (1900), uk. 38.2

¹²¹ Email to H. Haubeil C.S.

OMBI LA MFANO PAMOJA NA AHADI KWA AJILI YA KUFANYWA UPYA KILA SIKU NA ROHO MTAKATIFU

Baba wa mbinguni, Ninakuja kwako katika jina la Yesu Mwokozi wetu. Umesema: **Nipe moyo wako.** (Mithali 23:26) Ninataka kufanya hivyo sasa kwa kujitoa mwenyewe kwako leo kama nilivyo na vyote nilivyo navyo.¹²² Asante kwa kuwa tayari umekwisha jibu ombi hili kulingana na mapenzi yako, kwa sababu neno lako linasema kama tukiomba kulingana na neno lako tunajua kwamba tayari tumelipokea (1 Yohana 5:15). Na pia umesema kwamba ye yote ajaye kwako hutamtupa nje kamwe. (Yohana 6:37).

Yesu alisema: “Basi, ikiwa ninyi mlion waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, jel! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao **wamwombao?**” (Luka 11:13)

Zaidiya hayo pia ulisema kuwa ungewapa Roho Mtakatifu wale, wakuaminio (Yohana 7:38-39), wale wakutioo (Matendo 5:32), wale wanaojazwa na Roho (Waefeso 5:18) na **wanaoenenda katika Roho** (Wagalatia 5:16). Hii ndiyo nia yangu. Naomba utimize hili ndani yangu. Kwa sababu hii Baba ninakuomba kwa dharti unipatie Roho Mtakatifu leo. Kwa kuwa ni ombi sawasawa na mapenzi yako, ninakushukuru kwa kuwa umenipatia Roho Mtakatifu sasa (1 Yohana 5:15). Ninashukuru kwamba pia nimepokea upendo wako wa kimbingu, maana neno lako linasema: **“Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika miyo yetu na Roho Mtakatifu.”** (Warumi 5:5; Waefeso 3:17) Ninataka kusema pamoja na mtunga zaburi: **“Wewe, Bwana, nguvu zangu, nakupenda sana.”** (Zaburi 18:1) Ninashukuru kwamba ninaweza kuwapenda binadamu wenzangu kwa upendo wako.

Ninashukuru kwamba kuititia Roho Mtakatifu nguvu ya dhambi imevunjwa ndani yangu (Warumi 8:13; Wagalatia 5:16). Naomba unilinde na unikoe leo kutoka dhambini na kutoka ulimwenguni, nipatie ulinzi dhidi ya malaika waovu, niokoe dhidi ya majaribu na pale inapowezekana nishike na unikoe kutoka kwenye asili yangu ya uovu. (1 Yohana 5:18)

Nakuomba pia unisaidie kuwa shahidi wako katika maneno na matendo (Matendo 1:8). Ninakusifu kwa kusikia ombi langu. Amina.

¹²² “Wale watakaokuwa watendakazi pamoja na Kristo, wale tu watakaosema, Bwana, vyote nilivyo navyo, na hivi nilivyo, ni vyako, watakaokubaliwa kama wana na binti za Mungu” E. G. White, The Desire of Ages (1898), uk. 523.1

Yesu mwenyewe anataka kuishi ndani yetu kuitia Roho Mtakatifu (i Yohana 3:24; Yohana 14:23). E. G. White alisema: “Mvuto wa Roho Mtakatifu ni maisha ya Kristo ndani ya nafsi.”¹²³ Nguvu iliyombadilisha Petro, Paulo na watu wengine wengi pia inapatikana kwetu. Pia hutupatia “awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanya imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.” (Waefeso 3:16)

Kujazwa na Roho Mtakatifu ni kiiini cha maisha ya imani na furaha, nguvu, upendo na ushindi dhidi ya dhambi. “...walakin aliipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru.”² Wakorintho 3:17

Kwenye ujumbe niliopokea unasema yafuatayo: “Washiriki wengi wa kanisa kila siku huomba ombi lilipendekezwa wakiwa watu wawili. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita nimekuwa nikiomba ombi hilo pamoja na mke wangu. Si tu kwamba kila kitu kinaendelea visuri kwa mambo binafsi, bali pia nyumbani, katika mahusiano, katika ndoa, kiroho na kanisani—si kwa namna inayosababisha vurugu kubwa, bali hutokea kwa namna tulivu; ya kawaida. Tunastaajabu na kuona hili kama udhihirisho wa Mungu, ambao unaweza kufanya maisha kuwa rahisi kwa namna fulani, kwa kuwa tunahisi ukaribu wa Mungu zaidi na zaidi.”¹²⁴

JE MTU ANAWEZA KUBAKI KUWA WA KIROHO?

Ndiyo! Wakati tunapokataa kuruhusu tabia ya kutokuamini kujengeka na tunapumua kiroho: “kutoa pumzi” kwa kukiri dhambi zetu na “kuvuta pumzi” kwa kuutumia upendo wa Mungu na msamaha na kufanya upya maombi yetu ya imani ya kujazwa na Roho Mtakatifu.¹²⁵

Ni sawa na uhusiano kwa watoto wetu. Wakati mtoto analipokuwa mkaidi, bado aliendelea kuwa mtoto wetu. Lakinitunahisi kuvurugika kwa uhusiano. Mtoto anaweza asitutazamemachoni. Mvurugiko huu husahihishwa kwa kuungama.

Lakini kwa kawaida mtu anaweza kuwa mtu wa tabia ya mwilini kwa mara nyingine tena katika kipindi kirefu. Biblia haizungumzii kuhusu “ukishaokolewa mara moja, unaokolewa daima”. Hali yetu ya dhambi bado ipo. “Hakuna hata mmoja mionganii mwa mitume au manabii aliyewahi kudai kutokuwa na dhambi.”¹²⁶

¹²³ Editor Francis D. Nichol, *Adventist Bible Commentary* Vol. 6 (Hagerstown, 1980), uk. 1112

¹²⁴ Email to Helmut Haubeil: E.S.

¹²⁵ Helmut Haubeil & Gerhard Padderatz, *Gott, Geld & Glaube* (Eckental, 2009), uk. 97

¹²⁶ E. G. White, *The Acts of the Apostles* (1911), uk. 561.1

Lakini kupitia maisha pamoja na Roho Mtakatifu na pamoja na Yesu miyoni mwetu nguvu ya dhambi huvunjwa ili tuweze kuishi maisha ya Kikristo yenye furaha na ukamilifu. Haki yetu iko katika Yesu Kristo pekee. "... *aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi*" (1 Wakorintho:1:30). Mada hii muhimu itaelezewa kwa kina muda mfupi ujao

Ikiwa tumekuwa watu wa tabia ya mwilini kwa mara nyingine kwa kupuuza maisha ya kiroho kwa muda mrefu au kushindwa kupumua pumzi ya kiroho, basi tunaweza kufahamu kwamba mkombozi mwenye huruma anatusubiri.

Ni muhimu tufahamu njia ambayo kwayo tunaweza kufanywa upya na neema ya Mungu na kuishi maisha ya kiroho siku zote. Hakuna hata mtu mmoja anayepaswa kubakia mtu wa tabia ya mwilini.

Lakini kumbuka kama mtu mmoja na kwa ujumla kile ambacho Randy Maxwell alisema: "Je, tunadhani kwamba uamsho wa kanisa la Mungu kutoka karibu na kifo cha kiroho kunaweza kukamilika bila juhud?"¹²⁷

Uzima tele hapa [duniani] na uzima wa milele, wokovu wa watu wengi na shukrani zetu kwa kafara kuu ya Yesu unastahili juhud. Jambo la muhimu ni kukutana na Bwana wetu asubuhi kwa ajili ya kuabudu. Ni hapa ndipo hututia nguvu.

Tunasoma yafuatayo kuhusu mtume Yohana:

"Siku hadi siku moyo wake ulivutwa karibu na Kristo, mpaka alipokoma kujitazama nafsi yake mwenyewe kwa upendo wa Bwana wake. Tabia yake ya chuki na tamaa ya kutaka makuu ilisalimishwa chini ya nguvu ibadilishayo ya Kristo. Mvuto urejeshao wa Roho Mtakatifu uliumba upya moyo wake. Nguvu ya upendo wa Kristo ilileta badiliko la tabia. Haya ni matokeo ya uhakika ya umoja pamoja na Yesu. Wakati Kristo anapokaa moyoni, asili yote hubadilishwa."¹²⁸

"Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika sheria yako." (Zaburi 119:18) Asante kwa kuwa unaniongoza na ninaweza kusema: "*Naifurahia ahadi yako, Kama apataye mateka mengi.*" (Zaburi 119:162)

¹²⁷ Randy Maxwell, *If My People Pray* (Pacific Press, 1995), uk. 158

¹²⁸ E. G. White, *Steps to Christ* (1892), uk. 73.1

KUNA UZOEFU GANI ULIO MBELE YETU?

*Uzoefu binafsi, na vile vile uzoefu kutoka
makanisani, Konferensi na Unioni*

UZOEFU WA NDUGU

“Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita nimekuwa nikiomba kila siku kwa ajili ya kumwagwa Roho Mtakatifu maishani mwangu. Ombi langu ni kwamba Yesu hatimaye atakaa ndani yangu kwa wingi kila siku. Kuenenda kwangu na Mungu [katika kipindi chote hiki] kumekuwa kwa kushangaza. Tunda la Roho katika Wagalatia 5 limekuwa dhahiri zaidi maishani mwangu kwani huwa namuomba Yesu aishi ndani yangu, kufanya mapenzi yake ndani yangu na kunifanya upya kila siku kwa Roho Mtakatifu. Nina furaha kubwa katika kusoma Biblia, kuwaambia watu wengine habari za Kristo na nina shauku kubwa ya kuombea wengine; zaidi sana, mtindo wangu wa maisha umebadilika kabisa. Ninaona yote haya kama uthibitisho wa kumtafuta Mungu kila siku na ombi langu la kila siku kwa ajili ya Roho Mtakatifu.”C. H. anaelezea zaidi:

“Ninakupatia changamoto ya kuomba kila siku kujazwa na Roho Mtakatifu kwa wiki sita na uone nini hutokea.”

SIKU AROBAINI ZA MAOMBI HUKO SERBIA

“Mnamo Septemba 2010, tulitafsiri na kuchapa kitabu kiitwacho *40 Days: Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming*. Tulikisambaza kwa washiriki wa makanisa yote katika unioni yetu. Kisha tukaandaa mikutano ya maombi ya kila siku na kila juma katika kipindi cha siku 40 kilichofuata katika makanisa mahalia na katika nyumba za washiriki, ambapo watu walifunga na kuomba kwa ajili ya kujazwa upya kwa Roho Mtakatifu.

Kadri hili lilipokuwa linatoka, hali mpya kabisa ikaanza kujengeka katika mikutano ya kanisa mahalia. Washiriki waliokuwa wamerudi nyuma wakaanza kuwa na bidii zaidi na wakapenda zaidi kuwashudumia wengine. Wale ambao waligombana wao kwa wao kwa miaka mingi kwa mambo mbalimbali (na hata walikuwa wameacha kuzungumza!), wakapatana, ana kuanza kupanga mipango kwa ajili ya huduma za kijamii pamoja.

Kisha Oktoba 2010, katika Baraza la Mwaka, “the Revival & Reformation initiative” ikaanzishwa. Tuliipokea kwa furaha, na kuiona kama muendelezo wa kile ambacho Mungu alikuwa tayari amekianzisha katika unioni yetu.

Tumeona ushirika wa karibu, umoja wa hali ya juu na maelewano mazuri kati ya maofisa wa Unioni kama matokeo ya haraka ya mikutano hii ya maombi.”¹²⁹

SIKU 40 ZA MAOMBI HUKO ZURICH / SWITZERLAND

“Mchungaji wetu na mimi kwa wakati tofauti tulipeana kitabu ambacho yaliyomo ndani yake zilitusisimua. Kichwa cha habari kilikuwa: *40 Days: Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming* kilichoandikwa na Dennis Smith, Review and Herald Publishing Association. Kitabu hiki hakiwezi kusomwa na kisha kuwekwa kando tu. Yaliyomo ndani yake yalibadilisha maisha yangu

Kwa kuwa kanisa letu hapa Zurich-Wolfswinkel (lenye zaidi ya washiriki 100) lilitambua hitaji kubwa la uamsho na maombi, tulipanga Siku 40 za Maombi kwenye majira ya kipupwe ya mwaka 2011. Kitabu hicho kilitoa maelezo ya kina na ya thamani katika jambo hili na zaidi, siku 40 za ibada za kila siku.

Mada zilihusu kujazwa na Roho Mtakatifu, maombi, kuhubiri, maisha ya Yesu na ushirika wa kiroho.

Hivyo tukaanza Siku zetu 40 mnemo Oktoba 1, 2011 kwa matarajio na matumaini makubwa. Bahati nzuri, wengi wa washiriki wa kanisa walihusika. Wana kikundi cha maombi walikutana kila siku, ujumbe mfupi wa simu ulitumwa kila siku na watu waliomba kwa njia ya simu kila siku. Kundi moja lilikutana kila siku asubuhi saa 12:00 kwa ibada na maombi.

Siku zetu 40 ulikuwa ni uzoefu usiosahaulika. Mungu alijibu maombi yetu mengi, hasa kuhusiana na mfululizo wa masomo juu ya unabii wa Biblia, ambayo yalifanyika wakati huo huo. Masomo haya yalikuwa mbaraka mkubwa. Tulikuwa na wageni wengi na watu zo walijisajili kwa semina iliyofoata ya unabii. (Tathmini ya Machi 2013: Kati ya wageni 50-60 walifika, jambo ambalo halijawahi kutokea Zurich katika kipindi cha miaka zo.)

¹²⁹ M. Trajkovska, Southern European Union, Belgrade, quoted in www.revivalandreformation.org

Roho wa Mungu amefanya mabadiliko yanayoendelea ndani ya kanisa letu na ni furaha kuona jinsi makundi yetu machache yanavyoanza kukua na jinsi washiriki wa kanisa, ambao wanatamani kutoa mafundisho ya Biblia, hupata watu walio na shauku. Wale ambao walishiriki sasa wana hamu kubwa kwa ajili ya kuendeleza kazi ya Roho wa Mungu. Tunataka kumshukuru ye ye kwa miyo yetu yote na kumpatia utukufu.” Béatrice Egger, kutoka kanisa la Waadventista huko in ZurichWolfswinkel.

SIKU 40 ZA MAOMBI NA UINJILISTI HUKO COLOGNE / UJERUMANI

Mchungaji Joao Lotze ana asili Ujerumani na Brazil. Amefanya kazi kwa miaka 38 katika makanisa na hospitali huko Brazili, na vile vile katika unioni na Divisheni ya Amerika ya Kusini. Amestaafu mwezi Machi 2012. Yeye pamoja na mke wake walikubali kuja Cologne kama “His Hands Missionaries” na kufanya kazi katika makanisa yanayozungumza lugha ya Kireno na Kihispania.

“Tulianza na makundi madogo na kuwatia moyo washiriki wa kanisa kualika wageni. Kutokana na uzoefu wetu huko Brazil tulienesha Siku 40 za Maombi huko Cologne. Masomo yalipatikana kwa lugha ya Kireno.

Makanisa yaliyokuwa na washiriki wanaozungumza Kireno, Kihispania na Kijerumani kwa furaha walianza Siku 40 za Maombi. Kila siku tuliwaombea jamaa na marafiki 100. Majina ya watu hawa yaliyokuwa yameandikwa katika ubao mweusi wa matangazo kanisani. Hatukuwafahamisha watu hawa mpaka tulipofika siku ya 30 na ya 35 ya maombi kuwa tulikuwa tunawaombea na wakati huo huo kuwalika kwenye ibada maalum ya Sabato ya wageni. Watu 120 walikuja ibada maalum hii. Christian Badorre, mkurugenzi wa Huduma Binafsi wa Nordrhein-Westfalen, aliendesha ibada. Baadhi ya wageni walilia kwa furaha walipoona majina yao kwenye ubao.

Baada ya hapo, Antonio Goncalves, mwinjilisti kutoka Brazil, aliendesha mikutano ya uinjilisti kwa siku 15. Kila jioni alizungumza kwa saa 1.5 (akiwa na mtafsiri). Kichwa cha masomo hayo kilikuwa: ‘Let the Bible surprise you’ Ruhusu Biblia ikushangaze’. Mada zilihusu ujio wa mara ya pili wa Yesu, na vile vile mada kutoka Danieli na Ufunuo. Masomo na nyimbo vilitafsiriwa kutoka katika lugha ya Kireno kwenda katika lugha ya Kijerumani. Kulikuwa na kwaya ndogo na muziki mzuri kila jioni. Kila jioni ilifungwa na wito wa madhabahuni. Tunashukuru kwa matokeo mazuri. Washiriki wa kanisa waliomba kwa bidii, hasa kwa ajili ya watu waliojitoa kwenye Siku 40 za Maombi.

Kanisa letu lina uwezo wa kuchukua watu 80. Lakini zaidi ya watu 100 walikuja. Katika wikiendi kanisa lilija na katikati ya juma kulikuwepo na watu 60. Wageni 32 walihuduria kila siku. Hili liliongoza kwenye ubatizo wa watu 8 na watu 14 walijiunga na darasa la ubatizo. Mpaka kufikia mwisho wa mwaka watu 13 walibatizwa.

Tulikuwa na uzoefu wakushangaza. Ilikuwa vigumu kupata mtafsiri. Mwalimu wa Kikatoliki alijitolea kusaidia. Lakini hakuwa na uzoefu mkubwa wa Biblia. Baadaye tukaomba kwa ajili ya mtafsiri wa kiprotestanti. Mara tulipata kufahamu mwanamke mmoja katika mgahawa, ambaye alielezea kwamba anatafsiri kwa furaha kubwa kutoka katika lugha ya Kireno kwenda Kijerumani katika kanisa la Kipentekoste. Alikuwa mtafsiri wetu katika mfululizo wa masomo ya kiinjilisti na pia alibatizwa.

Maria, mtafsiri, aliuliza ikiwa angeweza kumwalika rafiki yake aje. Ni kiongozi wa kanisa dogo la Kikolombia huko Cologne lenye washiriki 13. Alikuja na kuleta washiriki kutoka kanisani kwake pamoja naye. Tangu hapo watu hawa wawili pia wamebatizwa. Elisabeth pamoja na familia yake sasa wanapokea masomo ya Biblia.

Uzoefu mwengine umeunganishwa na Kituo cha Hope Channel. Mwanamke wa Kijerumani aliiiona Hope Channel kwa bahati na alivutiwa na kile alichokisikia, kikiwemo kile kilichozungumzwa kuhusu Sabato. Alimwalika mume wake asikilize pamoja naye. Yeye pia aliufurahia ujumbe. Siku moja walipokwenda kumtembelea mama yake, walivutiwa kuendesha gari lao kwa kupita njia nydingine. Njiani waliona kibao cha Kanisa la Waadventista wa Sabato. Walitambua kwamba walikuwa ni Waadventista kutoka Hope Channel. Siku ya Sabato alikwenda katika ibada. Kisha akamwalika mume wake na kisha mama yake kuijunga naye. Tangu hapo wote watatu wamebatizwa.

Uzoefu mwengine unamhusu dada mwenye asili ya Kirusi na Kijerumani. Alihudhuria ibada ya Siku 40 za Maombi na akaanza kuomba kwa ajili ya majirani zake waliokuwa wakizungumza Kirusi. Alipomwambia mmojawapo wa majirani zake kwamba alikuwa akimwombea, jirani alishangaa sana na kusema kwamba alikuwa anatafuta kanisa lililokuwa linatunza Sabato ya Biblia. Yeye pamoja na jirani yake walikuja kwenye mikutano ya injili. Wawili kati yao wamebatizwa.

Uzoefu mwengine unahusiana na mwanamke aitwaye Jeanne. Alikuwa ni mshiriki wa kanisa la Kibaptisti huko nchini Brazil na sasa alikuwa akitafuta huko Cologne kanisa linalozungumza lugha ya Kireno. Alipata kanisa la Kiadventista, akapokea masomo ya Biblia na akabatizwa. Baada ya kubatizwa aliwapigia simu ndugu zake huko Brazil na kumwambia mjomba wake, ambaye ni Mwadventista, kwamba yeye pia ni Mwadventista sasa. Ulikuwa ni mshangao mkubwa sana kwa

mama yake, wadogo zake na kanisa la Kibaptisti huko Brazil, ambalo amekuwa ni mshiriki. Familia yake huko Brazil mara kwa mara hutembelea kanisa la Kiadventista kwa ajili ya kujifunza kuhusu Sabato. Hili limeongoza watu watano kubatizwa huko Brazil: mama yake, dada zake wawili na ndugu zake wengine. Sasa anaomba kwa ajili ya ubatizo wa dada yake mwengine, aishiye Argentina. Anataka kuwa pamoja nao katika ufalme wa Mungu.

Chini ya uongozi wa Mungu tumepata uzoefu mwengine mwangi. Katika ubatizo wa kwanza watu nane walibatizwa – mtu mmoja mmoja kutoka Italia, Ujerumani, Peru, Brazil, Ukraine, Venezuela, Kolombia na Urusi.

Katika majira ya kipupwe tuliendesha tena mikutano ya uinjilisti kuhusu Siku 40 za Ibada. Jimmy Cardoso pamoja na mke wake, wenyе asili ya Brazil, lakini sasa wanaishi Marekani, waliendesha mikutano ya uinjilisti. Ingawa masomo yaliendeshwa kwa juma moja tu, mwishoni tuliweza kubatiza wapendwa wanne. Walikuwa wakipata mafundisho ya Biblia hapo mwanzo. Kulikuwa na Wajerumani watatu na Muitaliano mmoja.

Ubatizo wa kwanza na wa pili ulifanyika katika kanisa kuu mjini Cologne, ambalo lina washiriki 400 na lina vifaa vizuri vya kubatizia.

Tunamshukuru Mungu kwamba ametushangaza kwa namna hiyo ya ajabu. Nimeshawishika kwamba bado ana uzoefu mkubwa zaidi ikitungojea. Tafadhali endelea kutukumbuka katika maombi yako.” João Lotze, kutoka Cologne, Ujerumani

Maombezi muhimu: Mara ya kwanza nilisoma kitabu cha [40-Days Book (Siku 40 Kitabu)] kwa kukipitia tu. Kutoka ukurasa wa kwanza na kuendelea nilivutiwa sana. Hatupaswi tu kuomba kwa ajili ya mtu fulani, bali na kuwajali kwa upendo. Hili hufanya maombezi kuwa na nguvu. Bahati mbaya, sijawahi kuona maombezi ya namna hii hapo kabla. Kuiishi imani yako! Ninashawishika kwamba ni muhimu kwa mtu anayeomba, kama ilivyo kwa mtu, anayeombewa. Vivyo hivyo, inanihakikishia tangu mwanzo kwamba ushirika ndani ya kanisa ungeimarishta. O, nina imani kwamba ushirika kama huo utatokea kama ulivyoelezewa katika sura za mwisho ndani ya hiki kitabu. Kwa kweli, nililia, kwa sababu nilitamani ushirika kama huo kwa muda mrefu. Ninaamini kwamba kitabu cha ‘Kristo ndani yangu’ hutukomboa na kutuweka huru kutoka kwenye mafanikio yetu wenyewe. Nimesoma vitabu kadhaa kuhusu ‘Kristo ndani yangu’, lakini hiki kitabu kinaonekana kuwa cha msaada zaidi kuliko vyote. Ninaamini kwamba maisha yako ya maombi yataimarishta kwa kitabu hiki, kwamba ushirika ndani ya kanisa utatunzwa na kwamba utafanya maombezi kuwa hai zaidi. Hiki kitabu hunipatia tumaini kwa ajili yangu mwenyewe, kwa ajili ya

kanisa na kwa ajili ya ulimwengu. Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya kitabu hiki. Baadaye ninapanga kusoma Siku 40 guide book, kukiombea na kisha kwenda nacho mahali popote Mungu anaponionyesha.”

Majuma kadhaa baadaye nilipokea barua pepe kutoka kwa huyu dada: “Kama unavyofahamu nimesoma kitabu chote kwanza. Lakini tangu nilipoanza kujifunza ibada pamoja na mwanamaombi mwenzangu nimegundua kwamba [maombi] ni ya thamani zaidi kuliko nilivyofikiria mwanzoni. Nina majibu kwa maswali, ambayo sikuweza kuyapata hapo mwanzo mimi mwenyewe. Ninamshukuru Mungu kwa mwanamaombi mwenzangu, ambaye anashiriki kwa bidii.” H. K.

Sina uhakika tena: “Kijitabu kii twacho *Hatua za Uamsho Binafsi* kimenigusa kwa namna ya ajabu ... Nikiwa nimezaliwa katika familia ya Kidventista niliamini kuwa nilikuwa katika njia sahihi. Sura iliyoelezea wanawali kumi na hasa Warumi 8:9: “*Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake*” ilinishtua sana. Sikuwa na uhakika tena kama nilikuwa na Roho Mtakatifu na kama alikuwa anatenda kazi ndani yangu, kwa sababu hasa sikuwa na ‘matunda’ yaliyotakiwa maishani yangu. Sabato hii mchana nimemaliza kusoma kijitabu na huzuni ya kina na isiyoweza kuelezeka ikanjija. Kisha nikasoma lile ombi karibu na mwisho wa kitabu na hamu kubwa ikaamshwa ndani yangu ili kupokea Roho Mtakatifu, kumruhusu abadilishe moyo wangu na kwamba Mungu angeniumba kulingana na mapenzi yake. A. P.

Mjue YEYE: Muda fulani uliopita nilisoma makala yako juu ya uamsho. Nimekuwa nikiifikiria mada hii karibu miaka mitatu hivi. Sasa, nimeanza kusoma *Hatua za Uamsho Binafsi*. Ninaweza tu kusema AMINA kwa hili! Ninafurahi kwamba katika kurasa hizi nimepata mawazo ‘yangu mwenyewe’ mengi. Ninashawishika kwamba ndani ya kanisa letu tunakosa lengo kwa inchi moja. Siwezi kuondoa hisia kwamba tumepoteza mwelekeo wa mambo ya muhimu! Mara nydingi inahusiana na ‘ukweli ni upi’, ‘tunapaswa kuishije’ au ‘unabii ni wa muhimu kiasi gani’, na sisemi kuwa hili ni kosa. Lakini tunashindwa kutambua KWA NINI Mungu alitupatia mambo haya! Je ukweli haukusudii kuwa na ushirika mkamilifu pamoja na Mungu? Badala yake, mambo haya hayapaswi kutusaidia kumfahamu Mungu KABISA? Je si lengo la unabii kwamba tukiri ukuu wa Mungu mwenyezi, kwamba tuelewe kwamba anaushikilia ulimwengu wote mikononi mwake na kuuongoza na kwamba kwa namna hiyo hiyo anaweza kuongoza na kutengeneza maisha yetu? Uzima wa milele ni nini? Yohana 17:3: ‘Na uzima

wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.’ Katika mfano wa bwana arusi unasema kwa wanawali watano wapumbavu: ‘*Siwajui ninyi*’ Kusudi la imani yetu ni kumjua Mungu tu, kuwa na ushirika na YEYE, ili kwamba YEYE aweze kutujaza kama alivyolijaza hekalu huko nyuma (2 Mambo ya Nyakati. 5:13-14). Na anapojaa ndani yetu, huujaza mwili wetu wote, kisha sisi hatuishi, bali Kristo huishi ndani yetu.” (Mtunzi anafahamika na Mhariri)

MAJIBU YA KUSHANGAZA KWA MAOMBEZI

“Kitabu cha pili cha Siku 40 kutoka kwa D. Smith ni mbaraka wa ajabu kwangu. Baadhi ya watu niliowaombea wameshuhudia mabadiliko ya nyuzi 180 maishani mwao.

Wakati wa Siku 40 nilikuwa na mazungumzo ya kina kuhusu mambo ya kiroho pamoja na rafiki. Aliniambia kwamba maisha yake yamekuwa na mwelekeo tofauti ndani ya majuma kadhaa. Alikuwa na hitaji kubwa la kuomba, alikuwa anatafakari zaidi neno la Mungu na aliweza kuachia baadhi ya mambo ambayo yalikuwa ya thamani na ya kupendeza kwake hapo kabla. Nilipata ujasiri na kumwelezea juu ya kitabu cha Siku 40 na pia nilimwambia kwamba alikuwa mmoja wapo wa watu watano niliokuwa nikiwaombea. Kisha alijibu kwa mshangao chanya: ‘Kwa hiyo unahuksika kwa yote haya.’

Msichana mmoja alifanya uamuzi wa kutoa maisha yake 100% kwa Mungu. Japokuwa alikuwa muumini tangu alipokuwa mdogo, alikuwa akiishi bila Mungu. Hakuwa na shauku ya imani kabisa na alikuwa amenaswa kabisa na maisha ya kidunia. Kwa sasa amebadilika kabisa; kila mtu, aliyemfahamu na akimuona sasa, hushangaa. Anajifunza Biblia pamoja nami sasa na anashiriki katika kipindi cha Siku 40 kanisani kwetu na anataka kuwatia moyo wengine kuwa na maisha makini ya kiimani.

Binti mwingine mdogo, ambaye nilimuombea, alilazimika kushiriki katika kozi ya mafunzo ya juma moja na alikaa pamoja na washiriki wengine katika nyumba moja. Alikuwa na hofu kuhusu kukaa kwa muda huu na watu wote hawa wageni. Siku moja kabla hajaondoka nilimtia moyo katika maombi na kumwambia kwamba nimekuwa nikimuombea kwa muda sasa. Kwa hiyo tulionomba kwamba Mungu ampatie amani katika hali hii na kwamba angeufanya uzoefu huu kuwa jibu katika maombi. Wakati wa kozi ya mafunzo alinipigia simu na kwa furaha akaniambia kwamba Mungu amefanya kitu fulani cha kushangaza kwake. Hajampatia tu amani kamilifu, bali pia amempatia ujasiri wa kutojihuisha na starehe za jioni, ambazo zilihuisha diskos, pombe, n.k.

Baada ya siku 40 nimeendelea kuomba kwa ajili ya watu hawa, kwa kuwa nimesikia na nimeona namna nyangi ambazo Mungu hujibu maombi.” A. M (Imefupishwa)

JINSI MUNGU ANAVYOFANYA KAZI KUPITIA MAOMBEZI

“Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita nilipoteza mawasiliano kabisa na mtu wa muhimu sana kwangu. Alionekana kutojali ujumbe wangu niliomtumia kwa njia ya simu. Nilisikia kwamba hakuwa akienda kanisani tena katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. (Alikulia kanisani) Na kwamba alikuwa na mahusiano na mwanamke ambaye hakuwa Mkristo. Nilimuweka kijana huyu katika orodha yangu ya maombi, japokuwa sikufikiria kama ingewezekana kuwasiliana naye tena, kwa kuwa aliishi umbali wa km 600 na hakuwahi kunijibu. Hatahivyo, niliomba kwa ajili ya ‘ishara ya uhai’.

Ndani ya muda mfupi nilisikia kuhusu ubatizo wa kaka yake, ambao ‘ulipaswa kufanyika’ karibu na mimi na ulikuwa kwenye tarehe ya kipindi cha siku 40 za Maombi (mwanzoni ulikuwa umepangwa kufanyika tarehe nyagine.) Niliamua kuhudhuria-na kukutana naye! Tuliweza kuwa na majadiliano ya kina na akaniambia kwamba kwa muda sasa amekuwa na hitaji kubwa la kurudi kwa Mungu, lakini hakuwa na nguvu ya kubadilisha mtindo wake wa maisha. Nilimwambia kwamba katika siku 20 zilizopita nimekuwa nikimuombea sana na kwamba hata kabla ya hapo amekuwa kwenye orodha yangu ya maombi. Alishangaa sana kwamba ni katika kipindi hicho ndipo amehisi Mungu akifanya kazi ndani yake.

Katika huduma ile ya ubatizo kiroho aliguswa sana na mchungaji alipotoa wito, niliweza kuhisi vita iliyokuwa ikiendelea ndani yake na baada ya kuhangaika kwa muda mrefu mwishowe alianguka chini na akaanza kulia. Alijisalimisha kwa Mungu kwa mara nyagine! Jioni ilipofika, aliniambia kwamba ameamua tena kwenda kanisani kila siku na kubadilisha mtindo wake wa maisha. Kamwe hakuwa ametarajia juma lile kumalizika kwa namna hii.

Majuma kadhaa baadaye nilikutana naye katika Misheni ya konferensi ya vijana, ambayo pia ilimuimarisha na kumjenga. Ninamshukuru Mungu kwa toba ya mpendwa huyu.” M. H.

KANISA HUKO LUDWIGSBURG / BADEN-WUERTTEMBERG, UJERUMANI

“Mwanzoni tulisoma kitabu cha Siku 40 kwa pamoja kama wanandoa na kushuhudia faida kubwa binafsi na mibaraka wakati wa kipindi cha maombi. Baadaye, tuliandaa mukutano wa maombi mara mbili kwa juma kanisani na kusoma kitabu pamoja na washiriki wa kanisa. Kwa namna ya pekee tulipata mbaraka wa Mungu na uongozi wake na kushuhudia miujiza mingi ndani ya muda wa siku 40. Kama kanisa Mungu alitufanya upya na kutuamsha: washiriki wa kanisa, ambao kamwe hawajawahi kuwa na ujasiri wa kuzungumza watu wasiowafahamu, ghafla wakaanza kuzungumza nao kwa mbinu zao wenyewe. Mungu anatuunganisha pamoja kama kanisa kupitia maombi ya pamoja. Tulipata upendeleo wa kuwa na uzoefu maalum katika maombezi na kusaidia watu watano ambao tuliwaombea katika kipindi cha siku 40. Mungu alifanya kazi kwa namna ya pekee katika maisha ya watu hawa. Mara kwa mara watu kutoka mtaani ghafla hujitokeza siku ya Sabato wakati wa ibada. Tunatoa masomo ya Biblia kwa mojawapo ya familia hizi. Wameifahamu Sabato kupitia video katika mtandao na kitabu cha *The Great Controversy* na wamekuwa wakilitafuta kanisa kwa muda sasa.” Katja na Christian Schindler, Kanisa la Waadvetista Wasabato huko Ludwigsburg (imefupishwa)

UZOEFU WA SIKU 40

“Kila kitu kilianza kwa semina juu ya *Hatua za Uamsho Binafsi*. Katika wakati ule shauku iliingia ndani yangu ya kuwa na uzoefu wa Mungu maishani mwangu. Kisha nikasikia kuhusu siku 40 za maombi na ibada. Mara ikawa wazi kwangu – Nilitaka kupata uzoefu wa tukio hili. Kwa kweli, sikufahamu kile nilichokuwa ninaanza kuhusika nalo. Kutafuta mtu wa kuomba naye (ambako kulikuwa ni sehemu ya kipindi) haikuwa vigumu. Changamoto yangu ilikuwa ni kutafuta muda kwa ajili ya kila mmoja wetu kila siku kwa siku 40. Kama nesi nina masaa ya kazi yasiyo ya kawaida. Sikuwa nimelifikiria hilo. Hata hivyo, Mungu alibariki uamuzi wangu tangu mwanzo. Nilizisubiri zile dakika za thamani kwa hamu ambazo tuliweza kujadiliana juu ya mada na kusihi kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Tuligundua kwamba maombi yalibadilisha kitu fulani maishani mwetu. Na hatukuweza kukaa nacho wenyewe. Katika kila fursa iliopatikana tulivutiwa kusema jambo fulani. Ilikuwa ni muhimu kwangu kuwatia moyo watu wengine kupata uzoefu kama huo. Matokeo hayakushindwa kuonekana. Baadhi ya washiriki waliambukizwa na shauku yetu. Haraka timu za maombi zikaungana pamoja. Tulitazamia kuwaambia wengine kila juma kile ambacho tulikipata.

‘Kirusi’ hiki pia kiliwakamata vijana wetu wachache. Siku 40 ziliisha haraka sana. Hatukutaka ziishe na hatungeweza kuacha. Hivyo tulienendelea na muda wetu wa ibada pamoja na kitabu cha *Maranatha – The Lord is Coming* kilichoandikwa na Ellen White. Na Mungu hakutufanya tusubiri muda mrefu. Bado katika kipindi cha siku 40 alitupatia majibu ya kushangaza kwa maombi yetu. Mtu fulani, tulyekuwa tukimuombea katika kipindi hiki, aliwasiliana na kanisa kwa mara nyine baada ya kutoonekana kwa muda mrefu. Tulifurahi sana. Watu walionizunguka wakawa wa muhimu sana kwangu. Nia yangu ya kuwambia wengine juu ya upendo wa Mungu ikaimarika zaidi. Maisha yangu yakabadilika. Wengi wetu tuliweza kufahamiana na kuelewana vizuri. Wengi wanahuusika katika maisha yawengine na wako kwa ajili ya kusaidiana kila mmoja. Ushirika umekuwa na maana mpya kabisa. Kitabu cha Siku 40 ya Maombi na Ibada cha Dennis Smith kilikuwa msaada mkubwa kwangu. Ni rahisi kuliko inavyoonekana kupata mtu wa kuomba naye na kuwa na uzoefu na Mungu. Watu waliokuwa karibu nasi watatushukuru kwa kwa jamo hili.” Hildegard Welker, Crailsheim Seventh-Day Adventist Church, ni nesi katika wodi ya upasuaji. (imefupishwa kidogo)

YESU MFANO WETU

Yesu ni mfano wetu mkuu katika mambo yote. Katika Luka 3:21-22 tunasoma: “*Baada ya watu wote kubatizwa, Yesu naye alibatizwa. Na alipokuwa akiomba, mbingu zilifunguka. Roho Mtakatifu akashuka juu yake kama hua ...*”

Ellen White alisema yafuatayo kuhusu tukio hili: “Kama jibu la ombi lake kwa Baba yake, mbingu zilifunguka, na Roho Mtakatifu alishuka na kukaa juu yake.”¹³⁰

Kilichotokea wakati wa huduma yake kinashangaza: Kila asubuhi aliwasiliana na Baba yake wa Mbinguni, **akipokea kutoka kwake kila siku ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu.**¹³¹ Ikiwa Yesu alihitaji ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu kila siku, sisi tunauhitaji zaidi kiasi gani!

¹³⁰ E. G. White, *Ye Shall Receive Power* (1995), uk. 14.4

¹³¹ E. G. White, *Signs of the Time*, Nov. 21, 1895

SHAUKU NA KUSHIRIKISHA WENGINE

*Zinahala tuitocayo hurudi mioyoni mwetu wenjewe.
(Mithali ya Kijerumani)*

*Ninawezaje kuwasaidia watu wengine kupata
"Uzima Tele". (Yohana 10,10)*

JINSI YA KUAMSHA SHAUKU KATIKA MAISHA YALIYOJAZWA NA ROHO?

Viongozi na makanisa wanaweza kufanya nini? Hapa kuna njia chache zinazoonyesha kile tunachoweza kufanya kama viongozi (mfano kama rais, mchungaji, kanisa au katibu wa misheni, viongozi wa taasisi au watu wengine muhimu) kwa kushirikiana na mabaraza ya makanisa, makanisa na makundi.

Njia zinazoweza kutumika

1. **Vikundi vya ibada vya watu wawili:** Jifunze program ya 40-Day-Worships kama wanandoa au pamoja na mtu wa kuomba naye. Anza na kitabu cha 40-Days “Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming”, cha Dennis Smith, Review and Herald, na ikiwezekana baadaye tumia kitabu cha pili cha 40 Days “Prayers and Devotions to Revive your Experience with God”. Pindi wanandoa wanapofanya ibada pamoja, kuna faida kubwa na hukuza upendo wao. Kwa kawaida, mnawenza pia kuwa na ibada ya pamoja na mtu mwengine. Yafaa sana kukutana pamoja, lakini pia inawezekana kwa njia ya simu au Skype au njia zingine za mawasiliano. Vikundi vya ibada vya watu wawili vina matokeo makubwa. Neno la Mungu hupendekeza kwamba tuombe wawili wawili (Mathayo 18:19) na kufanya kazi katika makundi ya watu wawili wawili

(Luka 10:1). Aina hii ya ibada ni sharti la muhimu kuwatia moyo wengine kufanya namna hiyo hiyo.

2. Elezea au gawa kitabu. Kwa mfano:

Kwa mfano Kijitabu cha “Hatua za Uamsho Binafsi” (kinapatikana bure katika lugha zote zilizotafsiriwa)

Zaidi ya shuhuda 80 za wasomaji na mamia ya mazungumzo yameonyesha kwamba kijitabu hiki kinakubalika zaidi katika namna zifuatazo:

- ▶ Kimefungua macho yao katika hali zao za kiroho: wameokoka au wamepotea? (maelezo zaidi katika sura ya 2)
- ▶ Wameelewa hatua muhimu ambazo huongoza katika maisha ya kiroho: Kujisalimisha kila siku kwa Kristo, kuomba kila siku kwa ajili ya kupokea Roho Mtakatifu. [Desire of Ages uk. 676.2]
- ▶ Hatua nyingine zote binafsi huonyeshwa na Roho Mtakatifu. (maelezo zaidi katika sura ya 3)
- ▶ Kwa kuomba kulingana na ahadi za Biblia, walikuwa na uhakika kwamba walipokea Roho Mtakatifu. (Maeleo zaidi katika sura ya 5)
- ▶ Furaha yao kubwa iliwafanya kuwa mashahidi na wasambazaji wa kijitabu.

Kupitia uzoefu wa wengi tumejifunza kwamba matumiziya “Hatua za Uamsho Binafsi” pamoja na kitabu cha 1 na cha 2 cha Siku 40 kumeleta matokeo bora zaidi. “Hatua za Uamsho Binafsi” hufungua macho tena ni msaada bora wa namana ya kuanza mara moja. Vitabu vya 40- Day vimepanua na kusaidia kuimarisha maisha ya kiroho. Zaidi ya yote, vimeongoza katika ibada binafsi ya asubuhi na maombi mengi yaliyojibowi.

3. Usomaji wa machapisho mafupi wakati wa ibada: Kwa kipindi cha ibadaaya zilizochaguliwa zinazohusu kuishi na Roho Mtakatifu zinaweza kusomwa wakati wa ibada kabla ya hubiri. (Dakika 5 mpaka 10) Machapisho yalivypendekezwa yameorodheshwa katika hatua iliyofoata. Baada ya muda, watu wanaweza kutiwa moyo kuunda vikundi vya watu wawili au kutekeleza wazo la siku 40 (angalia pointi ya 12).

4. Aya kutoka kwenye vitabu vyetu ambazo zinaweza kuchapishwa na kuwekwa katika ubao wa matangazo ya kanisa au zinaweza kupendekezwa wakati wa matangazo:

- ▶ Tumaini la Vizazi Vyote (The Desire of Ages), sura ya. 73: “Let your heart not be troubled.”

- ▶ Matendo ya Mitume (The Acts of the Apostles), sura ya 5 “The Gift of the Spirit”
 - ▶ Christ’s Object Lessons, sura ya 12 “Asking to Give”
 - ▶ Testimony Treasures volume 3, The Promise of the Spirit, uk. 209-215
 - ▶ Tafakari ya siku moja kutoka katika kitabu cha ibada cha EGW “Ye Shall Receive Power” (vinapatikana katika duka lililoko karibu nawe la Adventist Book Center)
5. **Shirikisha wengine uzoefu wako:** Mara kwa mara kadri inavyowezekana shiriki uzoefu wa kiroho katika ibada. Uzoefu binafsi unaweza kutumika au kutoka kwa washiriki wengine au kutoka makanisa mengine. Unaweza kupata shuhuda kwenye tovuti hii – bofya kwenye neno “Testimonies.”
6. **Semina ya awamu nne kama Sabato ya msukumo:** Huenda hii ndiyo njia yenye ufanisi zaidi kwa kuamsha shauku haraka ndani ya kanisa. Hii ni Sabato maalum yenye masomo 3-4, kuanzia siku ya Ijumaa jioni, kisha katika ibada ya siku ya Sabato na pia mchana. Mada kuu inaweza kuwa kipindi cha “Hatua za Uamsho Binafsi”:
- ▶ Ijumaa jioni unaweza kuwa muda unofaa wa juma kushirikisha uzoefu, kisha shirikisha uzoefu unaogusa. Ikiwezekana, unapaswa kutolewa uzoefu binafsi kutoka kwa mnenaji. Uwezekano mwagine ni kuzungumzia kuhusu “Surrender to Jesus”. Unaweza kupata mapendekezo ndani ya kijitabu cha “Abide in Jesus”, sura ya 2 ya “Kujitoa kwa Yesu”.
 - ▶ Inapendekezwa kuhubiri juu ya mawazo muhimu kutoka “Hatua za Uamsho Binafsi” wakati wa ibada. Ili kuwa na usahihi zaidi: shirikisha nukuu 2-3 kutoka kwenye utangulizi juu ya ukosefu wa Roho Mtakatifu. Endelea na mawazo makuu kutoka sura ya 1 “Yesu alifundisha nini kuhusu Roho Mtakatifu?” na kutoka sura ya 2 “Ni Nini Kiini Cha Matatizo Yetu?” (labda uigawanye katika masaa mawili tofauti)
 - ▶ Wakati wa mkutano wa kwanza mchana shirikisha mawazo kutoka katika sura ya 3 “Je Matatizo Yetu Yanatalulika – Jinsi Gani?”
 - ▶ Wakati wa mkutano wa pili mchana shiriki mawazo makuu kutoka sura ya 5 “Ufunguo Kwa Uzoefu Wa Utendaji”.

Kwa makanisa ambayo semina ya kwanza ya “Hatua za Uamsho Binafsi” imefanyika tayari, wanaweza kuwa na Sabato nydingine ya msukumo au semina nydingine kwa kutumia mada kutoka kwenye kijitabu cha “Abide in Jesus”. Kwa mara nydingine kunaweza kuwepo na vipengele vinne kutoka kwenye sura nne.

Yafaa wakati wa maandalizi ya Sabato ya msukumo kugawa vitabu vinavyohusiana na Sabato hiyo mapema pamoja na mapendekezo ya kuvisoma kwa umakini. Pia imethibitishwa kuwa na manufaa kuanza muda wa Siku 40 za Maombi mwishoni mwa juma mara tu baada ya Sabato ya msukumo (angalia pointi namba 12) au pamoja na usomaji wa mpango wa sura moja kwa juma kutoka “Hatua za Uamsho Binafsi”(angalia pointi ya 7).

7. **Usomaji wa Mpango:** **Sura moja kwa juma moja** – uwezekano rahisi na wenye mafanikio ni kusoma sura moja kila juma (ni vyema zaidi hata kama sura hii itasomwa zaidi ya mara moja) kutoka kwenye kijitabu cha “Hatua za Uamsho Binafsi” au “Abide in Jesus” au kutoka kwenye mojawapo ya vitabu vya Siku 40. Kundi au kanisa zima linaweza kukubaliana kuhusu tarehe ya kuanza. Hili linaweza kufanyika kwa maandalizi ya semina yenye sehemu nne (angalia pointi ya 6) au mara tu baada ya Sabato hii ya msukumo. Kila mtu anaweza kuamua ikiwa wanataka kusoma mwenyewe, pamoja na mtu mwingine au katika kikundi. Katika siku ya Sabato ingekuwa vyema kusoma masomo makuu kutoka katika sura zinazohusiana kwa muda wa dakika 5 na kisha kualika watu kusema shuhuda zao. Kama hakuna shuhud binafsi, basi ushuhuda kutoka kwa mtu mwingine unaweza kusomwa (andaa mapema – angalia Shuhuda). Kisha tangaza ni sura ipi itakayosomwa katika juma lijalo. Unaweza kuagiza vitabu vya Siku 40 kupitia tovuti ya www.spiritbaptism.org
8. **Endesha mahubiri** juu ya kuishi na Roho Mtakatifu au watie moyo watu na muombe mtu fulani afanye kazi hiyo. Yapo mahubiri mazuri ya Dwight Nelson yenye kichwa kisemacho: “Ground Zero and the New Reformation: How to be baptized with the Holy Spirit”. Mahubiri yake ya kuanzia tarehe 2 Septemba na blogu zake za tarehe 30 Agosti na tarehe 13 Septemba yanapatikana kwenye tovuti ya: www.pmchurch.tv/sermons
9. **Endesha Masomo ya Biblia** juu ya kuishi na Roho Mtakatifu au yasome kwa sauti.
10. **Vikundi vidogo au vikundi vya maombi** vinaweza kusoma na kujadili vitabu husika na kuomba pamoja. Zaidi ya hayo, vikundi vya watu wawili wawili vinatakiwa kuhimizwa, ambavyo vinafanya ibada za Siku 40 na kisha mara moja kwa juma kundi lote likutane kwa mjadala, kubadilishana uzoefu na kuomba pamoja. (angalia pointi ya 12).

11. **Sabato ya Utume** – Kwa kuwa kuishi na Roho Mtakatifu hutufanya kuwa wamishenari, ni fursa nzuri, katika namna ya kudumu au kwa muda maalum, kuzirejesha Sabato za utume. Hili lilikuwa ni jambo la msingi kwa waanzilishi wa Kanisa letu. Mababa zetu waliendesha Sabato za Kimishenari Sabato ya kwanza ya kila mwezi. Majukumu ya maandalizi na utekelezaji kwa maombi mengi yanapaswa kufanywa na mtu mmoja aliyejitoa kwa moyo au kikundi kidogo. Ikiwa wazo hili litaunganishwa na baadhi ya fursa zilizotajwa hapo juu, linaweza kuchangia kuwa na masaa ya Sabato yenye mafanikio na furaha. Zaidi ya hayo, inaweza kusaidia uamshwaji wa roho ya kimishenari.
12. **Jifunze na jadili wazo la 40-Days (Siku 40)** – Wazo hili limeelezewa katika kitabu cha kwanza, cha pili na cha tatu cha Siku 40, sehemu ya “Introduction and Overview”. Baadaye, linaweza kujadiliwa katika baraza la kanisa, baraza la utume au kamati tendaji ya konferensi. Wazo hili linaweza pia kuletwa katika mikutano ya kichungaji, mikutano ya wazee wa kanisa, mikutano ya kimishenari na mikutano ya vijana, katika mikutano ya maburudisho, mikutano ya mitaa na katika shule za utume. Wazo hili husaidia katika maeneo yafuatayo:
- ▶ Husaidia kuwa na uhusiano wa karibu zaidi pamoja na Yesu kupitia Roho Mtakatifu.
 - ▶ Husaidia kuimarisha maisha ya maombi (mtu mmoja, wawili, au vikundi).
 - ▶ Husaidia kukuza mahusiano yetu binafsi.
 - ▶ Husaidia kuimarisha maisha ya kiroho kupitia ibada za 40 Day juu ya Roho Mtakatifu..
 - ▶ Huwezesha maombezi kwa ajili ya waliopotea au watu ambao ni vigumu kuwafikia na kuwezesha kuwasiliana nao.
 - ▶ Husaidia uinjilisti, vikundi vyta kutoa msaada au masomo ya Biblia.

Hili hufanikishwa katika hatua tatu za kiroho:

- ▶ Uimarishaji binafsi wa kiroho kupitia ibada ya Siku 40 katika vikundi vyta watu wawili.
(Kupitia mjadala wa mada katika vitabu “Discussion Questions” na maombi ya kila siku kulingana na “Prayer Focus” kwa ajili ya Roho Mtakatifu.)
- ▶ Maombezi yaliyojazwa na Roho na kila mtu kuwasiliana na watu watano ambao hawajafikiwa au washiriki wa kanisa ambao ni dhaifu wa imani.
- ▶ Kazi za kiinjilisti (mawasilisho/semina, makundi ya msaada yenye mtazamo wa kimishenari, masomo ya Biblia, maonyesho madogo au ya kati kwa mfano ya afya, uumbaji au maonyesho ya unabii.)

Kwa wale wanaofanya maandalizi, Kitabu cha Dhana ya Siku 40, kitiwacho "Instruction Manual", kinapatikana hapa: www.missionsbrief.de/downloads/40tage-instructions.pdf ("40DayInstructions.pdf.") Kina hatua zote zinazoongoza kwenye uzoefu wenyewe mafanikio wa Siku 40. Njia ya kiroho iliyopendekezwa ni maandalizi bora kabisa kwa ajili ya mfululizo wa masomo ya kiinjilisti uliopangwa. Kwa namna hii, viongozi na washiriki wa kanisa watakuwa wamejiandaa wenyewe kiroho. Kupitia maombezi na kila mtu kuwasiliana na watu watano ambao hawajafikiwa, eneo linaandaliwa kwa ajili ya masomo ya kiinjilisti. Aina mbalimbali za uinjilisti zinaweza kutumika. Wasiliana na DennisSmith kwaajili ya kuagiza Vitabu ya Siku 40 kupitia www.spiritbaptism.org

13. Gawa karatasi ya taarifa juu ya mpango wa Siku 40 za maombi kwa washiriki wa kanisa. Zaidi ya hili, inapendekezwa kualika kuanzia siku ya kuanza mfululizo wa masomo ya Siku 40 kanisani kwako.
14. Chapisha makala zinazofaa kwenye matangazo ya kanisa, matangazo ya konferensi, matangazo ya unioni, majarida, tovuti za kanisa, na vile vile ndani ya magazeti ya kanisa na magazeti kutoka idara nyingine za kanisa.
15. **Utafiti:** Baada ya wasilisho juu ya mada ya Roho Mtakatifu, vipande nya karatasi vinaweza kupitishwa kwa utafiti mfupi ambao wahusika hawaandiki majina yao:
 - Kama mtu anaomba mara nyingi au kila siku kwa ajili ya Roho Mtakatifu, anaweza kuweka alama moja.
 - Kama mtu anaomba kila siku kwa ajili ya ahadi ya Roho Mtakatifu, anaweza kuweka alama mbili.Hii ni njia nzuri ya kuweza kutambua hali ya sasa ikoje mahali hapa.

Maandalizi yenyeye maombi na maombi kwa ajili ya fursa zote zilizotajwa hapo juu ni muhimu. Ni muhimu sana kama watu wanaofanya maombi kuwaomba baadhi ya washiriki wa kanisa, vikundi nya maombi viliyopo na hata kanisa zima kwa maombezi maalum kwa jambo mahsus – kwa ajili ya utekelezaji na mafanikio.

NAMNA YA KUSAMBAZA VITABU VYA UAMSHO

Lengo:

Ndugu mmoja wakati fulani alisema: "Ujumbe huu unapaswa kuifikia kila kaya ya Kiadventista ulimwenguni kote. Nitafanya sehemu yangu," na anaifanya – kwa juhudhi nyingi. Dada mmoja aliandika: "Hiki kijitabu kinapaswa kutafsiriwa katika lugha zote kuu, au vizuri zaidi katika lugha zote." Ameweza kuishawishi konferensi yake na sasa anahubiri mada hii katika mitaa yote. Zaidi ya yote, kupitia uongozi wa Mungu ameleta maelfu ya vijitabu katika nchi jirani ambayo hapo mwanzo haikuweza kupokea imani ya Kikristo.

Maendeleo na Fedha:

Kupitia uongozi wa Mungu, kitabu cha Hatua za Uamsho Binafsi kinaweza kusambazwa kwenye familia zote za Kiadventista katika lugha zao wenywewebure. Kwa msaadawa wachungaji, konferensi na unioni nyingi tayarizimesambaza nakala za bure kwa familia ndani ya mitaa yao husika. Watu wa kwanza kufanya hivi walikuwa ni Konferensi ya Swiss-German huko Uswisi, Unioni ya Austria huko Austria, na Konferensi ya Baden-Wuerttemberg huko Ujerumanii. Mradi huu uliendelezwa kupitia mpango wa kipekee wa Mungu. Kupitia mvuto Mungu na kwa neema yake zaidi ya nakala 600,000 zimesambazwa kufikia mwaka 2017. Tungependa kukualika umuombe Bwana aendelee katuongoza na kutupatia rasilimali zinazohitajika kuundeleza miradi huu. Mara nyingi tunaomba msaada wa kifedha kutoka Konferensi au Unioni mbalimbali zenyet uwezo mzuri wa kifedha kulipia nusu ya gharama za uchapishaji. Kwa wengine, lakini hasa kwa misheni, kwa msaada wa Mungu, tungependa kugharamia kila kitu sisi wenywewe. Lakini mtumiaji wa mwisho wakati wote atapokea kitabu bure, na hata kupokea vingi.

Kigezo muhimu

Tunatamani uwafikie wengine. Kigezo cha kushirikisha ni kwamba ni muhimu uwe umebarikiwa wewe binafsi na ujumbe huu na kuwa na Kristo akiishi moyoni mwako kwa kumpokea Roho Mtakatifu kila siku. Tafadhali soma katika Kitabu cha Desire of Ages, uk 676.2 [egwwritings.org] rejea muhimu kwa kauli ya Yesu katika Yohana 15:4:

"Kaeni ndani yangu nami ndani yenu" Hili humaanisha mambo mawili:

- ▶ kuendelea kupokea Roho wake
- ▶ na maisha ya kujitoa kwa dhati katika huduma yake

Kwa nini Yesu alidokeza hili? “Hayo nimewaambia, ili furaha yangu [furaha ya Yesu ni tunda la Roho Mtakatifu Wagalatia 5:22] iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe.” (Yohana 15:11)

Njia za Kusambaza:

Maombi

Ni muhimu kwamba kuwaambia wengine habari za Injili ni lazima kutanguliwe na ombi la upatanisho. E. G. White anasema katika kitabu cha Evangelism, uk.341.3, “Kupitia maombi mengi unapaswa kutafuta roho, maana hii ndiyo njia pekee unayoweza kuifikia mioyo.”

Kusambaza kijitabu:

Unaweza kugawa kijitabu hiki kwa kushirikisha wapokeaji kwa kuonyesha mtazamo wako na uzoefu wako. Hawa wanaweza kuwa marafiki, viongozi na watu wenyewe nyadhifa muhimu kanisani, katika konferensi na unioni, ofisi za uchapaji, miradi ya kimishenari, na taasisi nyingine. Fursa nyingine muhimu inapatikana katika mikutano mikubwa kwenye banda la maonyesho au usambazaji kwa wajumbe kwa ruhusa ya waandaaji. Weka akilini kwamba pia kila familia ya Kiadventista itapokea nakala ya bure.

Kijitabu hiki kinaweza pia kutumwa kwa njia ya posta au kwa wasambazaji kuonana ana kwa ana na wapokeaji.

Usambazaji kwa njia ya mtandao

Njia ya kisasa zaidi ya kusambaza ujumbe huu ni kwa njia ya barua pepe. Ujumbe ulitumwa Australia na kutokea hapo ukaenda Mizoram, India. Pia ulifika Pakistani kupitia Brazili. Unaweza kusoma ujumbe kupitia tovuti ifuatayo www.schritte-zur-persönlichen-erweckung.info. Unaweza kupiga chapa na/ au kikituma kupitia tovuti kwa mtu mmoja au wengi katika lugha zote zilizotafsiriwa. Unaweza pia kuwajulisha watu kwamba tovuti inapatikana kwa lugha ya Kiingereza katika www.steps-to-personal-revival.info. Kufikia mwishoni mwa mwaka 2016, chini ya uongozi wa Mungu na msaada wa dhati kutoka kwa wafasri, ujumbe huu utapatikana katika lugha 20, na lugha zingine 8 zitafuata baada ya muda mfupi. Kwa msaada wa Mungu, nyingine nyingi zaidi zitafuata kwa hakika.

Kusambaza kupitia vitabu vyatandaoni

Kitabu cha bure kinapatikana mtandaoni katika tovuti hii katika mfumo wa ‘epub’ na ‘mobi’. Unaweza pia kuagiza kupitia Amazon kwa kiasi cha €1.00.

Usambazaji kupitia Mitandao ya Kijamii

Njia bora zaidi ya kuwashirikisha marafiki na watu unaokutana nao mada zilizomo kwenye tovuti hii au kupitia vitabu vilivyo katika mfumo wa PDF ni kupitia mitandao kama vile Facebook, Google+, Twitter au WhatsApp. Kupitia kushiriki nao na kualika, unaweza kuwafikia watu ulio na mawasiliano nao, na vile vile watu wapya katika nchi na mabara tofauti.

Usambazaji kupitia Mahubiri na Semina

Wachungaji wote na wahubiri walei wana fursa ya kipekee kushirikisha makanisa ujumbe kupitia hubiri moja au mahubiri mengi. Unaweza kufanya hili kupitia masomo yako mwenyewe au kwa kutumia masomo kutoka katika kijitabu hiki. “Kamwe sijawahi kuhubiri mada ambayo kanisa tayari lilikuwa limeisikiliza au kusoma. Kupitia tafiti za kielimu ninafahamu leo kwamba kwa kweli ni lazima kusoma au kusikiliza mada muhimu mara 6-10,” (Uzoefu binafsi na ushauri wa Kaka Helmut Haubeil). Ukipenda, unaweza kutaja kwamba unatumia mawazo makuu na nukuu kutoka kwenye kijitabu hiki.

Endapo huhitaji kuhubiri basi unaweza kuomba watu wengine kutumia mada hii katika mahubiri yao.

Semina ya siku ya Sabato yenye mada ya jumla kuhusu “Hatua za Uamsho Binafsi” inapaswa kuwa na angalau mada tatu:

Hubiri:

Kiini cha matatizo yetu ni nini?

Je matatizo yetu yanatokana na sababu za kiroho?

Je tuna ukosefu wa Roho Mtakatifu?

Ninawezaje kufanya uchunguzi binafsi wa maisha yangu ya Kiroho?

(Haya ndio mawazo makuu kutoka kwenye utangulizi, na vile vile kutoka sura ya 1 na ya 2)

1. Kipindi cha mchana:

Matatizo yetu yanatalulika – lakini kwa namana gani?

- ▶ Tunawezaje kukuza maisha thabiti ya Kikristo yaliyojaa furaha?
- ▶ Roho Mtakatifu anajazaje maisha yetu? Neno la siri ni “kila siku”.
(Haya ni mawazo makuu ya sura ya 3).

2. Kipindi cha mchana au jioni

Mambo muhimu kwa ajili ya matumizi ya vitendo/Jinsi ya kutumia kwa vitendo (Mambo muhimu kwa Uzoefu Halisi)

- ▶ Ninawezaje kutumia kwa vitendo na kupata uzoefu wa suluhisho la Mungu maishani mwangu?
- ▶ Ninapaswaje kuomba kwa ajili ya hakikisho la kujazwa Roho Mtakatifu?
- ▶ (Haya ni mambo ya muhimu ya sura ya 5)

Shuhuda Binafsi

Shuhuda binafsi juu ya mada zifuatazo ni muhimu sana:

- ▶ Kuhusu mtazamo binafsi au ufahamu uliotokana na kusoma kitabu hiki
- ▶ Kuhusu matokeo ya ujumbe huu maishani mwetu.

Tafsiri katika lugha yako mwenyewe

Ikiwa kitabu hiki hakijatafsiriwa katika lugha yako mwenyewe, huenda unaweza – kuititia maombi na majaliwa ya Mungu–kumpata mtu, ambaye yuko tayari na anayewenza kutafsiri. Watafsiri, ambao walikuwa wameguswa binafsi na ujumbe wanafaa sana. Hadi sasa, tafsiri nyingi zimefanywa kwa kujitolea, kwa kuwa mfasiri naye amekuwa na shauku kubwa ya kusambaza ujumbe huu. Lakini wakati mwingine kutafsiri ni njia ya kujipatia kipato. Wale wafasri walilipwa walilipewa ujira wa “kindugu”. Tunashukuru, ikiwa utawasiliana na Helmut Haubeil wewe mwenyewe kuhusiana na suala la kutafsiri. Anaushauri mzuri wa kutoa na huhakikisha kwamba kijitabu kinatolewa katika muundo unaofanana kwa kila lugha.

Kupitia Roho Mtakatifu tuna kiongozi wa ajabu katika hali zote za maisha na tuna nguvu kulingana na utajiri wa utukufu wake.

Hivyo tabia zetu zinaweza kubadilika na tunaweza kuwa vitendea muhimu katika kazi ya Mungu. Kujitoa kwetu kila siku na kubatizwa kila siku na Roho Mtakatifu kutaongoza katika mafanikio halisi maishani mwetu.

Bwana anataka kutuandaa kwa wakati muhimu zaidi katika historia ya ulimwengu. Anataka tuwe tayari kila mmoja wetu kwa ujio wake na kwamba kwa nguvu ya Roho Mtakatifu tushirikiane pamoja katika kuimaliza kazi ya injili. Anataka kutuongoza kwa ushindi katika nyakati ngumu.

Mungu akupatie uamsho na matengenezo binafsi kupitia kujitoa kila siku na ubatizo wa kila siku wa Roho Mtakatifu.

Ninataka kuhitimisha kwa aya ya Biblia na ombi kwa ajili ya uamsho:

“Ikiwa watu wangu, ... watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.” (2 Mambo ya Walawi 7:14)

Ombi: Baba wa mbinguni, tunaomba utupatие unyenyekevu (Mika 6:8). Weka miyoni mwetu shauku kuu ya kuomba na kuutafuta uso wako. Tufanye kuwa tayari na tusaidie kuacha njia zetu mbaya. Tunaomba utimize matakwa ndani yetu na kama matokeo ya ahadi Yako tujibu maombi yetu. Tusamemehe dhambi zetu na tuponye na uvuguvugu wetu na uasi wetu. Tusaidie tujitoe kwa Yesu kila siku na kwa imani tupokee Roho Mtakatifu. Amina.

“Uamsho unaweza kutarajiwa tu kama mwitikio wa maombi.”¹³² Ubatizo wa Roho Mtakatifu kama ilivyokuwa siku ya Pentekoste utaongoza kwenye uamsho wa dini ya kweli na kwenye utendaji wa miujiza mingi.”¹³³

¹³² E. G. White, *Selected Messages, Book 1* (1958), uk. 121.1

¹³³ E. G. White, *Selected Messages, Book 2* (1958), uk. 57.1

Inapendekezwa Usome Zaidi

Pendekezo muhimu: Soma kijitabu hiki, kama inawezekana, kila siku kwa siku sita. Utafiti wa kujifunza umeonesha kwamba ni lazima somo muhimu kwa maisha yetu lazima isomwe au isikike mara sita hadi kumi hadi mtu aielewe vizuri. Ijaribu. Matokeo yataonesha ukweli.

Mwalimu alijaribu: "Maneno haya yalinitia moyo: 'Ijaribu mara moja. Matokeo yataonesha ukweli.' Nilitaka kupata uzoefu huo na baada ya mara ya tatu ilinishika na niliona nilikuwa na upendo mkuu kwa Mwokozi wetu, ambao niliutamani maisha yangu yote. Ndani ya miezi miwili nilisoma kitabu mara sira na matokeo yake yalitosha. Ilikuwa kama niliweza kuelewa ilivyokuwa Yesu anapokuja karibu nasi na tunaweza kuangalia machoni mwake kulipo na upendo na upole. Baada ya hapo sikutaka kuwa tena bila furaha kuu kwa Mwokozi tena."

C. P.

Nimepokea shuhuda nyangi yenyeye shukrani na furaha kuhusu maisha yao mapya na roho mtakatifu. Karibia wote walikuwa kutoka wasomaji, ambao waliosoma tena kijitabu mara kadhaa.

MWONGOZO WA SIKU 40

Unaweza kupata msaada wa vitabu kwa ajili ya kuandaa Siku 40 za maombi pamoja na mfululizo wa masomo ya kiinjilisti baadaye kwa kutumia kitabu cha 40 Day cha Dennis Smith kutoka katika tovuti hii: www.SpiritBaptism.org chini ya mwongozo wa 40 Days Instruction Manual.

Uzoefu Mpya wa Kuishi na Roho Mtakatifu

Bwana wetu Yesu alisema: "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwashilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu..." (Matendo 1:8 NKJV)

Ombi maalum: Utakapokuwa na uzoefu wa kuishi na Roho Mtakatifu maishani mwako binafsi au unapokuwa unashuhudia, basi tutafurahi sana kama utatuma taarifa fupi kwa Helmut Haubeil ili aweze kuwashirikisha watu wengine katika Missionsbrief (gazeti dogo la Ujerumanilnalohusu kazi za utume). Tafadhali tuambie ikiwa unataka vifupisho tu vya majina yako chini ya taarifa au kama tunaweza kuandika jina lako kamili na kanisa unalosali. Tafadhali kumbuka kuwa

uzoefu wako utawaimarisha wengine kukua katika kutembea kwao na Roho Mtakatifu au kuanza safari na Roho Mtakatifu.

Mawasiliano:

Helmut Haubeil

Rosenheimer Str.49

D-83043 Bad Aibling / Oberbayern, Germany

E-Mail: helmut@haubeil.net

helmut.haubeil@gmail.com

Lugha: German or English

Namba ya simu +49 8061 4900 712

Literature on this Topic

- *40 Days [Book 1] Prayers and Devotions to Prepare for the Second Coming*
- *40 Days [Book 2] Prayers and Devotions to Revive your Experience with God*
- *40 Days [Book 3] God's Health Principles for His Last-Day People*
- *40 Days [Book 4] Prayers and Devotions on Earth's Final Events*
Dennis Smith, Review and Herald 2009-2013
- *If My People Pray – An Eleventh-Hour Call to Prayer and Revival*
Randy Maxwell, Pacific Press 1995
- *Revive Us Again*, Mark A. Finley, Pacific Press 2010
- *How to Be Filled With the Holy Spirit und Know it*
Garrie F. Williams, Review and Herald 1991
- *The Radical Prayer*, Derek J. Morris, Review and Herald 2008



BROCHURE 2: HATUA ZA UAMSHO BINAFSI

The Path to Complete Joy

ABIDE IN JESUS

"Abide in Me, and I in you." Abiding in Christ means a constant receiving of His Spirit, a life of unreserved surrender to His service.
E. G. White (*Desire of Ages*, DA 676.2)

Abiding in Him is not a work that we have to do as a condition in order to enjoy His salvation. Rather it is our consent to let Him do everything for us, in us, and through us. It is a work He does for us – the result and the power of His redeeming love. Our part is simply to yield, to trust, and to wait for Him to accomplish what He has promised. (Andrew Murray)

CHAPTER 1: JESUS' MOST PRECIOUS GIFT

*What does Jesus teach about the Holy Spirit? Do you know Jesus' most impressive message?
What are the tasks of the Holy Spirit?*

CHAPTER 2: SURRENDER TO JESUS

*What does surrender mean? Do I consequently lose my own will? Or will I become stronger?
What can prevent us from surrendering ourselves to Jesus?*

CHAPTER 3: JESUS ABIDING IN YOU

*What are the prerequisites for Jesus living in me? How will "Christ abiding in me" effect my life?
The greatest achievement: Experiencing the fullness of God.*

CHAPTER 4: OBEDIENCE THROUGH JESUS

How can I live in joyful obedience? What are the characteristics of faithful obedience? Why is it a joy?

You can read, download and sent this booklet to a friend free of charge from
www.steps-to-personal-revival.info

Ndugu mpendwa mtendakazi mwenzangu,

Kwa sasa nachunga makanisa mawili huko California. Mara ya kwanza kupata mafundisho yenu kwa kumsikiliza Mchungaji Dwight Nelson [angalia hapa chini] katika mfululizo wa mawasilisho yake ya kila juma. Yalibadilisha kabisa roho yangu tangu mwanzo. Hapo kabla nilikuwa nimesikiliza mafundisho mengine juu ya Roho Mtakatifu, lakini nakiri kwamba sikuwahi kamwe kuyazingatia sana. Naamini kabisa kwamba kwa sababu fulani, Mungu amechagua wakati huu wa sasa ili kuwafikia watu wengi zaidi kupitia Roho Mtakatifu. Nami nina furaha kwamba nimempata kutokana na juhudzi zako.

Kwa sasa nachunga makanisa mawili huko California. Mara ya kwanza kupata mafundisho yenu kwa kumsikiliza Mchungaji Dwight Nelson [angalia hapa chini] katika mfululizo wa mawasilisho yake ya kila juma. Yalibadilisha kabisa roho yangu tangu mwanzo. Hapo kabla nilikuwa nimesikiliza mafundisho mengine juu ya Roho Mtakatifu, lakini nakiri kwamba sikuwahi kamwe kuyazingatia sana. Naamini kabisa kwamba kwa sababu fulani, Mungu amechagua wakati huu wa sasa ili kuwafikia watu wengi zaidi kupitia Roho Mtakatifu. Nami nina furaha kwamba nimempata kutokana na juhudzi zako!

Dondoo D.R. Jan. 2018

Mchungaji Dwight Nelson, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa Pioneer Memorial – Chuo Kikuu cha Andrews, alieleza kwamba kitabu hiki kidogo [Hatua za Uamsho Binafsi] “kilibadilisha maisha yangu ya ndani. Nataka kifanye vivyo hivyo kwa ajili yako”.

Alihubiri mfululizo wa mahubiri matatu:

“Hatua ya Msingi na Matengenezo Mapya: Jinsi gani ya kubatizwa kupitia Roho Mtakatifu?”

Alinukuu kutoka katika “Hatua za Uamsho Binafsi” na kukipendekeza kwa watu. Hiyo ilisababisha kupakuliwa mara 4,000 na kufanyika oda ya maelfu ya vitabu. Kiunganishi cha mahubiri haya na blogu yake: <https://www.pmcchurch.tv/sermons> (Sept. 2, Sept. 9, Sept. 23)

Ushuhuda wake binafsi na mahubiri matatu vipo katika:

www.steps-to-personal-revival.info

Hatua ZA UAMSHO BINAFSI

Helmut Haubeil ni mfanyabiashara na mchunganji. Baada ya kufanya ufanisi kwa kompani ya kusafirisha, akiwa na umri wa miaka 37 alikubali wito wa Mungu ili kujiunga na uchungaji, naye akatumika kama mchungaji kwa miaka 16. Baadaye alikuwa mkurugenzi wa kituo cha uuguzi cha Kiadventista huko Bad Aibling, Ujerumani. Yeye ndiye mwasihi na mhariri wa “Missionsbrief” (gazeti la utume katika lugha ya Kijerumani) na tangu astaafu ametenda jukumu muhimu sana katika kusaidia kujenga kazi ya misheni huko Asia kati na India.

“Kwa nini hatupati njaa na kin kwa ajili ya karuma ya Roho, kwa kuwa hii ndiyo njia ambayo kwayo tinapaswa kupokea nguvu?

Kwa nini hatumzungumzii, hatuombi kwa ajili yake, hatuhubiri juu yake?”

ELLEN G. WHITE, TESTIMONIES FOR THE CHURCH, VOL. 8, P. 22